ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1. Mhe. Ali Abdalla Ali	Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini.
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni.
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake.
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais.
5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani.
6. Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais.
7. Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu.
8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa na Rais.
13.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
14.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais.
15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.
16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.
17.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe.

18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni.
19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi.
21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole.
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.
25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
26.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi.
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae.
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake.
32.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu.
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais

37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
56.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
57.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
58.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
59.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
60.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
61.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
62.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani

63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
66.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
67.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
68.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
69.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
70.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
71.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
72.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Ndugu Yahya Khamis Hamad	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 30 Mei, 2014

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika, (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuweka mezani hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka 2014/2015. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Ussi Jecha Simai (Mwenyekiti, wa Kamati ya Katiba na Sheria): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha hati mezani inayohusu hotuba ya Maoni ya Kamati ya Katiba Sheria na Utawala kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka 2014/2015. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam.18.

Mkakati wa Kuondoa Msongamano wa Magari eneo la Bandari ya Abiria Malindi

Mhe. Saleh Nassor Juma (Kny: Mhe. Jaku Hashim Ayoub) – Aliuliza:-

Kumekuwa na msongamano mkubwa wa magari na watu katika eneo la bandari ya abiria Malindi, unaosababisha usumbufu mkubwa kwa wananchi hasa wanapotoka ofisini nyakati za jioni. Kwa kuwa ni kawaida kwa Serikali, kama ilivyowahi kusemwa na Mawaziri humu Barazani kuwa huyafunga maeneo ambayo husababisha msongamano wa magari kama vile Darajani, Forodha Mchanga na kadhalika.

(a) Kwa nini eneo hili la Bandari ya abiria Malindi limekuwa likiachwa msongamano uendelee.

(b) Hatua gani za dharura na muda mrefu, zinachukuliwa au zinakusudiwa kuchukuliwa ili kuondoa msongamano huo unaosababisha wafanyakazi wengi wa Serikali na taasisi nyengine kusumbuka na hata kuchelewa kufika majumbani mwao mapema.

Mhe. Naibu Waziri wa Mindombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 18 lenye kifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mjumbe naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mhe. Spika, barabara husika anayozungumzia Mhe. Mwakilishi imejengwa muda mrefu ambapo ukitokea eneo la Polisi Malindi kuelekea bandarini, eneo la *round about* ni eneo ambalo hutumiwa na magari mengi sana kwa wakati mmoja, wakiwemo wasafiri pamoja na magari ya mizigo yanayoingia katika lango kuu la Bandari yetu ya Malindi. Aidha, kutoka usawa huo wa lango kuu la Bandari mpaka eneo la *Mercury Hotel* napo pia imekuwa ndiyo barabara kuu kwa waendao kufuata huduma kadhaa katikati ya Mji Mkongwe, Forodhani au Shangani. Pamoja na ujenzi wa jengo jipya la abiria kuzingatia maegesho maalumu ikiwemo kituo cha *taxi* kwa ajili ya bandari. Bado suala la maegesho hasa kwa wasafiri na *taxi* bubu imekuwa tatizo.

a) Mhe. Spika, Wizara ya Miundombinu kwa kushirikiana na Bandari tunaendelea kuwataka wananchi wote kufuata taratibu husika za maegesho katika eneo hilo ili kuondosha usumbufu unaojitokeza.

Mhe. Spika, ni kwamba serikali haijaliachia suala hilo na bado tunaendelea kulifanyia kazi kuona usumbufu huo unaondoka. Tukiendelea hivyo tunafanya kila jitihada kuona tunawezaje kuzuia magari yasiingie bandarini ya abiria ama kuongeza maegesho bila ya kuleta usumbufu kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, tunaangalia kama kuna uwezekano wa kusimamia magari yenye ukubwa maalum kuingia katika Bandari ya abiria, msongamano uliopo unatokana na wembamba wa barabara pia kuongezeka kwa watumiaji wa magari na vyombo vya moto.

b) Mhe. Spika, hatua za dharura ni kuongeza nguvu ya wafanyakazi wakiwemo Jeshi la Polisi hasa usalama barabarani ili kusimamia taratibu za uingizaji na utumiaji bora zaidi ya barabara na eneo husika la bandari kwa lengo la kuondoa mrundikano na msongamano wa magari katika eneo hilo. Bila shaka mpango wa kudumu ni taratibu na mipango yetu ya serikali ya kujenga Bandari kubwa ya mizigo katika eneo la Mpigaduri.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri naomba kwa masikitiko makubwa sana niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri amekiri kwamba moja kati ya mambo yanayosababisha msongamano ni pale *round about* ya Malindi, na kwa kuwa pale kulikuwa na taa za kuongoza misafara ya magari (*traffic lights*) lakini kwa sasa zimeondoshwa jambo ambalo linaweza likasababisha vile vile zogo na vurumai barabarani pale.

a) Je, ni lini zile *traffic lights* pale watazirejesha ili kuweza kuongoza gari vizuri.

b) Kwa kuwa msongamano kama ule ulikuwepo Forodha Mchanga ambapo ulisababishwa na ma-*slab* yale yaliyowekwa *concrete slabs* baada ya kuziondosha hizo *concrete slabs* zile mumezihamishia katika barabara ya Malindi/Bandarini. Hamuoni kwamba nazo zile *concrete slabs* ni tatizo kwa kusababisha misongamano pale.

c) Kwa kuwa njia pekee za kuingia na kutoka wageni kwa sababu sisi ni kisiwa ni bandari ya Malindi na *airport* hizi za Pemba na hii Unguja, hamuoni kuendelea kusababisha vurumai kwa wasafiri wanaoingia au wageni wanaoingia ikiwa ni pamoja na watalii, hamuoni kwamba linaweza likasababisha watalii hawa wakavunjika moyo kuja Zanzibar na hatimaye kuteremka kwa uchumi wetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Mindombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, ni kweli kwamba tumezungumzia suala la *round about* lakini *round about* tuliyokuwa tukizungumzia ni *round about* ya kuingilia lango kuu la bandari ya Malindi. Lakini swali lako la nyongeza umeulizia habari ya *round about* iliyoko Malindi katika barabara ya Malawi. Sasa taarifa ni kwamba *round about* iliyoko Malindi katika barabara ya Malawi ni kweli kwamba palikuwa pana *traffic light*, na ni kweli kwamba tumeziondosha na hatukuziondosha kwa utashi huo, tumeziondosha kwa sababu zilikuwa zimeshakuwa mbovu hazitoi huduma iliyokusudiwa.

Hatua iliyofikiwa na serikali ni kwamba serikali tayari imeshaingia mkataba na Kampuni ya *ACT* ya Dar es Salaam ambao ndiyo mabingwa wa uwekaji wa taa hizi, na tunaamini kwamba wataweka taa nzuri za kisasa na za *solar* kwa ajili ya kutoa huduma hiyo, tutaweka hapo Malindi, tutaweka Mkunazini, tutaweka Mwanakwerekwe eneo la barabara ya Mombasa kuunganisha na barabara inayokwenda Jang'ombe.
Kwa hiyo, matarajio yetu katika bajeti hii 2014/2015 taa hizi zitawekwa ili kuweza kutoa huduma kwa wananchi wetu wanaotumia barabara.

Suala la pili ni kweli kwamba *concrete slabs* zilizokuwa zimewekwa Forodha Mchanga zilikuwa zimewekwa na zimezuia barabara kwamba usipite, *concrete slabs* zilizowekwa sasa hivi eneo la Bandarini zimejaribu kufanya *partition* kwa ajili ya kugawanya barabara wanaopita kwenda Mjini waende na anayetoka Mjini aweze kupita. Kwa hiyo, mimi naamini pamoja na makoseo ya kuwekwa *slabs* zile lakini maudhui ni mazuri, tunachoweza kukifanya sisi ni kutafuta namna nzuri zaidi ya kuweza kugawanya barabara ile ikiwa aidha kwa kuweka rangi kama inavyokubalika katika viwango vya kimaitafa au kuweka mawe maalum yale madogo yenye ishara ya kuleta *reflector* kwa ajili ya kuongoza watu vizuri zaidi hasa nyakati za usiku. Tunatambua kwamba jiwe lile lililowekwa ukifika wakati wa usiku taa zikipiga hazina *reflector* inaweza ikawaka sisi

wenyewe tunajua kwamba mawe yale uwekwaji wake hayakuzingatia viwango vinavyostahiki na tunahakikisha kwamba tutatafuta njia nyengine mbadala ya kuweza kugawanya barabara ile ili kuweza kuhuisha huduma za usafiri na usalama barabarani.

Suala la tatu unazungumzia suala la vurugu, sisi tunasema kwamba kuna tatizo la maeneo ya maegesho kwa eneo la bandarini, tunahakikisha kwamba kama wafanyakazi wetu watafanya kazi vizuri wakiwemo Jeshi la Polisi taratibu wanazozitoa wakiweza kuzisimamia tunaweza tukapunguza kwa sehemu kubwa msongamano hasa na tatizo la *parking*. Kwa sababu tatizo jengine ni kwamba kweli kuna wenzetu hawa wenye *taxi* bubu imekuwa nao ni tatizo, kwa sababu zile *taxi* za pale Bandarini zina maegesho maalum, lakini *taxi* bubu wamekuwa wasumbufu. Kwa hiyo, tunaamini kwamba kama wenzetu Jeshi la Polisi litasimamia vizuri tatizo hili kwa sehemu kubwa linaweza likapungua na kuweza kuimarisha huduma nzuri zaidi kwa watumiaji wa eneo la bandari.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii kuweza kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri katika jibu mama alikiri kuwa kweli ile barabara ingali nyembamba na ndiyo maana inaleta msongamano.

a) Je, Mheshimiwa kuongeza mawe yale huoni unaendeleza kuwa hii barabara unaifinya zaidi iwe nyembamba.

b) Mheshimiwa ni nani hasa aliyeweka mawe yale kati ya Manispaa na nyinyi watu wa barabara.

Mhe. Naibu Waziri wa Mindombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, tumeeleza katika jibu mama kwamba ni kweli mawe yale ukifanya *partition* barabara utakuwa unaifinya eneo lake. Na ni kweli kwamba tunalazimika kufanya utaratibu mwengine wa kugawanya barabara ile ikiwa pamoja na kuweka rangi ama yale mawe madogo madogo yenye *reflector* kwa ajili ya kuhuisha usalama lakini pia kuongeza eneo.

Suala la pili ni kwamba Mhe. Spika, kwa mujibu wa taratibu na sheria za nchi jukumu la Wizara ya Miundombinu ni kujenga na barabara zinazokuwa katika maeneo ya Manispaa mwenye dhamana ya kutunza ni Baraza la Manispaa. Kwa hiyo, naamini yaliyofanyika ni maamuzi ya serikali kwa kushirikiana na taasisi zote.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwanza napenda kumshukuru sana na kumpongeza Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo ameyajibu hivi punde kujibu swali la nyongeza la Mhe. Makame Mshimba Mbarouk.

Ni kweli serikali inafanya kazi kwa pamoja kama alivyoeleza Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, lakini sababu kubwa zilizosababisha kuwekwa kwa mawe yale ni kutokana na tukio lililokuwa limetokea katika eneo la Vuga au Shangani karibu na Ofisi ya Katiba, Sheria na Utawala ambayo liliporomoka jengo kubwa sana, hivyo serikali ikalazimika kuifunga njia na kuifungua njia rasmi inayopita mbele ya upande wa pwani wa eneo la Forodhani na njia ile ya Malindi ikawa inaruhusiwa badala ya kurudi tu ikawa inaruhusiwa kwenda na kurudi ili kuwarahishia wananchi au madereva kupita kwa usalama zaidi.

Na kama tusingefanya vile katika eneo lile la Bandari maana yake pangekuwa na vurugu zaidi na hapa pia tungepata maswali kwa nini vurugu lile lipo. Kwa hiyo, jambo lile lilifanyika kwa nia njema kwa jambo la dharura, lakini mara tu baada ya dharura hiyo itakapomalizika basi mawe yale yataondoshwa na utarejea utaratibu uliokuwepo tokea awali.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Spika, kwanza nichukue nafasi hii ya kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha kufika hapa katika hali ya usalama na afya, lakini pia nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii.
Mhe. Spika, kwa kuwa ile ni Bandari Kuu ambayo kila kitu kinakuwepo pale, na kwa kuwa tuliwaombea sisi wale wenye *taxi* ili wapangwe vizuri ili ile njia iweze kupitika.

Je, haya magari ambayo yako chini ya ofisi yao itakuwa kuwaje ni vyema wakashirikiana na usalama barabarani ili kuhakikisha huu upande huu hakukai gari hata moja, atatwambiaje Mhe. Naibu Waziri kuhusu suala hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Mindombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, tatizo kubwa liliopo ni kwamba barabara ni nyembamba na watumiaji wamekuwa wengi, kwa hiyo ili tuweze kupata ufumbuzi katika tatizo hili lazima watumiaji wapate maelekezo ya wasimamizi wa usalama barabarani. Tunaamini kwamba Jeshi la Polisi, watu wetu wa usalama masuala ya bandari wakikaa pamoja jambo hili litapata ufumbuzi, kwa sababu barabara ile haizidi mita 9 upana, lakini matumizi yake yanakuwa barabara tatu kwa maana ya magari matatu yanataka yapite kwa wakati mmoja na kwa humu pembeni kuna watu wanaegesha magari.

Kwa hiyo, la kwanza kuondosha wale watu wanaoegesha magari pembeni, la pili kusimamia kuonesha kwamba hakuna gari inayosimama au kukatisha basi tunaamini kwamba tukiweza kusimamia hivyo tutapunguza kwa sehemu kubwa msongamano na matatizo haya ya wanaotumia barabara kwa ajili ya safari zao.

Nam. 51

Kuimarisha Mchezo wa Riadha Zanzibar

Mhe. Saleh Nassor Juma – Aliuliza:-

Mchezo wa riadha ni moja katika michezo inayopendwa sana ulimwenguni, aidha mchezo huu umesaidia sana kuyatangaza mataifa mengi duniani kama vile Kenya, Ethiopia na kadhalika.

Kwa kuwa Zanzibar ni wapenzi wakubwa wa mchezo wa mpira wa miguu huku timu zetu zikiendelea kufanya vibaya siku hadi siku.

Je, ni lini Serikali itaamua kuwekeza katika mchezo wa riadha, ili kutoa nafasi kwa vijana wetu kujaribu bahati katika aina nyengine ya michezo badala ya kung'ang'ania mpira wa miguu usiokuwa na tija kwao pamoja na nchi yetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 51 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, mchezo wa riadha ni miongoni mwa michezo muhimu na unaopendwa sana ulimwenguni, na ni kweli mchezo wa riadha umesaidia kuyatangaza Mataifa mengi duniani kama vile Kenya, Ethiopia, Jamaica na kadhalika.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa makusudi iliamua kufanya matengenezo makubwa katika Uwanja wa Amani yaliyohusisha pia njia ya kukimbilia (*running track*) pamoja na kukipatia vifaa vya michezo Chama kinachosimamia mchezo wa riadha nchini kutoka Serikali ya Ujerumani kwa lengo la kuwawezesha vijana wetu kupata fursa zaidi za kushiriki na kuimarisha mchezo huo nchini.

Mhe. Spika, aidha jitihada za kumpata mtaalamu wa kufundisha mchezo huo kutoka Ujerumani bado zinaendelea na zina sura ya matumaini.

Mhe. Spika, kwa upande wa Uwanja wa Gombani, tayari jitihada na taratibu za uwekaji wa njia ya kukimbilia ya kisasa zimeanza na kukamilika kwake kutawapatia fursa vijana wetu kukuza vipaji vyao na kuweza kupeperusha vyema bendera ya nchi yetu katika mashindano ya kimataifa.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri napenda niulize swali dogo tu la nyongeza. Kwanza niipongeze serikali kwa kutaka kufanya viwanja vyetu kuvitia hiyo sehemu ya kukimbilia, pamoja na jitihada za muda mrefu ambazo hadi leo hazijafanikiwa za kuweza kuleta kocha kutoka Ujerumani.

Mhe. Spika, kwa kuwa wenzetu Waethiopia wanafanya vizuri sana katika medani hii ya riadha katika tasnia ya kimataifa, na kwa kuwa siku moja wakati nipo Kilimanjaro pale niliwaona wanariadha Waethiopia wameondoka kwao Addis-ababa kuja pale kufanya mazoezi ya kupanda ule mlima na kushuka huku wakipata baridi kali ili kufanya waoane na mazingira ya nchi wanayokwenda kushindana.

(a) Je, serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia wizara yako Mhe. Naibu Waziri mmewafanyisha ziara ngapi wanamichezo wetu hawa kwenda nchi za nje ili kuweza kujikita katika hali za hewa za nchi hizo katika mashindano ya kimataifa.

(b) Ni lini Mhe. Naibu Waziri utaishawishi serikali yetu hii kutia mtaala wa mambo haya ya *athletics* katika skuli zetu hizi za msingi na sekondari.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kwanza kabisa nimshukuru Mhe. Saleh Nassor Juma kwa kuweza kuniuliza maswali mawili ambayo yana tija kwa wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, mwaka juzi tulikuwa na kijana wetu ambaye ni mlemavu kwa kweli alituletea medali ya dhahabu, na nataka nimwambie Mhe. Mwakilishi tutaendelea kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili kuwawezesha vijana wetu, licha ya huyo mlemavu na hata wale waliokuwa si walemavu.

Mhe. Spika, swali lake la pili nataka nimwambie Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali tumeshakaa ili kuweza kuingiza mitaala ya michezo Zanzibar.

Mhe. Raya Suleiman Hamad: Ahsante Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mhe. Naibu Waziri na vile vile pia nimpongeze, naomba nimuulize swali dogo tu la nyongeza. Je, ni lini wataweza kuvijenga au kuviimarisha viwanja vya wilaya; Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, nataka nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba ameuliza swali hili kwa upeo zaidi na mimi nitamjibu kama inavyohitajika. Sasa hivi nataka nimwambie mwezi huu Katibu wetu wa Baraza la Michezo kwa kushirikiana na Wizara alitembelea mikoa yote ile tuliyoahidi kama itajengwa viwanja vya wilaya, alikuwepo hapa Unguja na akaenda Micheweni na Wilaya ya Wete pamoja na Wilaya ya Mkoani.

Namhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba, wizara yetu suala hili kwa kushirikiana na serikali iliahidi, na kwa kweli viwanja hivi vitajengwa usiwe na wasi wasi na vijana wako walemavu watapata maeneo ambayo wataweza kufanya mazoezi yao.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mchezo wa riadha ni mchezo ambao umeiletea sifa kubwa sana Zanzibar kipindi cha nyuma, hata Rais wetu wa Zanzibar alikuwa ni mkimbiaji mahiri wa mbio hizi za riadha. Halikadhalika kaka yetu Mzee Suleiman Ame Nyambui aliiletea sifa kubwa sana Zanzibar katika mashindano ya huko nyuma.

Je, Zanzibar ni mwaka gani wa mwisho wakimbiaji wetu wa riadha walishiriki katika mashindano ya kimataifa na kuleta kikombe hapa Zanzibar. Kama walishiriki ni mkimbiaji gani ambaye alituletea sifa ya mwisho Zanzibar katika mashindano haya ya riadha.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, ni kweli kwamba mchezo huu una uwezekano mkubwa wa kuipa heshima Zanzibar na huko nyuma tulifanya vizuri na bado matumaini ya kufanya vizuri yapo, ndio tukaamua kwamba chama hiki tukiimarishe vizuri na tukaweka safu nzuri ya uongozi akiwemo Mhe. Makame Mshimba Mbarouk kama Rais wa Chama cha Riadha Zanzibar.

Kwa hivyo, matumaini yangu ni kwamba, kwa umahiri wa Mhe. Makame Mshimba Mbarouk basi sasa chama hiki kitapata nafasi nzuri na Wazanzibari watakuwa ni miongoni mwa watu wanaofanya vizuri sana katika mashindano ya kimataifa, asiwe na wasiwasi hata kidogo, nina watu wa kunisaidia vizuri sana.

Kuhusu mashindano ya kimataifa tunafanya vizuri, nakumbuka hata mwaka jana Bi Sara Ramadhan ametuletea sifa nzuri hapa Zanzibar. Kwa hiyo, tunaendelea vizuri wasiwe na wasiwasi.

Nam. 19

Utafiti wa Magonjwa ya Saratani kwa Wanawake

Mhe. Saleh Nassor Juma (Kny: Mhe. Jaku Hashim Ayoub) – Aliuliza:-

Kumekuwa na ongezeko kubwa la wagonjwa wa Saratani hasa kwa wanawake, ambapo kampeni mbali mbali zimekuwa zikifanyika katika kusaidia kupambana na ongezeko hilo hapa nchini.

(a) Je, serikali imefanya utafiti gani na kugundua sababu ya ongezeko la magonjwa hayo kwa wanawake.

(b) Je, ni magonjwa yepi ya saratani yanawasumbua sana wanawake na serikali inatoa kauli ipi kwa wanawake kujikinga nayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 19 (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kumekuwa na hali ya ongezeko kubwa la wagonjwa wa saratani ulimwenguni kwa jinsia zote na umri wote. Kwa wanawake, na kwa kuwa wao ni wanawake na ndio maana wanaathirika zaidi na saratani za shingo ya kizazi (*cervical cancer*).

Sababu ya ongezeko la maradhi haya ni sehemu jinsia yao, anaishije, historia ya kuugua maradhi mbali mbali hasa ya kujamiiana mara kwa mara, na kuwepo kwa virusi vya *HPV* (*human papillomavirus*) vinavyoongeza nafasi ya kupata tatizo hili. Asilimia kubwa ya akina mama wanaogunduliwa kuugua saratani ya shingo ya kizazi hutambulika katika hatua za mwisho baada ya kuathirika, hali inayopelekea akina mama wengi kupoteza maisha.

Mhe. Spika, theluthi mbili ya wagonjwa wetu wa saratani wanaonekana katika hospitali maalum ya kuchunguza na kutibu saratani ya *Ocean Road* wanasumbuliwa na saratani ya shingo ya kizazi kwa mujibu wa ripoti ya *Ocean Road* ya mwaka 2009. Pia taarifa zilizopo ambazo zilikusanywa katika ukanda wa Afrika Mashariki zinathibitisha habari hizo kwa ukanda mzima. Hali inayoonesha kwamba, kiwango cha saratani ya shingo ya kizazi ni asilimia kama 43 kwa kila watu 100,000, na kwa kila mwaka kumekuwa na ongezeko la zaidi ya wagonjwa wapya 45,000 na wanawake zaidi ya 28,000 wanakufa kutokana na saratani ya shingo ya kizazi. Lakini kutoka takwimu zilizokusanywa katika hospitali mbali mbali hapa Zanzibar, taarifa kutoka kitengo chetu cha kutunza taarifa (*HMIS*) zinaonesha kwamba kuna kati ya kesi mpya 62-82 za saratani ya shingo ya kizazi kwa mwaka. Maelezo hayo yanatupa picha halisi ya hali ya saratani ya shingo ya kizazi inavyowaathiri wanawake wa Zanzibar.

Mhe Spika, kauli ya serikali kwa wanawake ni kujikinga na tatizo la saratani ya kizazi kwa kuzitumia huduma za uchunguzi ambazo zinafanyika katika matukio mbali mbali kama vile siku ya Afya ya Kijiji (*Village health days*), katika kliniki za wajawazito hasa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja na hata katika maadhimisho ya siku ya wauguzi duniani. Shughuli hizo zote zinalenga kuweza kugundua mapema saratani ya shingo ya kizazi kwa akina mama.

Aidha, pamoja na kuwa elimu ya afya imekuwa ikitolewa sana katika kliniki za mama na watoto, bado wizara inasisitiza wanawake kutumia fursa ya kuchunguza afya zao kila pale inapotokea.

Kuna njia tatu ambazo serikali inawashauri kina mama kujikinga na saratani ya shingo ya kizazi

(i)Kuwapatia chanjo ya kinga watoto wote wa kike wenye umri kuanzia miaka 9 hadi 13 (*HPV*) *Vaccine* ambapo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaanza kutoa chanjo hiyo kuanzia mwaka 2015.

(ii)Kufanyiwa uchunguzi kina mama wote wenye umri wa kuanzia miaka 30 na zaidi na kuwapatia matibabu wale wote watakao gundulika na ugojwa huo.

(iii)Kuwapatia matibabu stahiki wale wote walioathirika na ugonjwa huo katika hospitali maalum za kutibu magonjwa hayo.

Pamoja na yote hayo kufanyika, wizara bado imo katika kufanya jitihada zaidi ili kuwanusuru wanawake na janga hilo na kuhakikisha inatoa suluhisho sahihi ya tatizo hili. Kwa kupitia Kitengo cha Kudhibiti Magonjwa yasiyoambukiza pamoja na wataalamu wazalendo walio nje ya nchi, tayari "*proposal*" ya kufanya utafiti limeshatekelezwa, linalotakiwa kubaini ukubwa wa tatizo na aina ya virusi vya *HPV* vinavyopatikana hapa Zanzibar imekamilika na jitihada za kutafuta wafadhili wa utafiti huo zinaendelea.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kama lugha aliyoitumia kujibu hili swali la msingi na mimi naomba atumie lugha hiyo hiyo ya busara na nasaha katika kulijibu swali langu la nyongeza.

Baada ya maelezo hayo naomba kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa ulimwengu mzima nchi zote zina mpango wa kuzuia vifo vya mama na watoto, ni *millenium goals;* moja ni kwa kiasi fulani kupunguza vifo vya mama na mtoto, na kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri amekiri kwamba hili suala la saratani ya shingo ya uzazi huwa inagundulikana katika hatua ya mwisho ambapo kuizuia tena inakuwa shida.

Je, ni tatizo gani ambalo wataalamu wetu hapa Zanzibar wanalo mpaka wakafanya kwamba hii ionekane katika hatua za mwisho na sio hatua za awali na wakati hawa akinamama wengi kwa sasa asilimia zaidi ya 70 kwa mujibu wa takwimu nilizozichukua hivi karibuni wanakwenda katika vituo vya afya kupima ujauzito pamoja na kuwapeleka watoto wao kupimwa kule. Hilo la kwanza.

Pili, kwa kuwa akinamama vile vile hupata tatizo sana la kensa za matiti na kupelekea matiti yao kukatwa, jambo ambalo linaweza likapelekea vifo vya watoto wachanga na kushindwa ku-*achieve* ile *millenium goals* ya *reduction of mother-child mortality rate*. Je, serikali ina mpango gani sasa wa kuweza kupata mashine bora na za kisasa kama zilizopo *Ocean Road* wakaziweka hapa Unguja Mjini na nyengine wakazipeleka pale Chake Chake Pemba ili wasipate shida hawa kinamama kusafiri kwenda Dar es Salaam kwenda *Ocean Road* kupimwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kugundulika mwisho sio tatizo letu serikali ni tatizo la wagonjwa kuripoti katika hatua ya mwisho. Kama unavyofahamu hii ni sehemu ya ugonjwa inayohusisha sehemu nyeti ya binadamu, si wanawake wengi wanaopenda kujitokeza mapema yanapoanza matatizo hayo. Wengi wanakuwa wanafahamu lakini kwanza ile dhana ya kukubali kwamba ni tatizo hilo kwao inakuwa ni tatizo na si kwa maradhi hayo tu, kwa maradhi mengi tu watu huwa hawakubali.

Ukimwambia mtu una sukari anajisaili mara mbili au tatu sikwambii tatizo kama hili, wanayaona mapema, dalili zinajitokeza mapema, lakini hawaripoti mapema. Kwa hiyo, kwa wale wanaokuja nimesema hapa, wanaokuja kliniki haya yanasomeshwa na wanachunguzwa. Wako wawili watatu wanaogundulika mapema na wanatibiwa mapema, na ukitibiwa mapema tatizo hili linakuwa sio tatizo, kwa sababu ni suala la kufanyiwa operesheni na kupata matibabu mengine ya ziada ambayo yanaweza yakakufanya bado ukawa mzima ukaendelea kuishi vizuri.

Kwa hivyo, sio sisi tunaochelewa isipokuwa wagonjwa. Sasa ndio maana tukasema kwamba wanawake hasa kuanzia miaka 30 na kuendelea mbele wote wazitumie fursa tunazozitoa ili kwenda kupimwa kwa sababu hata watakapokuja kujigundua kwa yale madogo madogo tu wanayoyaona wakishaanza kujisikia wasiwasi waje, lakini hata kama huna wasiwasi uje kwa sababu utakapokuja utachunguzwa, ukigundulikana mapema hutafikia hatua hiyo na unaweza maisha yako yakaweza kuokolewa.

Suala la pili kuhusu saratani ya matiti. Saratani ya matiti sasa hivi karibu ma-*nurse* wote walioko kwenye vituo wanaweza kuchunguza hili, wameshafundishwa na wanaendelea kufundishwa ili waweze kuwagundua wagonjwa. Na si lazima awe *nurse* tu, tunawafahamisha mtu yeyote mwanamke anaweza kujichunguza mwenyewe saratani ya matiti bila ya kwenda kwa daktari. Kwa hiyo, wafike katika vituo zinapotolewa huduma hizi, wakati wa wito wa kampeni pia waweze kufika waende wakachunguzwe. Na kwenye televisheni, kwenye redio siku hizi ukitizama utaona bado matatizo haya yanaelezwa na jinsi gani ya kujitambua na jinsi gani ya kujichunguza. Wajitahidi waangalie vipindi vya habari tusiangalie taarabu tu, vipindi kama hivi vya kuelimisha jamii ni vizuri kwa ajili ya afya zao.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, na mimi kuniona ukanipa fursa nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri kakiri kama tatizo la saratani ya shingo ya uzazi lipo kwa wingi katika nchi yetu na kila mwaka anasema huwa wanapata wagonjwa zaidi ya 40. Kwa hivyo,

namuuliza Mhe. Naibu Waziri je, kwa kuwa suala hili lipo tuna wataalamu wangapi yaani madaktari ambao wanaweza kugundua wakajua hii ni saratani ya shingo ya uzazi katika nchi yetu ya Zanzibar. Na je, katika hao madaktari tulionao wanawake ni wangapi na wanaume ni wangapi, kwa kuwa ametueleza kuwa tatizo hilo linakuwa sehemu nyeti za siri.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kwa kulishughulikia suala hili kuna manesi wengi ambao wamefundishwa wanaweza kuchunguza na kuweza kuwaambia. Kwa hiyo wanaweza kupunguza na wanaweza wakaongeza. Kwa hiyo Kitengo cha Maradhi yasiyoambukiza kimeshatayarisha sehemu za hospitali kama 35 ambazo ni za *PHU Class,* ambapo kila hospitali kama hiyo iliyotengwa watu wanafundishwa hilo na wataweza kupunguza. Sasa hivi wapo katika mafunzo baadae watu watakapokuwa tayari watatangaziwa na wataweza kwenda huko wasiwe na wasiwasi.

Lakini tunaandaa kitengo hichi katika vitengo ambavyo vitakavyokuwa Mnazi Mmoja Hospitali kama Hospitali ya Rufaa, kitengo hichi kitakuwepo maalum, kwa hiyo shughuli zote zile za matibabu na operesheni zinaweza zikafanyika hapa kwa yale matibabu ya vidonge na operesheni. Na hatua za mbele ikiwezekana pia tutaweza kutibu kwa mionzi. Lakini hilo litachukua muda kidogo, kwa sababu tunahitaji maandalizi na pahala maalum kwa ajili hiyo.

Maandalizi ya madaktari, hivi sasa kuna daktari mmoja mwanamke na mwanamme ambao wapo katika hospitali mmoja Muhimbili, mmoja *Ocean Road* wanasomea mambo hayo. Tunategemea mmoja atakuwepo nchini mwakani mwaka, huu anamaliza. Lakini linapokuja suala la madaktari, madaktari wanaotizama matatizo nyeti karibu wote au wengi ni wanaume kwa sababu ndio wanaotaka kufanya kazi hiyo. Sio kwa sababu tu ni wanaume, hao ndio wanaopendelea kusoma hayo masomo kwa kuwa wanawake hatuyapendi. Na usisikie Mhe. Subeit Khamis Faki mgonjwa anayeumwa wala hana haja, huyo mwanamme hata akimuangalia kwa kweli hatomshughulisha.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa udi ni manukato ambayo wanawake wengi wanapenda kuyatumia. Na kwa kuwa wanawake wengi wanatishana na kujengeana khofu kama udi unasababisha ugonjwa huu wa *cancer*. Je, Mhe. Waziri suala hili ni kweli. Na kama ni kweli, kuna utaratibu gani unaofanyika. Je, Wizara yako inawaambia nini wanawake kuhusu manukato haya.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, nimesema kinachosababisha maradhi haya kwanza unatakiwa uwe mwanamke, unaishi vipi. Sasa sijui kama hiyo unaishi vipi kuna mahusiano na udi. Maana yake ukiwa unakitumia kiungo chako vibaya ndivyo nilivyokusudia unaishi vipi. Kwa sababu watu ambao wanafanya biashara ya ngono hao wanaathirika zaidi. Hapa ndipo nilipokusudia. Lakini kundi hilo hilo mara nyingi ndilo linalougua maradhi ya kujamiiana mara kwa mara, kwa sababu wanakuwa hawajilindi au wateja wao wanakuwa mara nyingi hawataki kujilinda. Sasa kunakuwa na virusi vya *Human Papilloma Virus (HPV),* hilo ndilo kundi la virusi linalosababisha watu wengi wavipate.

Sasa Mhe. Spika, udi na virusi sijui kama vina mahusiano; hatujawahi kufanya utafiti, kwa sababu katika tafiti zilizofanywa hicho hakimo. Lakini najiuliza huo udi huko unakwenda kufanya nini? Mimi ninavyojua udi unafukizwa nguo, unafukizwa chumba, labda wajaribu kunielimisha sijafahamu udi una uhusiano gani. Mimi si mtaalamu wa udi wala sijawahi kunukia, nakuja hapa kila siku, kwa hiyo mimi sijui kwa kweli hilo niseme. Labda Mhe. Salma Mohammed Ali anifahamishe.

Hoja za Serikali

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2014/2015 - Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu sasa likae kama Kamati kwa madhumuni ya kupokea, kujadili na hatimaye kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mhe. Spika, nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwenye wingi wa rehema, kwa kutujaalia kukutana hapa leo katika Baraza hili Tukufu tukiwa na afya njema na tukiendelea kushughulikia majukumu ya kitaifa katika hali ya amani na utulivu.

Mhe. Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, naomba kutumia nafasi hii kupitia Baraza lako Tukufu, kumshukuru na kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa uongozi wake wenye busara, hekima, uadilifu na unaothamini utu ambao umetuletea maendeleo na mafanikio makubwa kwa wananchi wa Zanzibar. Chini ya uongozi wake, Serikali imeweza kutekeleza kwa kiwango kikubwa Sera za Chama Tawala kama zilizovyoainishwa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010. Hapana shaka wananchi wa Zanzibar wanaendelea kuwa na imani na uongozi wake ambao kwa kweli umeleta matumaini katika kipindi chote cha uongozi wake. Jitihada zake zinaonekana wazi na zimeleta maendeleo makubwa ya kisiasa, kiuchumi na kijamii na kuendeleza amani na utulivu nchini.

Mhe. Spika, napenda pia kuchukua nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Makamu wa Kwanza wa Rais, Maalim Seif Sharif Hamad kwa mashirikiano na ushauri anaotupa. Pia napenda kumpongeza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi kwa kusimamia vyema shughuli za Serikali na utekelezaji wake. Aidha, nawapongeza viongozi hao kwa kumshauri na kumsaidia kwa karibu Mhe. Rais wa Zanzibar katika utekelezaji wa majukumu yake. Pia miongozo yao imesaidia kufanikisha shughuli za ofisi yangu.

Mhe. Spika, naomba pia kuchukua nafasi hii adhimu kukupongeza wewe binafsi kwa kuliongoza Baraza hili Tukufu kwa hekima, busara na uadilifu. Umakini ulionao katika uongozi umewezesha kuliendesha Baraza hili na umesaidia sana kuliwezesha kufanya kazi zake kwa ufanisi, ikiwemo kuishauri Serikali juu ya masuala mbali mbali yenye maslahi kwa Taifa. Nampongeza pia Naibu Spika Mhe. Ali Abdalla Ali, Mwakilishi wa Jimbo la Mfenesini, pamoja na Wenyeviti wa Baraza kwa kuendesha vyema shughuli za Baraza.

Mhe. Spika, naomba nitumie fursa hii kutoa shukrani maalum kwa Kamati ya Baraza la Wawakilishi ya Katiba, Sheria na Utawala chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Ussi Jecha Simai na Makamu wake Mhe. Abdalla Juma Abdalla ambao kwa kushirikiana na Wajumbe wote wametupa ushirikiano, ushauri, miongozo na maelekezo ambayo yamesaidia sana katika kuimarisha utekelezaji wa majukumu ya ofisi yangu.

MAJUKUMU MAKUU YA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA IDARA MAALUM ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

Mhe. Spika, kufuatia mabadiliko ya Baraza la Mawaziri tarehe 20 Agosti, 2013, yaliyofanywa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ iliundwa upya na kupewa baadhi ya majukumu ya iliyokuwa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Majukumu iliyopewa yanahusu usimamizi wa Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa, Idara Maalum za SMZ na Idara ya Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi.

Mhe. Spika, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kwa sasa ina majukumu makuu yafuatayo:-

a. Kusimamia Sera, Sheria na Kanuni mbali mbali za Ofisi.
b. Kubuni na kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo
c. Kudumisha Amani, Ulinzi na Usalama katika Mikoa na Wilaya hadi Shehia.
d. Kulinda mali za Taifa na za watu binafsi zisiharibiwe, kuzuia uingizaji au utoaji nje ya nchi kimagendo, pamoja na kusimamia kazi za uzimaji moto na uokozi.
e. Kuwasajili na kuwapa vitambulisho Wazanzibari wakaazi.
f. Kuwahifadhi kwa kufuata taratibu bora na kwa kuzingatia haki za binaadamu watuhumiwa na waliofungwa ambao wapo katika Vyuo vya Mafunzo.
g. Kuandaa na kutekeleza mipango ya kuijengea uwezo Mikoa kitaaluma na utumishi katika Mikoa.
h. Kutoa mwongozo na ushauri kwa Mikoa katika mambo ya kisheria na utaratibu, kujenga mazingira mazuri katika kuimarisha huduma za kijamii na kiuchumi katika Mikoa;
i. Kuratibu, kushauri, kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa shughuli za Serikali za Mitaa;

j. Kuimarisha Utawala Bora na kuimarisha uwezo wa Serikali za Mitaa na mamlaka zake;
k. Kufuatilia na kukagua utendaji wa Serikali za Mitaa katika utoaji wa huduma;
l. Kutoa msaada wa kiufundi na kisheria katika utoaji wa huduma za Serikali za Mitaa; na
m. Kuendeleza michezo katika Idara na Taasisi zetu.

Mhe. Spika, utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2013/2014 umezingatia Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya mwaka 2020, Awamu ya Pili ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar (MKUZA II), Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, Mpango Mkakati pamoja na Sera za Kisekta.

MUUNDO WA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA IDARA MAALUM ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

Mhe. Spika, utekelezaji wa malengo na shughuli za Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar unasimamiwa na Idara na Taasisi zilizogawika katika maeneo makuu manne (4) pamoja na Ofisi ya Ofisa Mdhamini Pemba. Idara na taasisi hizo ni kama ifuatavyo:-

a. IDARA ZA KAWAIDA

1. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti;
2. Idara ya Utumishi na Uendeshaji;
3. Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho;
4. Idara ya Uratibu wa Tawala za Mikoa; na
5. Idara ya Serikali za Mitaa;

b. MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MIKOA

6. Mkoa wa Mjini Magharibi;
7. Mkoa wa Kaskazini Unguja;
8. Mkoa wa Kusini Unguja;
9. Mkoa wa Kaskazini Pemba;
10. Mkoa wa Kusini Pemba;

c. MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA

11. Baraza la Manispaa – Unguja;
12. Baraza la Mji - Wete;
13. Baraza la Mji - Chake chake;
14. Baraza la Mji - Mkoani;
15. Halmashauri - Wilaya ya Magharibi;
16. Halmashauri - Wilaya ya Kaskazini ‘A’;
17. Halmashauri - Wilaya ya Kaskazini ‘B’;
18. Halmashauri - Wilaya ya Kati Unguja;
19. Halmashauri - Wilaya ya Kusini Unguja;
20. Halmashauri - Wilaya ya Wete;
21. Halmashauri - Wilaya ya Micheweni;
22. Halmashauri - Wilaya ya Chake Chake;
23. Halmashauri - Wilaya ya Mkoani;

d. IDARA MAALUM ZA SMZ

24. Idara ya Uratibu wa Idara Maalum za SMZ;
25. Tume ya Utumishi ya Idara Maalum za SMZ;
26. Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM);
27. Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU);

28. Idara ya Chuo cha Mafunzo (MFZ);
29. Kikosi cha Zimamoto na Uokozi Zanzibar (KZU);
30. Kikosi cha Valantia Zanzibar (KVZ).

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo ya Utangulizi, naomba sasa nichukue nafasi hii nitoe maelezo juu ya mapato na matumizi na utekelezaji wa malengo ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2013/2014 pamoja na mwelekeo wa malengo kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

MUHTASARI WA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2013/14

Mhe. Spika, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inakusanya mapato ya Serikali Kuu yanayoingia Mfuko Mkuu wa Serikali na mapato ya Serikali za Mitaa ambayo hutumiwa na Serikali hizo. Kwa upande wa mapato ya Serikali Kuu, katika mwaka wa fedha 2013/14 ilipangiwa kukusanya jumla ya TZS 121,330,000/= kupitia vianzio mbali mbali taasisi za ofisi yangu na hadi kufikia Machi 2014, jumla ya TZS 61,689,000/= zimekusanywa sawa na asilimia 61 ya lengo la mwaka. *(Angalia Kiambatanisho Namba 1)*. Kwa upande wa Serikali za Mitaa katika mwaka wa fedha 2013/14 zilipangiwa kukusanya jumla ya TZS 4,783,343,580/= na hadi kufikia Machi 2014, jumla ya TZS 2,934,237,898/=. *(Angalia Kiambatanisho Namba 2)*.

Mhe. Spika, Ofisi yangu inasimamia jumla ya mafungu saba ya kibajeti na kwa mwaka wa fedha 2013/2014, mafungu hayo yalitengewa jumla ya Shilingi 44,681,251,089 kwa kazi za kawaida. Kati ya hizo Shilingi 28,055,470,194/= ni kwa ajili ya mishahara, mchango wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na posho za wafanyakazi, Shilingi 2,061,000,000/= ni ruzuku kwa ajili ya Baraza la Manispaa na Mabaraza ya Miji, na Shilingi 13,794,780,895/= ni kwa matumizi mengineyo. Aidha, jumla ya Shilingi 770,000,000/= zilitengwa kwa kazi za Maendeleo *(Angalia Kiambatanisho Namba 3)*.

Mhe. Spika, hadi kufikia tarehe 30 Machi 2014, mafungu hayo yameingiziwa jumla ya Shilingi 32,942,525,700/= sawa na asilimia 74 ya lengo la mwaka. Kati ya hizo Shilingi 23,568,862,349/= sawa na asilimia 84 ya lengo la mwaka ni kwa ajili ya mishahara, mchango wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na posho za wafanyakazi, Shilingi 1,545,207,800/= sawa na asilimia 75 ya lengo la mwaka ni ruzuku kwa ajili ya Baraza la Manispaa na Mabaraza ya Miji, na Shilingi 7,681,145,551/= sawa na asilimia 56 ya lengo la mwaka ni kwa matumizi mengineyo. *(Angalia Kiambatanisho Namba 3)*.

Mhe. Spika, hadi kufikia mwezi wa Machi 2014, fedha zilizopatikana kutoka Mfuko wa Serikali kwa kazi za maendeleo ni Shilingi 147,310,000/= sawa na asilimia 19 ya makadirio ya mwaka. Uchanganuzi wa fedha hizo unaonekana katika *Kiambatanisho Namba 3*.

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MALENGO YALIYOPANGWA KWA MWAKA 2013/2014 NA MALENGO YA MWAKA 2014/2015 KIIDARA.

IDARA ZA MAKAO MAKUU

Mhe. Spika, baada ya kutoa muhtasari huo, naomba sasa kuelezea malengo yaliyopangwa kwa mwaka 2013/2014, kufanya mapitio ya utekelezaji wa malengo hayo pamoja na kuelezea malengo ya mwaka 2014/2015 na gharama zake kwa kila Idara au Taasisi ninayoisimamia.

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Spika, Idara hii ina jukumu la kutoa huduma na utaalamu wa uandaaji wa mipango ya maendeleo, bajeti, ufuatiliaji na tathmini ya programu na miradi, kuratibu na kusimamia uandaaji na mapitio ya Sera, Sheria, tafiti na Mipango ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Aidha, Idara inaratibu utayarishaji wa ripoti mbali mbali za utekelezaji wa majukumu ya Ofisi zikiwemo taarifa za utekelezaji wa Mpango Kazi kwa kila robo mwaka, ripoti mbali mbali zinazowasilishwa katika Kamati ya

Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza lako Tukufu pamoja na zile zilizowasilisha katika taasisi mbali mbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Malengo ya mwaka 2013/2014

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ililenga kutekeleza yafuatayo:-

i. Kuimarisha Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini;
ii. Kuimarisha uratibu na upangaji wa Programu za Ofisi;
iii. Kuimarisha ufanyaji wa tafiti za Wizara;

iv. Kuimarisha mazingira ya kisera na kisheria kwa utekelezaji wa masuala ya Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Ulinzi na Usalama; na
v. Kuimarisha uingizwaji wa masuala mtambuka katika Mipango na program za Ofisi.

Mhe. Spika, ili kutekeleza majukumu iliyojipangia katika mwaka wa fedha 2013/2014, Idara ilitengewa TZS. 118,083,000/= kwa utekelezaji wa kazi za kawaida.

Utekelezaji wa malengo ya 2013/2014

Mhe. Spika, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imefanya mapitio ya Mpango Mkakati wa iliyokuwa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na kuandaa Mpango Mkakati wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambao umeanza kutumika katika upangaji wa bajeti na mipango ya Ofisi ya mwaka wa fedha 2014/15.

Mhe. Spika, ili kujenga uwezo mzuri wa watendaji kuweza kumudu na kutekeleza vyema majukumu yao, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imetoa mafunzo maalum kwa maafisa mipango wa taasisi zote zilizo chini ya Ofisi hii. Jumla ya Maafisa 42 (wanawake 9, wanaume 33) walipatiwa mafunzo maalum ya matumizi ya kompyuta katika kutayarisha Bajeti na kuandaa taarifa mbalimbali za utekelezaji wa kazi.

Mhe. Spika, Idara imefanya ziara tatu za ufuatiliaji wa shughuli za Ofisi. Ziara moja ilifuatilia utekelezaji wa majukumu ya kazi kwa taasisi zote za Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Pemba. Ziara mbili zilifanyika kukagua utekelezaji wa miradi katika Idara Maalum za SMZ. Pia Idara imeratibu ziara za Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, Idara imeratibu utayarishaji wa Mpango wa Matumizi wa Muda wa Kati (*MTEF*) wa Ofisi pamoja na utayarishaji wa Hotuba ya Bajeti ya mwaka 2014/2015. Aidha imesimamia ukamilishwaji wa Sera ya Serikali za Mitaa kwa kufanyiwa tafsiri kwa lugha ya Kiswahili na kuchapisha nakala 500.

Mhe. Spika, Idara imeratibu ushiriki wa Ofisi katika maadhimisho ya Miaka 50 ya Mapindizi Matukufu ya Zanzibar kwa kuandaa machapisho ya taarifa mbali mbali yanayoihusu Ofisi na kushiriki kikamilifu katika Maonesho ya maadhimisho hayo. Pia Idara imeratibu utayarishaji wa miradi ya maendeleo ya taasisi zilizo chini ya Ofisi hii inayotarajiwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2014/2015.

Mhe. Spika, hadi kufikia Machi 2014, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imeingiziwa TZS. 34,277,625/= sawa na asilimia 29 ya makadirio ya matumizi ya kazi za kawaida.

Muelekeo na Malengo ya mwaka 2014/2015

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuimarisha Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini kwa shughuli za Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum.
ii. Kuimarisha uratibu na upangaji wa Programu za Ofisi pamoja na kujenga uwezo wa watendaji wa mipango;
iii. Kuhakikisha kuwa mradi inayotekelezwa na Taasisi zetu inakuwa na tija.
iv. Kuimarisha ufanyaji wa tafiti za ofisi katika maeneo ya kipaumbele kwa kushirikiana na taasisi za utafiti;
v. Kuimarisha mazingira ya kisera na kisheria kwa utekelezaji wa masuala ya Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Ulinzi na Usalama;
vi. Kuimarisha uingizwaji wa masuala mtambuka katika Mipango ya Wizara.

Mhe. Spika, ili Idara ya Mipango, Sera na Utafiti iweze kutekeleza malengo yake ipasavyo, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya TZS. 337,472,000/=, kati ya hizo 79,197,000/= ni mishahara, maposho maalum na michango ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) na TZS 258,275,000/= kwa kazi za kawaida.

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Mhe. Spika, Idara hii ina jukumu la kutoa na kusimamia huduma za uendeshaji na utumishi katika Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara maalum, zikiwemo kusimamia Sheria na Kanuni za Utumishi pamoja na Sheria ya Manunuzi na Ugavi sambamba na kuweka mazingira bora ya kiutendaji kazi, kuwaendeleza wafanyakazi kielimu pamoja na kusimamia maslahi yao. Vile vile Idara inatoa huduma za manunuzi, uhifadhi wa vifaa, huduma za uhasibu, uwekaji wa kumbukumbu za hesabu, mapato na matumizi pamoja na matayarisho ya ulipaji wa mishahara.

Malengo ya Mwaka 2013/2014

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara ya Utumishi na Uendeshaji ilikusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuweka mazingira bora ya ustawi wa watumishi wake kwa kuwapatia huduma bora.
ii. Kuwajengea uwezo watumishi kwa kuwapatia mafunzo kwa mujibu wa kada zao.
iii. Kuimarisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi kupitia Kamati ya Uongozi, Kamati ya Zabuni na Kamati ya Ukaguzi.

Mhe .Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Baraza lako Tukufu liliidhinisha jumla ya TZS 1,084,726,572/= kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia mwezi wa Machi 2014, Idara imeingiziwa jumla ya TZS 611,170,504/= kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 56 ya fedha zilizoidhinishwa.

Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2013/2014.

Mhe. Spika, Idara imelipa stahili mbalimbali kwa wafanyakazi ikiwemo mishahara, michango ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, posho la likizo, posho la kujikimu, malipo ya muda wa ziada pamoja na gharama za safari za ndani na nje ya nchi. Vile vile, Idara imenunua vifaa mbalimbali vya kuandikia, vifaa vya usafi na sare za wafanyakazi. Aidha, Idara imeandaa makisio na makadirio ya mishahara ya wafanyakazi.

Mhe. Spika, katika kuwaendeleza watumishi wake, Ofisi imewapatia mafunzo ya muda mrefu ndani ya Tanzania watumishi Kumi na Mbili (12) katika ngazi na fani zifuatazo: Stashahada 4: Ukatibu Muhtasi, (1), Rasilimali watu (2), Manunuzi na Ugavi (1). Shahada ya Kwanza 4: Mipango ya Tawala za Mikoa (1), Rasilimali Watu (1), Manunuzi na Ugavi (2). Shahada ya Pili 3: Utawala wa Umma (1), Usimamizi wa Biashara (1) na Usimamizi wa mazingira na mfanyakazi na mmoja (1) amehudhuria mafunzo ya muda mfupi nchini China.

Mhe. Spika, Idara imefanya mikutano ya Kamati mbali mbali ikiwemo mikutano ya kamati ya Uongozi wa Ofisi, Kamati ya Ukaguzi, Kamati ya Zabuni na Kamati ya Fedha.

Mhe. Spika, kupitia Kamati inayosimamia masuala ya Mtambuka, Idara imetoa elimu juu ya kujikinga na maradhi mbali mbali yakiwemo maambukizi ya UKIMWI na maradhi ya kisukari.

Mhe. Spika, Idara katika mwaka wa Fedha ujao inategemea kutekeleza yafuatayo:-

i. Kuweka mazingira bora ya kazi na ustawi mzuri wa watumishi;
ii. Kuimarisha kitengo cha Teknolojia ya habari na mawasiliano na;
iii. Kuendeleza uingizaji wa masuala ya mtambuka katika majukumu ya msingi ya Wizara

Muelekeo na Malengo ya mwaka 2014/2015.

Mhe. Spika, ili Idara ya Utumishi na Uendeshaji iweze kutekeleza malengo yake ipasavyo, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya TZS. 1,135,796,000/=. Kati ya hizo TZS. 527,545,000/= ni kwa ajili ya kazi za kawaida na 608,251,000/= kwa ajili ya mishahara, michango ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF*) na maposho maalum ya wafanyakazi.

OFISI YA USAJILI NA KADI ZA UTAMBULISHO.

Mhe. Spika, Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho imeanzishwa rasmi mwaka 2005 chini ya Sheria Namba7/2005 ikiwa na wajibu wa kuwasajili na kuwapatia vitambulisho Wazanzibari wakaazi wenye umri wa miaka 18 na kuendelea. Aidha, Ofisi ina wajibu wa kutunza taarifa zote za wananchi zilizokusanywa kwa ajili hiyo.

Malengo ya Mwaka 2013/2014

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho ilikusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuwasajili Wazanzibari Wakaazi waliotimiza masharti kwa mujibu wa Sheria na kuwapatia vitambulisho;
ii. Kutunza taarifa za waliosajiliwa katika database maalum;
iii. Kuwasajili na kutoa vitambulisho maalum kwa wageni wanaoishi Zanzibar kwa ruhusa maalum;
iv. Kuzishajihisha Taasisi za Serikali kutumia taarifa zilizowekwa katika “Database” ya Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho kwa usalama na kiuchumi;
v. Kuratibu masuala mtambuka pamoja na kutoa elimu ya kujikinga na maambukizi mapya ya UKIMWI kwa wafanyakazi;
vi. Kuendelea kuwajengea uwezo kielimu wafanyakazi wa Ofisi; na
vii. Kuongeza ufanisi kazini ikiwa ni pamoja na kuwapatia wafanyakazi stahili zao.

Mhe. Spika, Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 iliidhinishiwa jumla ya TZS. 2,055,000,000/= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia mwezi Machi 2014, Ofisi hii iliingiziwa TZS. 873,000,000/= sawa na asilimia 42.4 ya makadirio ya matumizi ya kazi za kawaida.

Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2013/2014.

Mhe. Spika, Ofisi imesajili Wazanzibari wakaazi 24,379 waliotimiza masharti ya usajili, imetengeneza vitambulisho vipya 25,078 vilivyomaliza muda wake wa matumizi na imetengeneza vitambulisho 3,236 kwa wananchi waliopoteza na walioomba kufanya marekebesho halali ya taarifa zao binafsi.

Mhe. Spika, Ofisi imeendelea kutengeneza vitambulisho vya wafanyakazi wa Serikali na Taasisi zake ambazo zimewasilisha taarifa za wafanyakazi wao kwa ajili ya kutengenezewa vitambulisho, ikiwa ni pamoja na Mashirika ya Serikali na Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Spika, Ofisi imefanya mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Usajili Namba 7 ya 2005 ili kuruhusu utoaji wa vitambulisho kwa wageni wanaoishi nchini. Vitambulisho hivyo vitaanza kutolewa mara tu baada ya taratibu nyengine kukamilika.

Mhe. Spika, katika jitihada za kujitangaza na kuielimisha jamii juu ya miongozo na taratibu za kiutendaji, Ofisi imechapisha Sera ya Vitambulisho vya Mzanzibari pamoja na kuandaa makala ya picha (*Documentary*) maalum juu ya shughuli za Ofisi na mafanikio yake.

Mhe. Spika, katika kuimarisha utendaji kazi, Ofisi imeendelea kuwajengea uwezo wafanyakazi 9 kwa kuwasomesha katika viwango vya Cheti, Stashahada pamoja na Shahada katika fani za Utawala na Takwimu, Ununuzi na Ugavi, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano. Aidha, Ofisi imefunga baadhi ya vifaa vipya na vya kisasa kabisa kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa mitambo na kudhibiti usalama wa taarifa zinazohifadhiwa.

Mhe. Spika, Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho imefanyiwa ukaguzi wa kimataifa juu ya muundo, mfumo na taratibu zake za kiutendaji na imethibitishwa kuwa inaendelea kufanya kazi zake kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vilivyowekwa na *International Standard Organisation* na *IQ Net* na kukabidhiwa vyeti vya ubora wa kazi kwa mara ya nane.

Muelekeo na Malengo ya Mwaka 2014/2015.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho imekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuendelea kuwasajili Wazanzibari Wakaazi wanaotimiza masharti ya usajili na kuwapatia vitambulisho.
ii. Kutunza taarifa za waliosajiliwa katika ‘database’ maalum.
iii. Kuwasajili na kutoa vitambulisho maalum kwa wageni wanaoishi Zanzibar kwa ruhusa maalum.
iv. Kuzishajihisha taasisi za Serikali kutumia taarifa zilizowekwa katika ‘database’ ya Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho kwa usalama na kiuchumi.
v. Kuratibu masuala mtambuka pamoja na kutoa elimu ya kujikinga na maambukizi mapya ya UKIMWI kwa wafanyakazi.
vi. Kuendelea kuwajengea uwezo kielimu wafanyakazi wa Ofisi.
vii. Kuongeza ufanisi kazini ikiwemo kuwapatia wafanyakazi stahili zao.

Mhe. Spika, ili Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho iweze kutekeleza malengo yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2014/2015, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe TZS. 1,939,000,000/= kwa kazi za kawaida.

IDARA YA URATIBU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

Mhe. Spika, Idara ya Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ina jukumu la kuratibu utekelezaji wa shughuli za Taasisi za Mamlaka ya Mikoa na Taasisi za Serikali za Mitaa, katika kuhakikisha utekelezaji wa majukumu hayo Idara ina wajibu wa kutoa maelekezo kwa mujibu wa Sera, Sheria na mipango mikuu ya **Serikali.**

Malengo ya Mwaka 2013/2014

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuimarisha mazingira bora kazini na utoaji wa huduma;

ii. Kujenga uwezo wa watumishi;
iii. Kuimarisha uratibu wa Taasisi za Mikoa, Wilaya, Serikali za Mitaa na wadau wa maendeleo; na
iv. Kuimarisha ushirikishwaji wa wananchi katika utawala wa kidemokrasia.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Idara ya Uratibu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilipangiwa jumla ya TZS. 705,866,937/= kwa kazi za kawaida na TZS. 1,200,000,000/= ikiwa ni ruzuku kwa Baraza la Manispaa. Hadi kufikia Machi 2014, Idara imeingiziwa TZS 300,629,990/= sawa na asilimia 43 kwa matumizi ya kazi za kawaida na TZS 900,000,000/= sawa na asilimia 75 ikiwa ni ruzuku kwa Baraza la Manispaa.

Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2013/2014.

Mhe. Spika, Idara iliendelea na uimarishaji wa mazingira bora kazini na utoaji wa huduma kwa wafanyakazi wake kwa kuwapatia stahili mbali mbali zikiwemo mishahara na michango ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Aidha, Idara imefanya manunuzi ya vifaa mbali mbali vya kuandikia pamoja na vipuri vya gari ili kurahisisha utendaji kazi wa Idara.

Mhe. Spika, Idara imeendelea kuwapatia watumishi wake mafunzo ya muda mrefu na mfupi. Jumla ya watumishi 5 wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu katika fani za utawala, uwekaji kumbukumbu, ukatibu muhtasi na uhasibu katika ngazi ya stashahada na mmoja ngazi ya shahada ya uzamili katika fani ya Utawala na Uendeshaji. Watumishi wawili wamehudhuria mafunzo ya muda mfupi nchini China.

Mhe. Spika, katika kuimarisha Uratibu wa Taasisi za Mikoa, Wilaya, Serikali za Mitaa na wadau wa maendeleo, Idara imeratibu kwa karibu zaidi shughuli za kiutendaji katika Mikoa, Wilaya na Serikali za Mitaa. Aidha, Idara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mawasiliano (*TCRA*) Tanzania Bara imeshiriki vikao vya maandalizi ya awali ya uwekaji majina ya nyumba na mitaa katika shehia nne za majaribio (Shehia ya Mombasa na Chukwani katika Wilaya ya Magharibi kwa Unguja na Shehia ya Selem na Limbani katika Wilaya ya Wete kwa Pemba). Aidha, kwa kushirikiana na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (*NIDA*) Idara imetoa mafunzo kwa masheha katika Mikoa yote ya Zanzibar kuhusiana na athari za kughushi nyaraka za Serikali.

Mhe. Spika, Idara imefanya ziara za kimasomo na kubadilishana uzoefu kwa watendaji katika Taasisi mbali mbali za Serikali za Mitaa huko Tanzania Bara. Sambamba na hili Idara imeratibu maandalizi ya mkutano wa mashirikiano ya pamoja baina ya viongozi wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ na Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI). Mkutano huo unatarajiwa kufanyika tarehe 19 na 20/6/2014 huko Morogoro Tazania Bara .

Mhe. Spika, katika kuimarisha ushirikishwaji wa wananchi katika utawala wa kidemokrasia, Idara imefanya marekebisho ya Sheria za Serikali za Mitaa (Sheria Nam.3 na 4 ya mwaka 1995 na Sheria ya Mamlaka ya Mikoa (Sheria Nam. 1 ya mwaka 1998). Marekebisho hayo yamefanyika kufuatia kukamilika kwa Sera ya Serikali za Mitaa. Mabadiliko hayo ya Sheria yatasaidia utekelezaji wa Sera kwa ufanisi. Aidha, Idara imeratibu vikao mbalimbali vya kupeana miongozo ya utendaji kazi kwa Waheshimiwa Madiwani ambao ndio waamuzi wakuu wa shughuli za Serikali za Mitaa. Miongozo hiyo inahusisha namna bora ya ushirikishwaji wa wananchi katika kupanga na kubuni miradi na matumizi bora ya rasilimali watu na fedha. Kutokana na hilo miradi mingi ya Serikali za Mitaa imekuwa endelevu na inaendeshwa kwa uhakika. Aidha, mapato katika Serikali za Mitaa yameongezeka.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara ya Uratibu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuandaa programu za kushajihisha jamii juu ya umuhimu wa kukasimu madaraka kwa wananchi kwa kupitia vyombo vya habari;
ii. Kufanya ufuatiliaji wa kila robo mwaka kwa kutemebelea taasisi za Serikali za Mitaa na Mamlaka ya Mikoa juu ya utendaji wao wa kazi za kila siku;

iii. Kukuza na kuimarisha uratibu wa Taasisi za Mikoa, Wilaya na Serikali za Mitaa na wadau mbali mbali wa maendeleo wa ndani na nje ya nchi;
iv. Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Serikali za Mitaa kwa mujibu wa miongozo ya Sheria mpya ya Mamlaka ya Mikoa na Serikali za Mitaa;

v. Kuendeleza namna bora ya ushirikishwaji wa wananchi katika utoaji wa maamuzi; na
vi. Kufanya ziara za kimasomo ndani na nje ya Tanzania kujifunza namna bora ya uratibu na usimamizi wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mhe. Spika, ili Idara iweze kutekeleza malengo yake kwa ufanisi kama ilivyojipangia kwa mwaka wa fedha 2014/2015, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe TZS 695,443,000/= kwa matumizi ya kazi za kawaida, TZS 200,000,000 kwa kazi za maendeleo na TZS 1,200,000,000 ikiwa ni ruzuku kwa Baraza la Manispaa.

MRADI WA MABORESHO YA SERIKALI ZA MITAA

Mhe. Spika, Serikali za Mitaa ndio mhimili mkubwa wa utekelezaji wa majukumu ya Serikali Kuu katika lengo zima la kuhakikisha maendeleo endelevu katika nchi yetu. Katika kufanisha azma hiyo, Serikali kupitia Mpango wa Uimarishaji Serikali za Mitaa imedhamiria kuzipitia sheria zote zinazosimamia utekelezaji wa majukumu ya Taasisi za Serikali za Mitaa. Kutokana na kwamba Sheria hizo ni muda mrefu hazijafanyiwa marekebisho ambayo kwa sasa hazikidhi haja katika utendaji wa kazi za Serekali za Mitaa.

Mhe. Spika, Idara ya Uratibu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa katika mradi wa Maboresho ya Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2013/2014 ulipangiwa jumla ya TZS. 150,000,000/= kwa shughuli za utekelezaji wa maboresho ya Sheria za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Hadi kufikia Machi 2014, Idara imeingiziwa TZS. 47,310,000/= ambazo ni sawa na asilimia 32 za fedha zilizoidhinishwa

Utekelezaji wa Mradi wa Maboresho ya Serikali za Mitaa

Mhe. Spika, Idara ya Uratibu Tawala za Mikoa kwa kutumia wataalamu wake wa ndani, imefanya mapitio ya Sheria ya Tawala za Mikoa Namba 1 ya 1998 na Sheria namba 3 na 4 za 1995 za Serikali za Mitaa. Idara imefanya mikutano miwili ya wadau Unguja na Pemba kwa lengo la kuziwasilisha rasimu za miswada hiyo ili kupata maoni ya wadau hao. Marekebisho haya ya Sheria yanafanyika kufuatia kukamilika kwa Sera ya Serikali za Mitaa.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara ya Uratibu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kupitia Mradi wa Maboresho ya Serikali za Mitaa imekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kufanya tathmini ya mahitaji ya watumishi katika Serikali za Mitaa
ii. Kutoa elimu ya Uraia kuhusiana na Serikali za Mitaa
iii. Kutoa elimu kwa madiwani juu ya wajibu na majukumu yao kuhusiana Urasimishwaji madaraka ya Serikali za Mitaa.
iv. Kufanya tathmini ya mahitaji ya watumishi katika serikali za mitaa
v. Kufanya tathmini na kuandaa mfumo, utaratibu na miongozo ya fedha.
vi. Kuhakiki mipaka ya Mamlaka ya Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mhe. Spika, ili Idara iweze kutekeleza malengo yake kupitia Mradi wa Maboresho ya Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2014/2015, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya TZS TZS.200, 000,000/=

OFISI YA OFISA MDHAMINI PEMBA

Mhe. Spika, Ofisi ya Ofisa Mdhamini Pemba inasimamia shughuli zote za Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa upande wa Pemba. Kwa mwaka wa fedha 2013/14, Ofisi iliidhinishiwa matumizi ya TZS. 508,084,350/=. Hadi kufikia Machi 2014, fedha iliyopatikana ni TZS. 333,869,300/= sawa na asilimia 66 ya makadirio yote. Kati ya fedha hizo TZS. 235,869,300/= zilitumika kwa

malipo ya mishahara, posho na michango ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) na TZS. 98,000,000/= zilitumika kwa shughuli mbali mbali za kuendeshea Ofisi ikiwa ni pamoja na malipo baada ya saa za kazi, matengenezo ya vipando, posho la likizo, gharama za masomo na safari kikazi Unguja.

Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2013/2014

Mhe. Spika, Ofisi Kuu Pemba imefanya ufuatiliaji wa shughuli mbali mbali za Ofisi na taasisi zake kwa lengo la kuimarisha utekelezaji wa shughuli hizo. Aidha, Ofisi imetoa mafunzo ya tathmini na ufuatiliaji kwa maafisa mipango wa (OR) Tawala za Mikoa ambayo yameongeza kiwango cha uwelewa juu ya umuhimu wa ufuatiliaji na tathmini.

Mhe. Spika, katika kuimarisha uingizwaji wa masuala mtambuka katika mipango ya Ofisi, Ofisi ya Ofisa Mdhamini Pemba imetoa mafunzo ya masuala mtambuka kwa wafanyakazi 40 ikiwajumuisha wajumbe wa Kamati ya Masuala Mtambuka. Mafunzo yaliyotolewa yalijumuisha masuala ya UKIMWI na madawa ya kulevya, Jinsia na Utawala Bora.

Mhe. Spika, Ofisi imeratibu upatikanaji wa taarifa mbali mbali za utekelezaji kwa taasisi zilizo chini ya Ofisi hii kwa upande wa Pemba pamoja na kuratibu maandalizi ya Bajeti na Mpango wa Utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Aidha, imewawezesha watendaji kushiriki katika vikao mbalimbali vya kazi vilivyofanyika Unguja na imeweza kulipia gharama za masomo kwa wafanyakazi wanne wanaoendelea na masomo yao katika ngazi na fani zifuatazo: Ustawi wa Jamii (Shahada ya kwanza 1), Rasilimali watu (Shahada ya pili 1), Biashara na Uongozi (Shahada ya pili 1) na Usimamizi wa fedha (Diploma 1).

Mhe. Spika, ili Ofisi ya Ofisa Mdhamini Pemba iweze kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2014/15, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya TZS. 571,061,000/=. Kati ya fedha hizo TZS. 143,845,000/= ni kwa ajili ya kazi za kawaida na TZS 377,216,000/= kwa ajili ya mishahara, Michango ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) na maposho maalum.

MAMLAKA YA SERIKALI ZA MIKOA.

Mhe. Spika, Mamlaka za Serikali za Mikoa zina jukumu la kuratibu, kusimamia na kusaidia utekelezaji wa shughuli za Serikali katika maeneo yao ya Utawala. Kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama kuhakikisha kuwa amani na utulivu zinadumishwa na kuimarishwa. Baada ya muhtasari huo, naomba kutoa maelezo kuhusu utekelezaji wa malengo ya Mamlaka za Serikali za Mikoa kwa mwaka 2013/2014 na malengo yaliyopangwa kwa mwaka 2014/2015.

MKOA WA MJINI MAGHARIBI

Mhe. Spika, Mkoa wa Mjini Magharibi una jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za maendeleo katika ngazi za Wilaya na Shehia. Aidha, kuhakikisha ulinzi na usalama unaimarika pamoja na kutatua matatizo mbalimabali ya wananchi wa Mkoa huo.

Malengo ya Mwaka 2013/2014

Mhe. Spika, katika kuyatekeleza majukumu hayo Mkoa wa Mjini Magharibi, uliidhinishiwa TZS 1,608,175,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014. Hadi kufikia mwezi Machi 2014, Mkoa huu umeingiziwa TZS 875,560,856 sawa na asilimia 54 ya makadirio ya matumizi hayo.

Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2013/2014.

Mhe. Spika, katika kuimarisha ufanisi wa utendaji kazi, Mkoa ulifanikiwa kulipa stahili za wafanyakazi zikiwemo mishahara, maposho na likizo, kununua vifaa vya kutendea kazi, pamoja na kufanya matengenezo makubwa ya sehemu ya jengo kongwe la Ofisi ya Mkoa iliyopo Vuga na sehemu ya jengo la Ofisi ya Wilaya ya Magharibi. Hata hivyo kufuatia uchakavu wa jengo la Ofisi ya Mkoa na uhaba wa nafasi, Ofisi ya Mkoa iko

katika hatua za mwisho za mazungumzo na wawekezaji ambapo michoro ya awali imekamilika na michoro ya mwisho inatarajiwa kukamilika ndani ya kipindi cha mwisho cha mwaka wa fedha 2013/2014 ambapo itajumuisha kusaini hatua za mwisho za ujenzi, ujenzi unatarajia kuanza mapema katika mwaka wa fedha 2014/2015.

Mhe. Spika, aidha, jumla ya wafanyakazi wanane wakiwemo wanawake sita na wanaume wawili wamepatiwa mafunzo katika ngazi ya cheti na Stashahada katika fani ya utunzaji wa kumbukumbu, uandishi wa habari, ukatibu muhtasi, uongozi wa rasilimali watu na utawala wa umma. Mafunzo ya mkakati wa mawasiliano yametolewa kwa wafanyakazi kwa ngazi ya Mkoa, Wilaya, Baraza la Manispaa Halmashauri kwa lengo la kuimarisha hali ya mawasiliano miongoni mwa taasisi na utendaji ndani ya Mkoa.

Mhe. Spika, kutokana na ongezeko la idadi ya watu katika Mkoa huu, takwimu za Sensa ya Watu na Makaazi ya 2012 zinaonesha kuwa, Mkoa una watu 593,678 sawa na asilimia 46 ya wakaazi wote wa Zanzibar na una ukubwa wa ardhi wa kilomita za mraba 224 ambayo ni chini ya asilimia 10 ya ardhi yote ya Zanzibar. Kutokana na na hali hiyo na kwa kuwa matokeo ya uhalifu yanapangwa na kufanyika katika Mkoa wa Mjini Magharibi na kwa kuzingatia umuhimu wa sekta ya Utalii wa uchumi wa nchi. Hivyo, Ofisi ya Mkoa inaendelea na mazungumzo na wawekezaji kuhusu uimarishaji wa ulinzi katika maeneo ya mji hususan Mji Mkongwe kwa kutumia teknolojia ya kisasa ya CCTV (*Close Circuit Television*).

Mhe. Spika, shughuli nyengine zilizotekelezwa katika kuimarisha ulinzi na usalama wa wananchi na mali zao, ni pamoja na kuandaa vikao 24 vya kawaida na vikao 19 vya dharura vya kamati za Ulinzi na Usalama kwa lengo la kujadili masuala ya yanayohusu ulinzi na usalama.

Aidha, Mkoa ulifuatilia usalama katika eneo la kupokelea umeme Fumba na maeneo ya madiko yasiyo rasmi yanayotumiwa kufanyika vitendo vya uhalifu Nyamanzi, eneo la soko la samaki Mazizini lililovamiwa na wananchi, maeneo ya gofu la Magomeni, ujenzi wa vibanda vya wakaushaji wa madagaa Maruhubi, uvamizi wa barabara za ndani K/chekundu, uchafuzi wa mazingira eneo la Michenzani block 8 pamoja na zoezi la uondoshaji wa kituo cha daladala cha Darajani na matayarisho ya sherehe za Mapinduzi kiulinzi. Mkoa unaendelea kuratibu na kusimamia zoezi la uandikishaji wa vitambulisho vya kitaifa kupitia Taasisi ya Mamlaka ya Vitambulisho vya Kitaifa (*NIDA*) ambapo kazi ya uandikishaji inaendelea.

Mhe. Spika, mafunzo juu ya kupiga vita UKIMWI yamefanyika kwa wafanyakazi 40, vijana 40 katika makundi hatarishi kwa maambukizi ya virusi vya UKIMWI pamoja na uhamasihaji kwa njia ya semina katika Shehia za Kizimbani na Mwakaje.

Mhe. Spika, katika kuhakikisha maendeleo endelevu kwa jamii, Mkoa wa Mjini Magharibi umetekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Umefanya ziara kwa ajili ya kuhamasisha jamii juu ya kuanzisha shughuli za ujasiriamali kwa lengo la kukuza kipato na mahitaji yao zimefanyika ambapo jumla ya vikundi 18 vya vijana vikiwemo vya ushoni, mazingira, kazi za amali na mapishi vimetembelewa katika shehia za Mtofaani na Shakani. Mkoa umeendelea kuwapatia mafunzo ya ujasiriamali na stadi za kazi kwa vijana 11 wa shehia tano za Mkele, Matarumbeta, Shangani, Jang'ombe na Mwembeladu.
ii. Jumla ya miradi 14 ya wananchi ikiwemo ya umeme, maji, elimu afya na barabara imefuatiliwa katika shehia za K/hewa, Mpendae, Chumbuni, M/ladu, Dole, Sharifu Msa, Kihinani, Mwanyanya, Magogoni, Fuoni, Bumbwisudi, Dimani na M/kwerekwe *(Angalia Kiambatisho Namba 4)*. Jumla ya wazee 2,071 wamepatiwa misaada ya fedha, na wananchi 41 na vikundi viwili vya sanaa ya muziki na skauti wamepatiwa misaada mbalimbali ikiwemo ya ada ya masomo, vifaa vya michezo, matibabu na ujenzi wa vyoo kwa lengo la kuendeleza shughuli zao za kijamii na kiuchumi.
iii. Jumla ya maombi 125 ya uvunaji wa rasilimali zisizorejesheka yamefuatiliwa na vibali 91 vya ukataji miti vimetolewa. Doria 15 za udhibiti wa ukataji wa miti na mikoko zimefanyika katika shehia za Nyamanzi, Maruhubi, Lumumba, Fuoni Kibondeni na visiwa vya Miwi na Chumbe.
iv. Ufuatiliaji na utatuzi wa migogoro saba ya ardhi umefanyika katika shehia za Mchangani, Mwakaje, Mwera, Kiembesamaki, Dole na Kama, na jumla ya vikao vinne vya utatuzi wa migogoro ya ardhi vimefanyika.

v. Uhamasishaji wa shughuli za kilimo umefanyika na jumla ya ekari 2,000 za mpunga, ekari 1,300 za mazao ya chakula na ekari 450 za mboga zimelimwa katika maeneo mbali mbali ya kilimo ndani ya Mkoa wa Mjini Magharibi.
vi. Mkoa umefanikiwa kuhamasisha jamii juu ya zoezi la chanjo na matone pamoja na uzinduzi wa kampeni ya 'Tuboreshe Chakula' yenye lengo la kuongeza virutubisho vya madini na vitamin katika vyakula vya watoto wenye umri chini ya miaka mitano katika shehia za Chumbuni na Karakana.
vii. Mkoa umeendelea kuhamasisha uanzishwaji wa madarasa mapya, wazee kufuatilia maendeleo ya watoto wao na kusimamia ufanikishaji wa mitihani ya Kitaifa.
viii. Ahadi za viongozi wakuu wa kitaifa zimefuatiliwa.
ix. Katika kudhibiti vitendo vya udhalilishaji Mkoa kwa kushirikiana na kamati za Usalama za Mkoa na Wilaya umeendelea kuhamasisha jamii juu ya upigaji vita udhalilishaji wa kijinsia katika shehia za Fumba, Bweleo, Dimani na Kombeni. Aidha, kesi 23 za wanawake na watoto wa kike na wa kiume zilifuatiliwa na zipo katika uhakiki wa awali wa ngazi za shehia, vituo vya polisi na mahakamani.

Muelekeo na Malengo ya Mwaka 2014/2015

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Mkoa wa Mjini Magharibi, unatarajia kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kuimarisha ulinzi na usalama kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi.
ii. Kuimarisha mazingira bora ya utendaji kazi.
iii. Kuhakisha utoaji wa huduma za kijamii unaimarika.
iv. Kuratibu, kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa shughuli za sekta mbalimbali.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Mkoa umejipangia kukusanya jumla TZS 20,000,000 kutoka katika vyanzo vyake vidogo vya mapato, mapato hayo yanajumuisha malipo ya ada ya uhaulishaji ardhi, malipo ya usafirishaji magari na vyombo vyengine vya moto na malipo ya ada za ndoa za kiserikali.

Mhe. Spika, ili Mkoa wa Mjini Magharibi uweze kutekeleza malengo uliojipangia kwa mwaka wa fedha 2014/2015, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe TZS 1,757,800,000/=.

MKOA WA KASKAZINI UNGUJA

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Mkoa wa Kaskazini Unguja ulikusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuimarisha hali ya ulinzi na usalama katika Mkoa;
ii. Kuimarisha ushiriki wa wananchi katika utawala wa kidemokrasia;
iii. Kuongeza uelewa wa wafanyakazi katika masuala mtambuka (UKIMWI na Mazingira);
iv. Kuandaa mazingira mazuri katika uendeshaji wa shughuli za Ofisi; na
v. Kuwajengea uwezo wafanyakazi.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Mkoa wa Kaskazini Unguja ulitengewa TZS 1,247,000,000/= kwa matumizi ya kawaida na hadi Machi 2014, Mkoa uliingiziwa TZS 924,300,000/= sawa na asilimia 74 ya makadirio ya matumizi ya kawaida.

Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2013/2014

Mhe. Spika, Mkoa umeratibu vikao 13 vya Kamati ya Ulinzi na Usalama ambavyo vilijadili masuala mbalimbali na kupitia taarifa ya hali ya ulinzi na usalama katika Mkoa. Hali ya usalama katika Mkoa inaendelea kuimarika siku hadi siku na wananchi wanaendelea kuishi katika hali ya usalama, amani na utulivu. Aidha, Mkoa kwa kushirikiana na vyombo husika ulishughulikia ipasavyo majanga ya upepo yaliyotokea mwezi wa Februari, 2014 katika Wilaya ya Kaskazini "A" ambapo nyumba zipatazo 685 zimeezuliwa mapaa na kusababisha hasara ya kiasi cha TZS 95 milioni. Shehia hizo na idadi ya nyumba ni Nungwi 86, Kilimani 157,

Fukuchani 44, Kidoti 60, Tazari 176, Kigunda 63, Kijini 17, Tumbatu16, P/Mchangani 8, Matemwe 3, Kilindi 15, Kidagoni 29 na Bwereu 11. Aidha, ZALU, Z-HOTEL na Amani Bungalow iliezuka mapaa.

Mhe. Spika, Mkoa ulishughulikia ajali ya meli ya MV Kilimanjaro iliyotokea baada ya kuyumbishwa na upepo mkali na kumwaga watu baharini. Ajali hii ilitokea katika mkondo wa Nungwi ambapo jumla ya watu wanane waliokolewa kati yao watano wakiwa wamefariki na watatu wakiwa hai.

Mhe. Spika, katika kuimarisha utawala wa kidemokrasia, Mkoa umekuwa karibu sana na wananchi katika kupanga, kutekeleza na kusimamia shughuli za maendeleo. Mikutano sita ya kuhamasisha wananchi juu ya umuhimu wa kushiriki katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo, mikutano miwili ya Kamati ya Maendeleo ya Mkoa na mikutano sita ya Kamati za Maendeleo za Wilaya imefanyika. Wananchi wameshirikia katika uendelezaji wa miradi 17 ya maendeleo kama inavyoonekana katika *Kiambatanisho Namba 5*.

Mhe. Spika, jumla ya vikao tisa vimefanyika katika Shehia mbalimbali za Mkoa huu ambavyo vimewahamasisha wananchi kuwa na muelekeo mzuri wa ushirikiano, mshikamano, umoja, usalama, upendo, amani na utulivu ambavyo ni muhimu sana kwa maendeleo ya uchumi na ustawi wa jamii. Aidha, msaada wa wazee umeweza kutolewa kama kawaida. Jumla ya wazee 2,070 wamepatiwa misaada ya fedha ili ziwasaidie kimaisha.

Mhe. Spika, Mkoa umejitahidi kuongeza uelewa wa wafanyakazi katika masuala mtambuka ambapo jumla ya mikutano tisa imefanyika juu ya uhamasishaji wa kujikinga na maambukizi mapya ya VVU. Wafanyakazi 77 na masheha 67 wamepatiwa mafunzo hayo.

Mhe. Spika, mazingira mazuri katika uendeshaji wa shughuli za ofisi ni jambo la muhimu katika utendaji bora wa kazi. Katika kutekeleza jambo hili Mkoa umeweza kulipa stahili za wafanyakazi zikiwemo mishahara na maposho mbalimbali. Pia Mkoa umenunua vifaa vya kuendeshea kazi na uendelezaji wa ujenzi wa jengo jipya la Mkoa.

Mhe. Spika, katika kuwajengea uwezo wafanyakazi, jumla ya wafanyakazi watano wa Mkoa wanaendelea kupatiwa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi katika ngazi ya Stashahada ya juu na Shahada ya pili ya Maendeleo vijijini, Shahada ya kwanza ya Uhasibu, stashahada ya Ukatibu Muhtasi na stashahada ya Manunuzi na Ugavi. Wafanyakazi wengine wanne wamepatiwa mafunzo ya cheti katika fani za uhudumu, takwimu na uandishi wa habari.

Mhe. Spika, shughuli nyengine zilizofanywa na Mkoa ni pamoja na:-

i. Ufuatiliaji wa utekelezaji wa shughuli za elimu ambapo Mkoa umefanya ukaguzi wa Skuli 20. Ufuatiliaji huo uliangalia ufundishaji na mahudhurio ya wanafunzi ili kutatua tatizo la utoro. Pia, ukaguzi wa Skuli zenye vituo vya mitihani pamoja na vikao vya kuhamasisha ufundishaji bora kwa lengo la kuongeza ufaulu wa wanafunzi vimefanyika.
ii. Kusimamia na kufuatilia uchimbaji wa visima tisa vya ziada vinavyofadhiliwa na Ras al Khaima. Kati ya visima hivyo vitano viko Kaskazini ‘A’ na visima vinne viko Kaskazini ‘B’.
iii. Kuhamasisha kilimo cha mpunga ambapo jumla ya ekari 6,200 zimelimwa kati ya lengo la 6,700 sawa na asilimia 92.5.
iv. Mkoa umeadhimisha sherehe ya kutimia miaka 50 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar kwa kuzindua miradi mbali mbali, kuweka mawe ya msingi na kuandika kitabu cha historia ya Mkoa katika kipindi cha miaka 50 ya Mapinduzi.

Muelekeo na Malengo ya Mwaka 2014/2015

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Mkoa wa Kaskazini Unguja unakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuratibu, kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa shughuli za sekta mbalimbali.

ii. Kuendeleza shughuli za ulinzi na usalama.
iii. Kuongeza uelewa wa wafanyakazi na wananchi katika masuala Mtambuka (Ukimwi na Mazingira).
iv. Kuandaa mazingira mazuri katika uendeshaji wa shughuli za Ofisi
v. Kuwajengea uwezo wafanyakazi na
vi. Kuendeleza ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kwa kujenga fensi pamoja na ujenzi wa ofisi za Wakuu wa Wilaya ya Kaskazini "A"na "B".

Mhe. Spika, ili Mkoa wa Kaskazini Unguja uweze kutekeleza malengo yake kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe TZS 1,362,700,000 kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida.

MKOA WA KUSINI UNGUJA

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Mkoa wa Kusini Unguja ulipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kusimamia shughuli za ulinzi na usalama;
ii. Kuratibu, kusimamia, kufuatilia na kusaidia utekelezaji wa shughuli za sekta mbali mbali;
iii. Kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na mrefu ili kuongeza ufanisi kazini;
iv. Kusimamia na kuzitumia ipasavyo rasilimali watu na vitu katika kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii;
v. Kuendeleza jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Wilaya na matengenezo madogo madogo; na
vi. Kuratibu masuala Mtambuka zikiwemo za UKIMWI, mazingira na masuala ya watu wenye ulemavu.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014, Mkoa wa Kusini Unguja uliidhinishiwa Tzs. 1,247,000,000/= kwa matumizi ya kazi za kawaida, na hadi kufikia mwezi wa Machi 2014 Mkoa uliingiziwa Tsh. 924,300,000/= sawa na asilimia 74 ya fedha zilizoidhinishwa.

Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2013/2014.

Mhe. Spika, katika kusimamia shughuli za ulinzi na usalama, Mkoa umefanya vikao 9 vya ulinzi na usalama vya kawaida na vikao 8 vya dharura ili kuratibu na kutathmini masuala ya ulinzi na Usalama ndani ya Mkoa kwa lengo la kuimarisha amani, utulivu, usalama wa raia na mali zao.

Mhe. Spika, katika kuratibu, kusimamia, kufuatilia na kusaidia utekelezaji wa shughuli za sekta mbali mbali, Mkoa kwa kushirikiana na Kamati za Wazee za Skuli na Polisi Jamii umeendelea kufanya ukaguzi wa watoto wenye mazingira magumu katika Skuli 10 ili kupunguza tatizo la utoro maskulini. Jumla ya watoto 62 wamesaidiwa sare na viatu. Sambamba na hilo, Mkoa unaendelea na hatua za kuwarejesha skuli wanafunzi watoro. Aidha, Mkoa umezitembelea skuli zenye vituo vya mitihani na kufanya vikao na walimu wakuu na masheha kwa lengo la kuhamasisha ufundishaji na kuondokana na vitendo vya udanganyifu katika mitihani. Mikakati iliyobuniwa na kutumika imeweza kusaidia kuongeza idadi ya wanafunzi waliofaulu wa Mkoa wa Kusini Unguja.

Mhe. Spika, Mkoa kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maji (ZAWA) umeratibu uchimbaji wa visima vya maji kumi na mbili (12) ambavyo Bwejuu/Michamvi 2, Mtende 1, Mzuri 1, Tunguu 2, Jendele 2, Bambi/Uroa 1, Pagali 1, Bambi 1 na Umbuji 1. Aidha, jumla ya miradi 33 ilizinduliwa kwa uwekaji wa mawe ya msingi na ufunguzi katika uzinduzi wa sherehe za miaka 50 ya Mapinduzi Matukufu. Sambamba na hayo, Kitabu cha Historia ya Miaka 50 ya Mapinduzi kuhusu maendeleo yaliyopatikana katika Mkoa kimeandikwa.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2013/2014 Mkoa kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Maliasili umeweza kuhamasisha kilimo cha mpunga na kuwezesha kulimwa ekari 3,905 kwa utaratibu ufuatao:-

i. Ekari 2,703 kwa matrekta ya Serikali

ii. Ekari 1,082.75 kwa matrekta binafsi.
iii. Ekari 36.25 kwa kutumia plau.
iv. Ekari 78.50 kwa jembe la mkono.

Mhe. Spika, katika kuendeleza sekta ya utalii, uongozi wa Mkoa umefanya mikutano mitatu na wawekezaji ili kuimarisha maendeleo ya sekta, jamii na Taifa.

Mhe. Spika, katika kuwajengea uwezo wafanyakazi, Mkoa umeendelea kuwapatia mafunzo wafanyakazi 12; Shahada ya Kwanza katika fani ya mipango - 1, shahada ya pili fani ya sheria - 1, Stashahada ya utunzaji kumbukumbu - 2, Stashahada katika fani ya utunzaji wa ghala - 1, Stashahada katika fani ya ukarani – 4, cheti katika fani ya ukarani – 1, Stashahada ya Rasilimali Watu – 1 na Stashahada ya Manunuzi na Ugavi– 1.

Mhe. Spika, katika kutekeleza lengo la kuendeleza jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na Wilaya, matengenezo ya ukuta yamefanyika kwa Ofisi ya Mkoa, aidha ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kati umeendelezwa.

Mhe. Spika, Mkoa umeendelea kutoa elimu ya V.V.U na UKIMWI kwa wafanyakazi na wananchi hususan walio katika maeneo hatarishi zaidi. Jumla ya wafanyakazi 38 na wajumbe 12 wa Kamati za UKIMWI za shehia walipatiwa elimu hiyo. Aidha, wananchi wameendelea kupatiwa huduma za ushauri nasaha na kupima kwa hiari ambapo kwa Wilaya ya Kati watu 5,148 walichunguzwa na waliogundulika na virusi ni watu 134 sawa asilimia 2.6. Kwa upande wa Wilaya ya Kusini watu waliochunguzwa ni 2,492 kati yao watu 34 waligunduliwa na virusi vya UKIMWI sawa na asilimia 1.4.

Muelekeo na Malengo ya Mwaka 2014/2015.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Mkoa umekusudia kuendelea kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kusimamia shughuli za Ulinzi na Usalama.
ii. Kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi ili kuongeza ufanisi kazini.
iii. Kuweka mazingira bora ya utendaji kazi kwa kuimarisha ofisi na upatikanaji wa vitendea kazi.
iv. Kuratibu, kusimamia, kufuatilia na kusaidia utekelezaji wa shughuli za sekta mbali mbali katika Mkoa na
v. Kuratibu masuala mtambuka

Mhe. Spika, ili Mkoa wa Kusini Unguja uweze kutekeleza malengo yake vizuri na kwa ufanisi, kwa mwaka wa Fedha 2014/2015 naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya TZS. 1,362,700,000/= kwa matumizi ya kawaida.

MKOA WA KASKAZINI PEMBA

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Mkoa wa Kaskazini Pemba ulikusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuimarisha mazingira bora ya kazi na kuona wafanyakazi wanawajibika ipasavyo;
ii. Kuimarisha ulinzi na usalama wa raia na mali zao;
iii. Kusimamia, kuratibu na kufuatilia shughuli mbali mbali za kisekta na maendeleo ya Mkoa;
iv. Kuwajengea uwezo wa kielimu wafanyakazi saba (7) kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi; na
v. Kuwajengea uwezo wafanyakazi juu ya kujikinga na maambukizi mapya ya VVU na UKIMWI.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Mkoa wa Kaskazini Pemba uliidhinishiwa jumla ya TZS. 1,557,030,000/= kwa kazi za kawaida. Kati ya hizo TZS. 280,000,000/= ni Ruzuku ya Baraza la Mji Wete. Hadi kufikia mwezi wa Machi 2014, Mkoa umeingiziwa TZS. 1,003,351,365/= sawa na asilimia 64 ya makadirio ya matumizi.

Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2013/2014

Mhe. Spika, katika kuimarisha mazingira bora ya kazi na kuona wafanyakazi wanawajibika ipasavyo Mkoa umefanikiwa kuwalipa wafanyakazi stahili zao ikiwemo mishahara, maposho na michango ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Aidha, Ofisi imenunua Vifaa vya kufanyia kazi na kufanya ukarabati mkubwa wa Ofisi ya Ofisa Elimu Mkoa ambayo ilikuwa katika hali duni kwa muda mrefu.

Mhe. Spika, hali ya ulinzi na usalama katika Mkoa wa Kaskazini Pemba inaendelea vizuri. Wananchi wanaendelea na shughuli zao za uzalishaji mali kama kawaida. Mkoa unaendelea kushajihisha suala zima la ulinzi shirikishi katika Shehia zote 59 zilizomo ndani ya Mkoa.

Mhe. Spika, kwa Msimu huu wa Karafuu, Mkoa wa Kaskazini Pemba ulianzisha Operesheni maalum ya kupambana na magendo ya karafuu na kufanikiwa kwa kiasi kikubwa. Aidha, Uongozi wa Mkoa wa Kaskazini, umeunda Kikundi Kazi kilichopelekea kuanzishwa kwa mageti ya vizuizi vya barabarani ikiwa ni njia moja wapo ya kudhibiti magendo ya karafuu. Lengo la kuwekwa vizuizi hivyo ilikuwa ni kufanya upekuzi ndani ya magari ya abiria na mizigo, kuhakikisha kuwa karafuu hazihamishwi kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyengine bila ya kufuata utaratibu au kwenda kinyume na Sheria.

Mhe. Spika, Mkoa wa Kaskazini Pemba kupitia Shirika la Biashara la *ZSTC* umesimamia manunuzi ya zao la karafuu kutoka kwa wakulima na kufanikiwa kununua karafuu kavu gunia 34,693 zenye thamani ya TZS. 21,842,717,000/- hadi kufikia tarehe 31/01/2014.

Mhe. Spika, Mkoa umeratibu na kusimamia miradi 20 ya maendeleo iliyoanzishwa na wananchi. Utekelezaji wa miradi hiyo na hatua iliyofikiwa unaonekana katika *Kiambatisho Namba 6*. Aidha, jumla ya vikundi 25 pamoja na SACCOS zimetembelewa na kupatiwa taaluma mbali mbali na ushauri.

Mhe. Spika, Kamati za Mazingira za Wilaya zimeundwa, Kamati za UKIMWI na zile za Maafa ambazo zinaendelea na shughuli za uhamasishaji wananchi juu ya uhifadhi wa mazingira na kujikinga na maradhi ya kuambukiza na namna ya kukabiliana na maafa mbali mbali.

Mhe. Spika, kwa upande wa Wilaya ya Micheweni Kamati ya Maafa ilikutana na kujadili hali na namna ya kuwafariji wananchi wa Shehia ya Micheweni, Shumba Mjini na Maziwang'ombe kutokana na maafa ya moto yaliyotokea mwanzoni mwa mwaka huu na kupelekea kuundwa kwa Kamati ndogo katika Shehia za Maziwang'ombe na Shumba Mjini ambazo zitasimamia Ukarabati wa nyumba hizo. Jumla ya nyumba 55 zimeungua moto.

Mhe. Spika, katika kuwajengea uwezo wa kielimu wafanyakazi ili waweze kumudu majukumu kwa ufanisi zaidi, Serikali ya Mkoa imewasomesha wafanyakazi wake saba (7) katika fani mbali mbali kama ifuatavyo:-

Teknolojia ya Habari ngazi ya cheti – 2, Rasilimali watu ngazi ya cheti – 2, Manunuzi na Ugavi ngazi ya cheti – 1, Biashara na Utawala ngazi ya Diploma – 1 na Shahada ya Pili katika fani ya Sheria - 1. Aidha, Mkoa ulifanya semina moja juu ya UKIMWI na athari za unyanyapaa kwa wafanyakazi wote 36 wa Mkoa, Semina kama hizo pia zimefanyika katika ngazi za Wilaya.

Mhe. Spika, shughuli nyengine zilizotekelezwa na Mkoa ni pamoja na:-

i. Kikao cha pamoja na wadau mbali mbali kujadili masuala ya unyanyasaji wa kijinsia na wimbi la ubakaji ndani ya Mkoa. Wadau wenyewe ni Maafisa wa Polisi, waendeshaji wa kesi, Viongozi wa dini, Maafisa Ustawi, Maafisa wanawake na watoto, Daktari na Walimu. Katika kikao hicho, Mkoa uliweka mikakati na maazimio ya kupunguza tatizo hilo.
ii. Vikao 12 vya Kamati ya Ulinzi na Usalama vya kawaida na vikao 5 vya dharura na kujadili masuala mbali mbali ya kiusalama.

iii. Ukaguzi wa Vituo 17 vya Mitihani ya darasa la saba (7), darasa la kumi (Form II) na darasa la kumi na mbili (*Form IV*) kwa mwaka 2013.

iv. Uratibu wa vikao 2 vya walimu wa Wilaya ya Wete na Micheweni ili kuwapongeza walimu kwa matokeo mazuri ya wanafunzi wa kidato cha pili na darasa la saba na pia kuwaomba walimu kutilia mkazo zaidi ili wanafunzi wapende kusoma masomo ya sayansi na hesabu.

v. Ufuatiliaji wa karibu wa miradi ya usambazaji wa maji safi na salama kwa mijini na vijijini. Miradi yenyewe ni;

Ujenzi wa Tangi la Maji Taifu, Ujenzi wa Tangi la Maji Mtemani Wete, Ujenzi wa Matangi mawili ya Maji Bahanasa na Uchimbaji wa Kisima Kambini Mchanga Mdogo.

vi. Ufuatiliaji na usimamizi wa ujenzi wa Barabara 5 za Mkoa wa Kaskazini. Mradi huo umefadhiliwa na Jumuiya ya watu wa Marekani MCA-T na hadi sasa barabara hizo zimekamilika na kufunguliwa rasmi na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tarehe 29/03/2014.

vii. Ufuatiliaji wa ujenzi wa barabara ya Wete – Gando na Wete – Konde mradi unatekelezwa na Jumuia ya *BADEA* kupitia Kampuni ya *MECCO*. Mradi huu bado unaendelea.

viii. Umesimamia kilimo cha mpunga ekari 9,857.75, zilizolimwa kwa kutumia jembe la mkono ni ekari 7,457.75 na zilizolimwa kwa trekta ni ekari 2400. Kiasi cha tani 4,670 za mpunga zilivunwa kwa msimu huo.

ix. Umesimamia uandikishaji wa watoto 6,469 waliofikia umri wa kuanza darasa la kwanza katika Skuli mbali mbali kati ya hao wanawake ni 3,207 na wanaume ni 3,262.

x. Mkoa umefanya vikao 2 kujadili hali ya Usafiri na usalama wa barabarani. Wadau walioshiriki katika vikao hivyo ni:- Wenyeviti wa madereva, madereva wenyewe, wamiliki wa magari ya abiria, Polisi wa Usalama Barabarani, wanaosimamia njia za magari, baadhi ya Jumuiya za kiraia, waendeshaji wa mashitaka na baadhi ya Masheha.

xi. Mkoa umefanya vikao 4 vya Bodi ya Zabuni kwa ajili ya kujadili ununuzi wa gari moja ya Ofisi na hadi sasa taratibu za manunuzi bado zinaendelea.

xii. Mkoa umeratibu matukio 67 ya udhalilishaji yakiwemo kubakwa, kulawitiwa, kutoroshwa, kupewa ujauzito, shambulio la aibu, matusi na kupigwa.

xiii. Kufanya ukarabati kwa nyumba ya Mkuu wa Wilaya ya Micheweni. na

xiv. Kusimamia ukarabati wa nyumba 28 katika Shehia ya Shumba Mjini na Nyumba 27 katika Shehia ya Maziwang'ombe ambazo zilipata ajali ya kuungua moto.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015, Mkoa wa Kaskazini Pemba umepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kusimamia amani, Ulinzi na Usalama ndani ya Mkoa kwa kushirikiana na Vyombo vya Ulinzi na Usalama na Wananchi (Polisi Jamii).
ii. Kuimarisha mazingira bora ya kufanyakazi kwa kuhakikisha upatikanaji wa vifaa, huduma na kukarabati majengo.
iii. Kuwajengea uwezo wa kielimu wafanyakazi ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi
iv. Kuratibu vikao na ziara za Viongozi wa Kitaifa na Kimataifa.
v. Kuwajengea uwezo wafanyakazi juu ya kujikinga na maambukizi mapya ya V.V.U na UKIMWI na athari za unyanyapaa.

vi. Kuimarisha uratibu na usimamizi wa utekelezaji wa sekta zilizomo ndani ya Mkoa. na
vii. Kuratibu utekelezaji wa masuala mtambuka.

Mhe. Spika, ili Mkoa wa Kaskazini Pemba uweze kutekeleza kwa ufanisi malengo iliyojipangia kwa mwaka wa fedha 2014/2015, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya TZS. 1,642,000,000/= kati ya fedha hizi Tshs 276,700,000/= ni ruzuku ya Baraza la Mji Wete.

MKOA WA KUSINI PEMBA

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Mkoa wa Kusini Pemba ulikusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuimarisha ulinzi na usalama kwa raia na mali zao;
ii. Kuimarisha uratibu, usimamiaji na ufuatiliaji wa kazi za maendeleo ya Mkoa;
iii. Kuimarisha kiwango cha taaluma kwa wafanyakazi saba kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi;
iv. Kuwajengea uwezo wafanyakazi juu ya kujikinga na maambukizi mapya ya VVU na UKIMWI; na
v. Kuimarisha mazingira bora ya kazi ili kuleta ufanisi, umakini na uwajibikaji.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Mkoa wa Kusini Pemba uliidhinishiwa TZS 1,871000,000, kwa kazi za kawaida na hadi kufikia mwezi wa Machi 2014 Mkoa huu uliingiziwa TZS. 1,477,000,000/= sawa na asilimia 79 ya makadirio ya matumizi.

Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2013/2014

Mhe. Spika, Mkoa umeimarisha doria kwa kuwashirikisha Polisi Jamii. Aidha, umehamasisha jamii kuanzisha vikundi vya Polisi Jamii kwa kila shehia, hali iliyopelekea kupungua kwa vitendo vya uhalifu ikiwemo wizi, matumizi ya madawa ya kulevya na magendo ya karafuu. Jumla ya vikao saba vya Kamati ya Ulinzi na Usalama vimefanyika kutathmini hali ya usalama ndani ya Mkoa.

Mhe. Spika, katika kuimarisha uratibu, usimamiaji na ufuatiliaji wa kazi za maendeleo, Mkoa umefanya vikao sita na wakuu wa taasisi mbali mbali zilizo ndani ya Mkoa kwa ajili ya kujadili mambo mbali mbali yanayohusu Mkoa ikiwa ni pamoja na kupeana taarifa mbali mbali za kiutendaji ndani ya Mkoa. Aidha, vikao vitatu vya masheha na madiwani vimefanyika kwa ajili ya kujenga mashirikiano mema ya kazi baina yao ili kuleta ufanisi.

Mhe. Spika, Mkoa umeweza kusimamia na kuratibu mpango wa Mkoa wa kilimo cha mpunga kwa msimu wa mwaka 2013/2014. Hadi kufikia mwezi wa Machi 2014, jumla ya ekari 9,401 za mpunga zimelimwa.

Mhe. Spika, Mkoa ulisimamia na kufuatilia utekelezaji wa miradi mbali mbali ya wananchi ikiwemo ujenzi wa vituo vya afya Ndagoni, Tasini - Kiwani, Kibokoni na Vikunguni. Pia, ujenzi wa skuli ya Chanjamjawiri, Kilindi, Ng'ambwa, Jambangome na skuli ya sekondari Mkanyageni. Aidha, Mkoa unaendelea kusimamia mradi mkubwa wa maji wa mijini na vijijini unaodhaminiwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*).

Mhe. Spika, Mkoa umefanya ukaguzi wa vituo 34 vya mitihani ya kumalizia darasa la kumi na mbili *(Form IV)*. Vile vile, kufuatia agizo la Mheshimiwa Rais kuhusu kufuatilia utoro katika skuli ya Kengeja, kikao kimoja kimefanyika kilichojumuisha walimu, Kamati ya Skuli na uongozi wa Mkoa kwa kuweka mikakati ya kuzuia utoro skulini hapo. Kiwango cha utoro kimepungua sana na mahudhurio yameongezeka.

Mhe. Spika, kwa upande wa zao la karafuu, Mkoa umeweza kusimamia na kuratibu uokoaji wa zao la karafuu. Kwa msimu uliomalizika, jumla ya tani 3,342 zimepatikana.

Mhe. Spika, mnamo Tarehe 10/02/2014 nchi yetu iliathirika kutokana na upepo mkali ulioambatana na mvua iliyonyesha alfajiri ya tarehe 10/02/2014. Mkoa uliwaagiza masheha kufuatilia na kuripoti athari zilizotokea. Jumla ya nyumba 175 zimeathirika, kati ya hizo nyumba 52 ziliathirika vibaya na kuhamwa. Nyumba 142

zilipata madhara madogo madogo na wamiliki waliweza kuzifanyia ukarabati. Kwa upande wa vipando jumla ya ekari 194 ziliathirika zilizowahusisha wananchi 747. Mkoa uliitisha kikao cha Kamati ya Maafa ya Mkoa na kujadili hali hiyo pia Mkoa uliunda Tume ndogo ili kufanya tathmini kwa upande wa nyumba zilizoharibika. Tathmini hiyo iligundua hasara iliyopatikana ilikua ni TZS. 38,115 milioni kwa zile nyumba 52 zilizoathirika vibaya.

Mhe. Spika, Mkoa umeendelea kuwajengea uwezo wafanyakazi wake kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi katika ngazi na fani mbali mbali. Jumla ya wafanyakazi 6 wanaendelea na masomo katika fani za uchumi, mipango, rasilimali watu na kompyuta.

Mhe. Spika, Mkoa umefanikiwa kutoa mafunzo juu ya mbinu za kujikinga na V.V.U. na athari zitokanazo na UKIMWI. Mafunzo hayo yalitolewa kwa wafanyakazi 74 (wanawake 37 na wanaume 37) na masheha 62 (wanawake 6 na wanaume 56). Aidha, katika mafunzo hayo, washiriki walihamasishwa kupimwa afya zao kwa hiari na matokeo ni kwamba washiriki wote walikuwa salama.

Mhe. Spika, katika kuimarisha mazingira bora ya kazi, Mkoa umewapatia nyenzo na motisha wafanyakazi wake ili waweze kuwajibika ipasavyo na kuleta ufanisi katika kazi. Wafanyakazi wamepatiwa stahiki zao kwa wakati ikiwemo mishahara, posho za likizo, malipo baada ya saa za kazi na zawadi kwa wafanyakazi bora. Aidha, Mkoa umewapatia baadhi ya wafanyakazi vyombo vya usafiri.

Mhe. Spika, katika kuhakikisha kuwa kunakuwepo matumizi sahihi ya fedha za umma, kamati ya uchunguzi wa hesabu imeendelea kufanya kazi zake ikiwa ni pamoja na kupitia na kuchambua taarifa za mkaguzi wa ndani na wakaguzi wa nje na kushauri ofisi kuhusu matumizi bora ya fedha za umma.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Mkoa wa Kusini Pemba umepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuwajengea uwezo wafanyakazi ili waweze kuwajibika na kuweza kufanya majukumu yao kwa ufanisi.
ii. Kuimarisha mazingira bora ya kazi ili kuleta ufanisi, umakini na uwajibikaji ikiwa ni pamoja na kuipatia ofisi vitendea kazi
iii. Kuhakikisha amani, utulivu na usalama unapatikana kwa kulinda raia na mali zao.
iv. Kuimarisha uratibu, usimamiaji na ufuatiliaji wa kazi za maendeleo ya Mkoa.
v. Kuratibu masuala mtambuka kama vile UKIMWI, mazingira na jinsia.

Mhe. Spika, ili Mkoa wa Kusini Pemba uweze kutekeleza malengo yake, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe TZS. 1,916,900,000/= kwa kazi za kawaida. Kati ya hizo TZS. 581,000,000 kwa ajili ya ruzuku ya Mabaraza ya Miji ya Chake Chake na Mkoani.

IDARA MAALUM ZA SMZ

IDARA YA URATIBU WA IDARA MAALUM

Mhe. Spika, Idara ya Uratibu wa Idara Maalum za SMZ ina jukumu la kuratibu na kusimamia kazi za Idara Maalum za SMZ zikiwemo za utekelezaji wa sera, sheria na kanuni za Idara Maalum, kusimamia vikao vya Mahakama ya Rufaa ya Idara Maalum za SMZ. Aidha, Idara ina jukumu la kisera kusimamia mwenendo wa kiutumishi, maslahi ya maafisa na wapiganaji na kuwajengea uwezo wa kiutendaji na kuratibu masuala ya michezo ya pamoja ya Idara Maalum za SMZ na SMT.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara ya Uratibu wa Idara Maalum za SMZ ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuweka mazingira mazuri ya kufanya kazi ili Idara iweze kutoa huduma nzuri;
ii. Kuimarisha uratibu na ufuatiliaji wa shughuli za Idara Maalum za SMZ Unguja na Pemba;

iii. Kuwajengea uwezo wa kiutendaji watumishi wa Idara kwa kuwapeleka mafunzoni ndani na nje ya Zanzibar; na
iv. Kuandaa vikao vya Mahkama ya rufaa vya Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Idara ilitengewa TZS. 141,828,775/= kwa matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia Machi 2014, Idara imeingiziwa TZS. 18,314,775 sawa na asilimia 13 ya fedha zilizoidhinishwa.

Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2013/2014

Mhe. Spika, Idara ya uratibu wa Idara Maalum za SMZ imekamilisha muundo wa utumishi wa Idara Maalum za SMZ (*Scheme of Service*) ili kuimarisha maslahi na majukumu ya watumishi wa Idara hizo, miundo hiyo tayari imeanza kutumika kuanzia tarehe 01 Machi, 2014.

Mhe. Spika, katika kuimarisha uratibu na ufuatiliaji wa shughuli za Idara Maalum za SMZ Unguja na Pemba Idara ya Uratibu imefanya ufuatiliaji wa miradi ya kiuchumi na maendeleo inayotekelezwa na vikosi vya Idara Maalum. Miradi iliyotembelewa ni pamoja na Mradi wa mbogamboga wa Shamba la pamoja JKU Bambi, Mradi wa Kiwanda cha Ushoni, Ujenzi wa Chuo cha Mafunzo Hanyegwa mchana, Hospitali ya KMKM - Kibweni na Ujenzi wa Makao Makuu ya KVZ – Mtoni. Aidha, ufuatiliaji wa shughuli za kawaida umefanyika kwa upande wa vikosi - Pemba.

Mhe. Spika, katika kuwaendeleza watumishi kitaaluma, mfanyakazi mmoja anaendelea kupatiwa mafunzo ya muda mrefu katika fani ya Mipango ya Maendeleo.

Mhe. Spika, Idara ya Uratibu imeandaa vikao viwili vya Mahkama ya Rufaa ya Idara Maalum za SMZ. Katika vikao hivyo jumla ya kesi sita zimesikilizwa na kati ya hizo kesi tatu zimetolewa maamuzi.

Mhe. Spika, Kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Idara ya Uratibu wa Idara Maalum za SMZ imepanga kuendelea kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuweka mazingira mazuri ya kufanya kazi ili Idara iweze kutoa huduma nzuri.
ii. Kuimarisha uratibu na ufuatiliaji wa shughuli za Idara Maalum za SMZ Unguja na Pemba.
iii. Kuwajengea uwezo wa kiutendaji watumishi wa Idara kwa kuwapeleka mafunzoni ndani na nje ya Zanzibar; na
iv. Kuandaa vikao vya Mahkama ya Rufaa vya Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 idara ilitengewa TZS. 141,828,775/= kwa matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia Machi 2014, Idara imeingiziwa TZS. 18,314,775 sawa na asilimia 13 ya fedha zilizoidhinishwa.

Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2013/2014

Mhe. Spika, Idara ya Uratibu wa Idara Maalum za SMZ imekamilisha muundo wa utumishi wa Idara Maalum za SMZ (*Scheme of Service*) ili kuimarisha maslahi na majukumu ya watumishi wa Idara hizo, miundo hiyo tayari imeanza kutumika kuanzia tarehe 01 Machi, 2014.

Mhe. Spika, katika kuimarisha uratibu na ufuatiliaji wa shughuli za Idara Maalum za SMZ Unguja na Pemba Idara ya Uratibu imefanya ufuatiliaji wa miradi ya kiuchumi na maendeleo inayotekelezwa na vikosi vya Idara Maalum. Miradi iliyotembelewa ni pamoja na Mradi wa mbogamboga wa Shamba la pamoja JKU Bambi, Mradi wa Kiwanda cha Ushoni, Ujenzi wa Chuo cha Mafunzo Hanyegwa mchana, Hospitali ya KMKM - Kibweni na Ujenzi wa Makao Makuu ya KVZ – Mtoni. Aidha, ufuatiliaji wa shughuli za kawaida umefanyika kwa upande wa vikosi - Pemba.

Mhe. Spika, katika kuwaendeleza watumishi kitaaluma, mfanyakazi mmoja anaendelea kupatiwa mafunzo ya muda mrefu katika fani ya Mipango ya Maendeleo.

Mhe. Spika, Idara ya Uratibu imeandaa vikao viwili vya Mahkama ya Rufaa ya Idara Maalum za SMZ. Katika vikao hivyo jumla ya kesi sita zimesikilizwa na kati ya hizo kesi tatu zimetolewa maamuzi.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Idara ya Uratibu wa Idara Maalum za SMZ imepanga kuendelea kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kuweka mazingira mazuri ya kufanya kazi ili Idara iweze kutoa huduma nzuri.
2. Kuimarisha uratibu na ufuatiliaji wa shughuli za Idara Maalum za SMZ Unguja na Pemba.
3. Kuwajengea uwezo wa kiutendaji watumishi wa Idara kwa kuwapeleka mafunzoni ndani na nje ya Zanzibar; na
4. Kuandaa vikao vya Mahkama ya Rufaa vya Idara Maalum za SMZ.
5. Kuratibu Shughuli za kilimo na kuhakikisha matumizi bora ya matrekta yaliyopo na mapya manne yaliyotolewa na Serikali hivi karibuni.

Mhe. Spika, Ili Idara ya Uratibu wa Idara Maalum za SMZ iweze kutekeleza malengo yake kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya TZS. 78,128,000/= kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida.

Mhe. Spika, maelezo kamili yanapatikana katika kitabu cha hotuba yangu ukurasa namba 55 hadi ukurasa namba 58.

TUME YA UTUMISHI IDARA MAALUM ZA SMZ

Mhe. Spika, Tume ya Utumishi Idara Maalum za SMZ, imeanzishwa kwa Sheria Nam. 6 ya mwaka 2007, na ina jukumu kubwa la kusimamia shughuli za utumishi katika Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Tume ya Utumishi ya Idara Maalum ilikusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

(i) Kuimarisha mazingira bora ya Utumishi wa Idara Maalum;
(ii) Kutoa elimu kwa Maafisa na Wajumbe wa Tume ya Utumishi ya Idara Maalum za SMZ;
(iii) Kuhakikisha kazi za Tume zinafanyika ipasavyo; na
(iv) Kufuatilia ajira na maslahi ya watumishi wa Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Tume ya Utumishi ya Idara Maalum iliidhinishiwa TZS 46,636,975/= kwa matumizi ya kazi za kawaida, hadi kufikia mwezi wa Machi, 2014 Tume ya Utumishi ya Idara Maalum imeingiziwa jumla ya TZS 20,991,500/= sawa na asilimia 45 ya bajeti iliyoidhinishwa.

Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2013/2014

Mhe. Spika, Katika kuimarisha mazingira bora ya Utumishi wa Idara Maalum, Tume imenunua vifaa vya kufanyiakazi ikiwemo samani na shajari.

Mhe. Spika, Tume imeendesha mafunzo ya Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2/2011 na Sheria ya Tume ya Utumishi wa Idara Maalum Nam. 6/2007 kwa Wakuu wa Idara Maalum na Maafisa Waandamizi wa Idara Maalum za SMZ ili kujenga uelewa wa Sheria hizo kwa watendaji hao. Aidha, Tume imefanya semina kuhusu Muundo wa Utumishi wa Idara Maalum za SMZ kwa Wakuu wa Idara Maalum za SMZ na pia imesimamia na kuendesha zoezi la ajira kwa watumishi wa Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Spika, katika kuhakikisha kazi za Tume zinafanyika ipasavyo, Tume imefanya vikao vinne vya kawaida vilivyojadili utendaji kazi wa Idara Maalum za SMZ katika masuala ya kiutumishi.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Tume ya Utumishi ya Idara Maalum za SMZ inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

(i) Kuhakikisha upatikanaji wa watumishi wenye sifa katika Idara Maalum pamoja na kuboresha mazingira ya utendaji kazi wa Tume; na

(ii) Kuimarisha Utawala Bora katika Idara Maalum za SMZ.
(iii) Kutoa elimu kwa Maafisa na Wajumbe wa Tume ya Utumishi ya Idara Maalum za SMZ;
(iv) Kuhakikisha kazi za Tume zinafanyika ipasavyo; na
(v) Kufuatilia ajira na maslahi ya watumishi wa Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Spika, Ili Tume ya Utumishi ya Idara Maalum za SMZ iweze kutekeleza malengo yake kwa ufanisi, katika mwaka wa fedha 2014/2015, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe TZS. 68,500,000/= kwa matumizi ya kazi za kawaida.

Mhe. Spika, maelezo kamili yanapatikana katika kitabu cha hotuba yangu ukurasa wa 58 hadi ukurasa namba 60.

KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO (KMKM)

Mhe. Spika, Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) kimeanzishwa kwa Sheria Namba 1 ya 2003 na kina majukumu ya kulinda usalama wa bahari ya Zanzibar. Kuzuia njia zote zinazoweza kutumika kupitisha magendo, kusaidia usalama wa vyombo vya baharini ikiwemo vya abiria, mizigo na watumiaji wengine wa bahari pamoja na uokozi baharini na kuongoza misafara ya viongozi katika shughuli maalum wanapotumia usafiri wa bahari.

Mhe. Spika, Kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

a. Kuwapatia chakula bora askari wanapokuwa kazini na mafunzoni;
b. Kuimarisha hali ya ulinzi wa doria;
c. Kuimarisha sehemu ya uzamiaji kikosini;
d. Kuhakikisha kuwa maofisa na wapiganaji wanawajibika ipasavyo kwa kupatiwa stahiki zao;
e. Kuwapatia sare maofisa na wapiganaji wote;
f. Kuendeleza kuwapatia elimu ndani na nje ya kikosi na
g. Kuendeleza ukarabati wa majengo ya kikosi Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kiliidhinishiwa jumla ya TZS. 10,693,819,480/= kwa matumizi ya mishahara na maposho pamoja na kazi za kawaida. Hadi kufikia mwezi Machi, 2014 Kikosi cha KMKM kimeingiziwa jumla ya TZS. 7,770,035,258/= sawa na asilimia 73 ya fedha zilizoombwa.

Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2013/2014

Mhe. Spika, Kikosi cha KMKM kimetoa huduma ya chakula kwa askari kama kilivyojipangia. Katika suala zima la kuhifadhi mazingira, Kikosi kimeanza kutumia majiko ya gesi katika kambi ya Makao Makuu Kibweni. Aidha, Kikosi kimejipanga kuendeleza matumizi hayo katika Ofisi Kuu ya KMKM – Wete - Pemba na Chuo cha KMKM – Kama.

Mhe. Spika, Kikosi cha KMKM kimeendelea na operesheni za doria katika maeneo mbalimbali yanayozunguka Zanzibar. Katika Operesheni hizo, kikosi kimeweza kudhibiti utoroshwaji wa zao la karafuu kwa asilimia kubwa na jumla ya matukio sita (6) ya magendo ya bidhaa mbali mbali yamedhibitiwa. Bidhaa hizo ni pamoja na; Mafuta ya diseli lita 5,800, Sukari Kilo 5,300, Mchele kilo 9,650, Karafuu kavu kilo 8,285, Makonyo ya karafuu kilo 3,000 na mifuko ya plastiki katuni tisa.

Mhe. Spika, katika kujiimarisha zaidi na shughuli za doria, Kikosi kimefanya matengenezo makubwa ya vyombo vikubwa na vidogo vya doria na kujiweka katika hali ya utayari ili kukabiliana na matokeo ya uhalifu. Aidha, vyombo vikubwa viwili (2) tayari vimefanyiwa ukaguzi wa kitaalam na wataalam kutoka Kampuni ya *Damen Shipyards* ya Uholanzi.

Mhe. Spika, katika kuimarisha nguvu za ulinzi, kikosi kimeweza kuongeza vifaa vya mawasiliano kwa kununua "*repeater*" moja (1) na *radio walktalk* nane (8) pamoja na kuyafanyia matengenezo baadhi ya magari.

Mhe. Spika, Kikosi cha KMKM kimeendelea kuimarisha sehemu ya uzamiaji kwa kuipatia vifaa mbalimbali vikiwemo makoti ya uokozi jozi 200, taa za kuongozea vyombo vya baharini na vigari vitatu vya kubururia boti ndogo. Aidha, mazungumzo kuhusu uendeshaji wa mafunzo ya awamu ya pili ya uzamiaji yanaendelea baina ya Kikosi na wakufunzi kutoka Uingereza.

Mhe. Spika, katika kuwapatia wapiganaji stahiki zao, Kikosi kimeweza kulipa mishahara na maposho kwa askari wake. Aidha, askari 180 wamelipwa posho la likizo na askari 23 wamelipwa fidia.

Mhe. Spika, kikosi kimeweza kuwapatia sare mbalimbali Maafisa na Askari wake zikiwemo "*combat*" jozi 150, viatu vya buti jozi 200, sare za Sherehe za Miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar na fulana za fatiki jozi 3,000.

Mhe. Spika, Kikosi cha KMKM kimeweza kuwapatia elimu wapiganaji wake katika fani mbalimbali kwenye vyuo vya ndani na nje ili kuwajengea uwezo wa kiutendaji. Jumla ya wafanyakazi 50 wamepatiwa mafunzo katika fani zifuatazo: Ubaharia Daraja la pili (1), Uhandisi wa meli Daraja la pili (1), Uhasibu (1), Usimamizi wa Bahari (1), Sheria (Shahada ya kwanza 1), Utawala (Shahada ya kwanza 1), Uuguzi (Shahada ya kwanza 1), Utawala wa Biashara (Shahada ya Kwanza 1), Uuguzi (Diploma 8), Famasia (Diploma 1), Maabara (Diploma 2), Ofisa wa Afya (Diploma 1), Teknolojia ya Mawasiliano ya Habari na Uhasibu (Diploma 2), Sheria (Cheti 3), Ufundi umeme (Cheti 17) na Fundi Mekaniki (Cheti 8). Pia, Kikosi kimeweza kuendesha mafunzo ya ndani kwa wapiganaji wake kwa ngazi tofauti ikiwemo Mafunzo ya Uongozi, Uofisa na mafunzo ya awali.

Mhe. Spika, kikosi kimefanya ukarabati wa majengo mbalimbali, ikiwemo utiaji wa "*fitting*" na uungaji wa umeme katika Kambi ya Tumbatu na upakaji wa rangi majengo yake ya Makao Makuu Kibweni. Aidha, Kikosi kimefungua jengo lake jipya la Hospitali ambapo kwa hivi sasa huduma mbalimbali za matibabu zinatolewa zikiwemo huduma ya mama na mtoto, matibabu ya meno, macho, maskio pamoja na ushauri nasaha wa masuala ya V.V.U. na UKIMWI.

Mhe. Spika, Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kwa mwaka wa fedha 2014/2015 kimejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

(i) Kujenga na kukarabati majengo katika kambi za Kikosi
(ii) Kuweka mazingira mazuri ya kazi na ustawi wa wapiganaji
(iii) Kuimarisha nguvu za ulinzi wa magendo kwa kuimarisha doria; na
(iv) Kutoa huduma bora za uokozi Afya na endelevu kwa wapiganaji na raia.

Mhe. Spika, Ili Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kiweze kutekeleza malengo yake kiliyojipangia kwa mwaka 2014/2015 naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya TZS. 12,266,800,000/- kati ya fedha hizo TZS. 9,231,000,000/- ni mshahara na maposho, TZS. 2,535,800,000/- ni kwa matumizi ya kazi za kawaida na TZS 500,000,000/- kwa ajili ya matumizi ya kazi za maendeleo. Aidha, Kikosi kimekadiria kukusanya mapato ya TZS. 15,830,000/= kupitia shughuli za ujenzi.

Mhe. Spika, maelezo kamili yanapatikana katika kitabu cha hotuba yangu kwenye ukurasa namba 60 hadi ukurasa namba 65.

JESHI LA KUJENGA UCHUMI (JKU)

Mhe. Spika, Jeshi la Kujenga Uchumi limeanzishwa kwa Sheria Nam.6 ya mwaka 2003 na lina jukumu kubwa la kutoa mafunzo kwa vijana katika nyanja za kuimarisha uchumi kupitia kilimo, mifugo, uvuvi, ufundi, kazi za amali na mafunzo ya uzalendo na ulinzi wa nchi yao. Vijana wanaojiunga na JKU hupatiwa mafunzo kwa lengo la kuwawezesha kujiajiri wenyewe au waweze kuajirika wakati wanapomaliza mafunzo yao.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Jeshi la Kujenga Uchumi lilikusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

(i) Kutoa mafunzo kwa vijana wanaojiunga na JKU katika nyanja za kilimo, mifugo, ufundi, kazi za amali na ulinzi wa Taifa ili waweze kujitegemea na kuijenga nchi yao;
(ii) Kuwapatia wapiganaji sare na vifaa;
(iii) Kutoa mafunzo kwa watumishi ili kuongeza ufanisi wa kazi;
(iv) Kuimarisha mashirikiano na Taasisi mbali mbali ndani na nje ya Zanzibar; na

(v) Kuimarisha utoaji wa huduma kwa wana JKU na jamii kwa ujumla.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, JKU iliidhinishiwa jumla TZS 7,457,000,000/= kwa kazi za kawaida na TZS 250,000,000/= kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi 2014, Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) limeingiziwa jumla ya TZS 6,655,855,655 sawa na asilimia 89 ya matumizi ya kazi za kawaida, na fedha kwa ajili ya kazi za maendeleo hazikupatikana.

Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2013/2014

Mhe. Spika, Jeshi la Kujenga Uchumi limeendelea kutoa mafunzo ya uzalendo na uzalishaji katika kilimo na mifugo kwa vijana 600 (Unguja 400 na Pemba 200) na mafunzo ya ufundi na kazi za amali kwa vijana 490 (Unguja 300 na Pemba 190)

Mhe. Spika, J.K.U. imeweza kuwapatia maofisa, wapiganaji na vijana sare pamoja na vifaa mbalimbali vya kufanyia kazi. Aidha, sare maalum kwa ajili ya sherehe za maadhimisho ya Miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar zilipatikana.

Mhe. Spika, JKU imeweza kuwapeleka mafunzoni ndani na nje ya Zanzibar watumishi wake 15 (wanawake 3 na wanaume 12) katika ngazi na fani zifuatazo: watumishi 2 (ngazi ya shahada ya uzamili katika fani za Uchumi wa Kilimo na Utawala wa Biashara), (2 shahada ya kwanza katika fani za Rasilimali watu), (1 Shahada ya Kwanza katika fani ya Afya), (2 Stashahada ya juu ya afya), (watumishi 4 Stashahada ya Sayansi ya Afya na watumishi 4 ngazi ya Cheti cha Kilimo na Mifugo. Aidha, wapiganaji 30 (wanawake 12, wanaume 18) wamepelekwa Jeshi la Wananchi Tanzania kwa mafunzo ya uongozi. Kati ya hao 20 kwa mafunzo ya Uongozi Mdogo na 10 Uongozi Mkubwa. Pia, maofisa 10 (wanawake 4, wanaume 6) wamehitimu mafunzo ya Uofisa yaliyoendeshwa na Chuo cha KMKM. Vilevile, maofisa 37 (wanawake 5, wanaume 32) wanaendelea na mafunzo ya Uongozi wa Platuni.

Mhe. Spika, katika kuimarisha mashirikiano na taasisi mbali mbali za ndani na nje ya Zanzibar, wakuu wa vikosi na Kambi za JKU wamefanya ziara za mafunzo JKT - Tanzania Bara, vilevile wakuu wa vikosi na Kambi za JKT walifanya ziara kama hizo Zanzibar. Aidha, ziara za kubadilishana uzoefu zimefanyika kwa wanamichezo wa JKU na JKT. Pia, Mkuu wa JKU alifanya ziara katika vikosi mbalimbali vya JKT na Mkuu wa JKT alifanya ziara katika vikosi vya JKU Unguja na Pemba. Vile vile, timu ya mpira wa pete imeweza kushiriki katika mashindano ya klabu bingwa Afrika Mashariki na Kati na kufanikiwa kuwa mshindi wa pili.

Mhe. Spika, JKU imeweza kutoa huduma kwa watumishi wake na jamii kwa ujumla. Watumishi wa JKU wamepatiwa mishahara na maposho, huduma za chakula kwa maofisa na wapiganaji pamoja na kuwapatia vitendea kazi ikiwemo vifaa vya michezo.
Aidha, kupitia vituo vya afya vya JKU huduma kwa wana JKU na raia wa maeneo ya jirani na vituo hivyo zimetolewa. Kwa mwaka 2013/2014 jumla ya wagonjwa 19,520 wamepatiwa huduma tofauti za afya zikiwemo huduma za mama na mtoto, ushauri nasaha na upimaji wa VVU.

Mhe. Spika, katika kusaidia jamii, JKU imeshiriki katika shughuli mbali mbali ikiwemo usafishaji wa mji na maeneo ya Hospitali ikiwemo Mnazi Mmoja, Kidongo Chekundu, Makunduchi, Kivunge na Chake chake Pemba. Aidha, JKU ilitoa mapipa ya kuhifadhia taka katika Hospitali hizo. Sambamba na hili JKU imekuwa ikishiriki sana katika uchangiaji wa damu salama.

Mhe. Spika, pamoja na kutekeleza majukumu waliyojipangia, JKU imemudu kutekeleza kazi za ziada kwa kutumia vyanzo vyake vya ndani. Miongoni mwa kazi hizo ni pamoja na kuanza ujenzi wa jengo la ghorofa tatu litakalotumika kwa madarasa, maabara, maktaba na ofisi ya Skuli ya Sekondari ya JKU. Ujenzi wa nyumba za mapumziko Gombani Pemba, ujenzi wa bwalo la chakula na mikutano kwa ajili ya vijana wa JKU Bambi pamoja na upanuzi wa mabanda ya kufugia kuku JKU Kama lenye uwezo wa kuchukua kuku 2,500.

Mhe. Spika, JKU kwa mwaka 2014/2015 imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

(i) Kutoa mafunzo kwa vijana 1,620 katika nyanja za kilimo, mifugo na ulinzi wa Taifa

(ii) Kuwawezesha watumishi wa JKU kushiriki kikamilfu katika shughuli za ulinzi wa raia na mali zao na kuimarisha amani na utulivu wa Taifa

(iii) Kutengeneza mazingira bora ya kazi kwa wana JKU kwa ajili ya kuwahudumia vijana na jamii kwa ujumla; na
(iv) Kuendeleza Miradi ya Maendeleo ikiwemo kilimo, ufugaji, uvuvi na mambo mengine yatakayosaidia kukuza uchumi wetu.

Mhe. Spika, Ili Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) liweze kutekeleza malengo yake kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya TZS. 9,482,600,000/= kwa kazi za kawaida na TZS. 150,000,000/= kwa kazi za maendeleo.

Mhe. Spika, maelezo kamili yanapatikana katika kitabu cha hotuba yangu ukurasa namba 65 hadi ukurasa namba 69

CHUO CHA MAFUNZO (MF)

Mhe. Spika, Chuo cha Mafunzo kimeanzishwa kwa Sheria Namba 1 ya mwaka 1980 na Sheria ya marekebisho Namba 3 ya mwaka 2007, kikiwa na jukumu kuu la urekebishaji, udhibiti na ulinzi wa wanafunzi na mahabusu wanaoletwa chuoni kwa mujibu wa Sheria. Idara pia ina jukumu la kushirikiana na vyombo vyengine vya ulinzi na usalama katika kuimarisha ulinzi wa nchi, wananchi na mali zao kwa ujumla.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Idara ya Chuo cha Mafunzo ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

(i) Kuimarisha huduma bora za urekebishaji tabia kwa wanafunzi na mahabusu, kuwaendeleza na kuwajengea uwezo wanaporudi katika jamii;
(ii) Kuhakikisha haki za binaadamu zinatolewa kwa wanafunzi na mahabusu kwa mujibu wa sheria za nchi, kikanda na makubaliano ya Kimataifa;
(iii) Kuweka mazingira mazuri ya kazi, maendeleo na ustawi wa maofisa na wapiganaji pamoja na usimamizi mzuri wa fedha; na
(iv) Kuendelea na ujenzi wa Chuo kipya cha Mafunzo Hanyegwa mchana.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara ya Chuo cha Mafunzo iliidhinishiwa TZS. 6,099,000,000/= kwa matumizi ya kazi za kawaida na TZS. 300,000,000/= kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Machi 2014, Idara iliingiziwa TZS. 5,106,200,000/= sawa na asilimia 84 ya fedha zilizoidhinishwa kwa kazi za kawaida na TZS. 30,000,000/= sawa na asilimia 10 kwa ajili ya mradi wa maendeleo.

Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2013/2014

Mhe. Spika, katika kuimarisha utoaji wa huduma bora za urekebishaji tabia kwa wanafunzi, kuwaendeleza na kuwajengea uwezo wanaporudi katika jamii, Idara imeandaa program ya elimu ya watu wazima, na tathmini ya mahitaji ya uanzishwaji wa programu hiyo imeshaandaliwa. Aidha, mchakato wa kuzifanyia marekebisho Sheria namba 1 ya mwaka 1980 na Sheria namba 3 ya mwaka 2007 za Chuo cha Mafunzo unaendelea. Mchakato huo umewashirikisha wataalam wa Idara, wanafunzi na mahabusu, maofisa na wapiganaji wa Idara pamoja na wadau mbali mbali kutoka taasisi za Serikali kwa lengo la kupata maoni yao ili Sheria itakayoandaliwa iweze kukidhi mahitaji ya shughuli za Idara.

Mhe. Spika, Katika kuhakikisha haki za binadamu zinatolewa kwa wanafunzi, mahabusu na watumishi wa Idara, Idara imeweza kuwapatia chakula cha kutosha, sare na mahitaji mengine mbalimbali. Ili kuwawezesha wanafunzi kupata habari za ulimwengu na burudani, Idara imeweka Televisheni na ving'amuzi kwa kambi zote za Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, Idara imefanya ukarabati wa majengo ya kambi ya Kinumoshi, Ubago na Hanyegwa Mchana kwa Unguja na Kengeja na Kangagani kwa upande wa Pemba. Ili kuimarisha afya za wapiganaji, Idara imewapatia vifaa mbali mbali vya michezo kwa timu za mpira wa miguu, mpira wa pete na wavu pamoja na kugharamia safari za kimichezo ndani ya nchi.

Mhe. Spika, Katika kuweka mazingira mazuri ya kazi Idara imekamilisha ujenzi wa nyumba ya familia mbili iliyopo Kangagani Pemba, aidha, imefanya matayarisho ya vifaa vya ujenzi wa msingi wa ofisi ya Kamanda Mkuu iliyopo Wete Pemba. Ukarabati wa ofisi ya Mkuu wa Utawala, ofisi ya manunuzi na Makao Makuu ya

Idara yamefanyika. Huduma mbali mbali za ofisi ikiwemo upulizaji wa dawa za kuulia wadudu katika kambi, upatikanaji wa sare na vifaa mbali mbali vikiwemo vifaa vya *Brass Band* kwa ajili ya maadhimisho ya sherehe za miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar vimepatikana.

Mhe. Spika, Katika kutekeleza shughuli za mradi wa maendeleo Idara pia imeweza kuendelea na ujenzi wa ukuta wenye urefu wa mita 544 wa Chuo kipya cha Mafunzo Hanyegwa Mchana.

Mhe. Spika, Kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara ya Chuo Cha Mafunzo imekusudia kuendelea kutekeleza malengo yafuatayo:-

(i) Kuimarisha huduma bora za urekebishaji tabia kwa wanafunzi, kuwaendeleza na kuwajengea uwezo wanaporudi katika jamii;
(ii) Kuhakikisha haki za binaadamu zinatolewa kwa wanafunzi na wale walioko mahabusu kwa mujibu wa Sheria za nchi, kikanda na makubaliano ya kimataifa;
(iii) Kutoa huduma bora za afya kwa wanafunzi, maofisa na wapiganaji pamoja na wananchi wanaoishi karibu na makambi;
(iv) Kuweka mazingira mazuri ya kazi, maendeleo na ustawi wa maofisa na wapiganaji pamoja na usimamizi mzuri wa fedha; na
(v) Kuendelea na ujenzi wa Chuo kipya Cha Mafunzo Hanyegwa Mchana.

Mhe. Spika, ili Chuo cha Mafunzo kiweze kutekeleza majukumu yake, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha TZS. 3,787,500,000 kwa kazi za kawaida.

Mhe. Spika, maelezo kamili yanapatikana katika kitabu cha hotuba yangu ukurasa namba 69 hadi ukurasa namba 73.

KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI (KZU)

Mhe. Spika, Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kimeanzishwa kwa Sheria nambari 7 ya mwaka 1999 na kina jukumu la kusimamia shughuli zote za uzimaji moto na uokozi wa maisha na mali za watu. Vile vile, kikosi kina jukumu la kusimamia na kuhakikisha kuwa huduma za zimamoto na uokozi kwenye viwanja vya ndege vya Unguja na Pemba, zinakwenda sambamba kulingana na sheria na matakwa ya Kitaifa na Kimataifa. Aidha, kikosi kinatoa ushauri wa kujikinga na majanga ya moto kwa taasisi mbali mbali za serikali na za watu binafsi na kutoa huduma za kibinaadamu kulingana na mahitaji.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Kikosi cha zimamoto na Uokozi kilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

(i) Kupunguza muda wa kuwahi kufika katika tukio la moto na majanga mengine bila ya kuzidi dakika 15;
(ii) Kuboresha ujenzi wa vituo na kupatikana vifaa vya kazi vituoni ili kuleta ufanisi wa huduma zinazotolewa;
(iii) Kuwapa motisha wafanyakazi ili kukuza ufanisi na tija kwa aina ya huduma zinazotolewa nchini;
(iv) Kuboresha rasilimali watu kwa kuwapatia maofisa na askari elimu za aina mbalimbali;
(v) Kuendelea kutoa elimu ya tahadhari za moto; na
(vi) Kuongeza uhusiano na mashirikiano ya namna ya kukabiliana na majanga mbalimbali kitaifa na kimataifa.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014, Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kiliidhinishiwa kutumia TZS. 3,113,000,000/= kwa matumizi ya kazi za kawaida na hadi kufikia mwezi wa Machi, 2014 Kikosi kimeingiziwa TZS. 2,567,500,000/= sawa na asilimia 82 ya fedha zilizoidhinishwa. Kwa upande wa mapato, Kikosi kilipangiwa kukusanya jumla ya TZS. 10,000,000/=, hadi kufikia mwezi wa Machi, 2014 kikosi kimeshachangia TZS. 6,000,000/= sawa na asilimia 60 ya makadirio.

Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2013/2014

Mhe. Spika, Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kimeendelea na utekelezaji wa majukumu yake ambapo hadi kufikia Machi 2014, kimeweza kutoa huduma katika ajali 367 zilizoripotiwa Unguja na Pemba kama ifuatavyo; Moto wa majumba 210, Moto wa mahoteli ya Kitalii 25, Moto wa Magari 5, Moto wa Misitu 50, Watu kuingia visimani 6, Wanyama 3, Kuzama watu baharini 2, taarifa za matukio ya moto ambazo si za kweli 10, Moto wa

majaa 20, Moto wa Transfomer za umeme 25, Ajali za Ndege 5, Ajali za kuangukiwa na miti 3, Kuzama kwenye Mabwawa 3.

Mhe. Spika, kwa ujumla ajali hizi zilisababisha vifo vya watu 15 pamoja na hasara inayokadiriwa TZS. 845,250,000/=. Aidha, jumla ya TZS. 3,650,000,000/= zimeokolewa na Kikosi cha Zimamoto wakati wa kuyakabili matukio mbali mbali ya ajali Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, kikosi kimeweza kutoa huduma katika Viwanja vya Ndege Unguja na Pemba ambapo kimeweza kusimamia utuaji, urukaji na utiaji wa mafuta ya ndege kubwa na za kisasa. Jumla ya ndege kubwa 2440 zimepatiwa huduma bila ya matatizo.

Mhe. Spika, katika kuboresha ujenzi wa vituo na upatikanaji wa huduma, Kikosi kimeweza kufanyia matengenezo madogo madogo vituo vyake vyote na kuendelea na ujenzi wa kituo kipya cha Marumbi, Kitogani na M/kwerekwe. Kikosi kimeanza kutoa huduma kwa wilaya ya Wete Pemba na mchakato wa kupatiwa eneo huko Micheweni unaendelea na ujenzi utafanyika mara baada ya kupatikana eneo.

Mhe. Spika, kikosi kimeanza hatua za ujenzi wa kituo kipya cha zimamoto Marumbi Wilaya ya Kati, Mkoa wa Kusini Unguja baada ya kupatiwa hatimiliki ya eneo hilo. Kikosi kinaendelea na mchakato wa kupata Hatimiliki kwa eneo la Muyuni na Tunguu kwa ajili ya ujenzi wa vituo.

Mhe. Spika, kikosi kimewapatia askari wake huduma za chakula, sare na stahiki nyengine zikiwemo maposho ya likizo na safari ili kukuza ufanisi na tija katika kutekeleza majukumu yao. Aidha, Kikosi kimefanikiwa kusomesha wafanyakazi (26) katika ngazi na fani mbali mbali kama ifuatavyo: Sheria (Shahada ya kwanza 3), Usimamizi wa fedha (Diploma 2 na Cheti 6), Utunzaji wa Kumbukumbu (Cheti 3), Uandishi wa Habari (Cheti 4), Manunuzi na Ugavi (Diploma 3 na Cheti 2) na Mafunzo ya Zimamoto (Diploma 3).

Mhe. Spika, kikosi kimeendelea kutoa elimu ya tahadhari ya moto kwa jamii kwa kutoa vipindi 30 vya Redio na vipindi 10 vya televisheni kupitia ZBC. Aidha, vipeperushi 2,000 vimetolewa pamoja na kutoa elimu kwa Taasisi 40 za Serikali, 25 za binafsi, Vyuo 4 na Skuli 2.

Mhe. Spika, katika kukuza uhusiano kitaifa na kimataifa Kikosi kimeshiriki katika mikutano 3 iliyoandaliwa na Shirikisho la Afrika Mashariki, na kimeendelea na mazungumzo na wafadhili wa Kijerumani na Taasisi ya Zimamoto ya India juu ya kupatiwa msaada wa nafasi za masomo na mafunzo kwa wafanyakazi wa kikosi na baadhi ya vifaa kwa ajili ya kuboresha huduma zetu.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Kikosi kimelenga kutekeleza malengo yafuatayo:-

(i) Kutoa huduma za Zimamoto na Uokozi kwa haraka, tija na uweledi.
(ii) Kuboresha mazingira ya kazi, kuwajengea uwezo na maslahi kwa maofisa na wapiganaji
(iii) Kusogeza huduma za zimamoto na uokozi karibu zaidi na wananchi; na
(iv) Kukuza uhusiano kitaifa na kimataifa.

Mhe. Spika, ili Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kiweze kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2014/2015, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha TZS 3,787,500,000/= kwa kazi za kawaida.

Mhe. Spika, maelezo kamili yanapatikana katika kitabu cha hotuba yangu ukurasa namba 73 hadi ukurasa 77.

KIKOSI CHA VALANTIA ZANZIBAR (KVZ)

Mhe. Spika, Kikosi cha Valantia kimeanzishwa kwa Sheria Nam. 5 ya 2004 na kina majukumu ya kutoa ulinzi kwa kushirikiana na vikosi vya ulinzi na usalama vya SMT na SMZ, kusaidia kulinda raia na mali zao na kutekeleza shughuli za kijeshi kwa wakati wa dharura kwa ajili ya kulinda na kuweka usalama wa nchi.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Kikosi cha Valantia kilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:

(i) Kuimarisha nguvu za ulinzi na usalama;
(ii) Kuwaongezea uwezo wa kiutendaji wapiganaji wa kikosi cha Valantia;

(iii) Kuandaa mazingira mazuri ya utendaji kazi kwa wapiganaji wa Kikosi cha Valantia;
(iv) Kuendeleza ujenzi pamoja na kuyapatia hatimiliki maeneo ya Kikosi Unguja na Pemba; na
(v) Kuhakikisha wafanyakazi wanawajibika ipasavyo.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Kikosi cha Valantia kilitengewa jumla ya TZS. 3,258,000,000/= kwa matumizi ya kazi za kawaida na TZS. 70,000,000/= kwa matumizi ya kazi za Maendeleo. Hadi kufikia mwezi wa Machi 2014, Kikosi kimeingiziwa jumla ya TZS. 2,594,600,000/= sawa na asilimia 80 kwa matumizi ya kazi za kawaida na TZS 70,000,000/= sawa na asilimia 100 kwa matumizi ya kazi za maendeleo. Aidha, Kikosi kilipangiwa kukusanya TZS. 7,000,000/= na hadi kufikia mwezi Machi 2014, Kikosi kimeweza kukusanya TZS. 4,400,000/= sawa na asilimia 63.

Mhe. Spika, Kikosi cha Valantia kimeendelea kuimarisha nguvu za ulinzi na usalama kwa kuwapatia chakula cha kutosha askari wake katika muda wote wanapokuwa kazini katika kambi zake zote za Unguja na Pemba. Aidha, kikosi kimeendelea kusimamia masuala ya usafirishaji wa askari wakati wa kuwapeleka katika sehemu za ulinzi na utawala.

Mhe. Spika, Kikosi cha Valantia kimeendelea kuwaongezea uwezo wa kiutendaji Maofisa na wapiganaji wake tisa (9) kwa kuwapatia elimu katika ngazi na fani zifuatazo: Rasilimali watu (Diploma 1), Ununuzi na Ugavi (Diploma 3 na Cheti 1), Utibabu (Diploma 1), Utunzaji Kumbukumbu (Cheti 1) na Ufundi (Cheti 2). Aidha, kikosi kimeweza kuwaongezea uelewa wafanyakazi wake katika masuala ya UKIMWI.

Mhe. Spika, katika kuweka mazingira mazuri ya kufanyia kazi, Kikosi cha Valantia kimeweza kulipa gharama za upatikanaji wa hatimiliki kwa maeneo yake saba ambapo taratibu za upatikanaji wa hatimiliki zinaendelea. Kikosi kimeweza kuunganisha umeme katika kambi zake mbili za Kisakasaka kwa Unguja na Ndugukitu Pemba. Aidha, kikosi kimenunua kompyuta mbili na Vifaa vyake, samani za ofisini pamoja na magodoro 179.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 kikosi cha Valantia kimejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

(i) Kuhakikisha kuwa amani na utulivu kwa raia na mali zao unaimarika;
(ii) Kuendelea kuwajengea uwezo wa kiutendaji kwa kuwapatia elimu maofisa na wapiganaji wa kikosi ndani na nje ya kikosi;
(iii) Kuimarisha makaazi ya wapiganaji na maofisa wa kikosi na kusimamia upatikanaji wa hatimiliki za maeneo ya Ndugukitu na Pujini Pemba;
(iv) Kuboresha mazingira mazuri ya kufanyia kazi
(v) Kuhakikisha kuwa wafanyakazi wanawajibika ipasavyo;
(vi) Kuimarisha ulinzi na usalama wa raia na mali zao;

Mhe. Spika, ili Kikosi cha Valantia kiweze kutekeleza malengo yake kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya TZS 4,660,400,000/= kwa matumizi ya kazi za kawaida.

Mhe. Spika, maelezo kamili yanapatikana katika kitabu cha hotuba yangu ukurasa namba 78 hadi ukurasa namba 80.

SHUKURANI

Mhe. Spika, naomba kutumia fursa hii kutoa shukurani zangu za dhati, kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dk. Ali Mohamed Shein, kwa kuiunda upya Ofisi yake hii inayoshughulikia Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ na kunikabidhi mimi na wenzagu jukumu la kusimamia kazi zake. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nachukua fursa hii pia kuwashukuru Makamu wa Kwanza, Mhe. Seif Sharif Hamad na Makamu wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi, kwa miongonzo na ushauri wanaotupa mara kwa mara, ambao umesaidia sana kufanikisha majukumu yetu.

Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri na Wajumbe wote wa Baraza la Mapinduzi, Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza lako Tukufu.

Aidha, naomba pia kutoa shukurani kwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Mstahiki Meya wa Mji wa Zanzibar, Wenyeviti wa Mabaraza ya Miji na Halmashauri na Madiwani wote Unguja na Pemba, kwa mashirikiano mazuri wanayonipa.

Mhe. Spika, naomba kuwashukuru Wakuu wa Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambao ni; Mkuu wa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo - *Commodore* Hassan Mussa Mzee, Kamishna wa Zimamoto na Uokozi Zanzibar - Kamishna Ali Malimussy Abdalla, Mkuu wa Jeshi la Kujenga Uchumi - Kanali Soud Haji Khatibu, Kamishna wa Vyuo vya Mafunzo Zanzibar - Kamishna Khalifa Hassan Choum, Mkuu wa Kikosi cha Valantia Zanzibar - Luteni Kanali Mohamed Mwinjuma Kombo na Mwenyeketi wa Tume ya Utumishi Idara Maalum na Wajumbe wake, pamoja na watumishi wote wa Idara Maalum kwa mashirikiano yao wanayonipa na kazi nzito ya kusimamia ulinzi na usalama wa nchi yetu.

Aidha, nawashukuru kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kufanikisha sherehe za miaka 50 ya Mapinduzi matukufu wao na wapiganaji wote. Aidha, nawashukuru kwa kutuletea sifa kubwa katika michezo mbali mbali.

Mhe.Spika, natoa shukurani kwa vyombo vya Ulinzi vya Jamuhuri ya Muungano kwa mashirikianao wanayotupa katika ulinzi na usalama wa nchi yetu. Pia, wamesaidia sana katika kuendesha mafunzo kwa vyombo vyetu vya ulinzi na nawaomba wadumishe ushirikiano huo.

Mhe. Spika, shukrani zangu za dhati nazitoa kwa watendaji wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, hususan Katibu Mkuu - Ndugu Joseph Abdalla Meza, Naibu Katibu Mkuu - Ndugu Mwinyius Abdalla Hassan, *CDR*. Julius Nalimi Maziku, Mkurugenzi wa Usajili na Kadi za Utambulisho, Wakurugenzi wote, Maofisa Tawala wa Mikoa na Wilaya, Makatibu wa Miji na Halmashuri zote na watumishi wote kwa ushirikiano wa hali ya juu, wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu na kufikia malengo tuliyojipangia.

Mhe. Spika, naomba kumshukuru Katibu Mkuu wa Tume ya Mipango, Katibu Mkuu - Wizara ya Fedha, kuwashukuru Ofisi ya Mdhibiti na Mkagauzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na watendaji na watumishi wote wa SMZ na Taasisi zake.

Aidha, naomba kuishukuru Kamati ya Katiba Sheria na Utawala, ambayo iliijadili na kuitolea ushauri na michango katika rasimu ya hotuba ya bajeti, ambayo imetuwezesha kuwasilisha hotuba leo hii katika Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, naomba kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Tumbatu, kwa mashirikiano na moyo wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu katika Ofisi ya Uwaziri, pamoja na kazi za Jimbo langu la Tumbatu. Pia, naishukuru familia yangu kwa uvumilivu wao kutokana na muda mwingi ambao nalazimika kutumikia Taifa na kuwa mbali nao. Uvumilivu wao na mashirikiano wanayonipa yananiongezea nguvu na ujasiri wa kutekeleza majukumu yangu. Aidha, nawashukuru wananchi wote wa Zanzibar kwa umoja na mshikamano waliouonyesha katika ujenzi wa taifa letu na kudumisha amani ambayo inawezesha shughuli mbali mbali za kiuchumi kufanyika.

Mhe. Spika, mafanikio niliyoyaeleza katika hotuba hii, yamechangiwa na wengi na kwa namna mbali mbali. Kwa hivyo, nachukua nafasi hii kuzishukuru nchi marafiki zifuatazo: China, India, Uholanzi, Korea, Uingereza, Romania, Israel, Afrika Kusini, Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Benki ya Dunia, UNDP, ADB, ILO, na wengine wote waliochangia kufanikisha maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

HITIMISHO

Mhe. Spika, ofisi inasimamia mafungu saba ya bajeti, fungu 9 (Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ), fungu 17 (Jeshi la Kujenga Uchumi), fungu 18 (Chuo cha Mafunzo), fungu 29 (Kikosi Maalum Cha Kuzuia Magendo) fungu 32 (Kikosi cha Zimamoto na Uokozi), fungu 34 (Kikosi cha Valantia), fungu 37 (Mkoa wa Mjini Magharib), fungu 38 (Mkoa wa Kusini Unguja), fungu 39 (Mkoa wa Kaskazini Unguja), fungu 40 (Mkoa wa Kusini Pemba), fungu 41 (Mkoa wa Kaskazini Pemba) na fungu 43 (Ofisi ya Usajili na Kadi za Vitambulisho).

Mhe. Spika, kwa upande wa mapato, mafungu hayo kwa mwaka 2014/15 yanategemea kukusanya jumla ya TZS 121,330,000/= na kwa upande wa matumizi, mafungu hayo yanategemea kutumia jumla ya TZS 52,230,000,000/=, kati ya fedha hizo TZS 51,180,000,000/= kwa kazi za kawaida na TZS 1,050,000,000/= ni kwa kazi za Maendeleo.

Mhe. Spika, kati ya TZS 51,180,000,000/= kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za kawaida, jumla ya TZS 36,616,600,000/= ni kwa matumizi ya mishahara, na TZS 12,513,800,000/= kwa matumizi ya kazi nyenginezo yaani (*OC*) na TZS 2,050,000,000/= ni ruzuku ya Baraza la Manispaa na Mabaraza ya Miji ya Wete, Chake Chake na Mkoani.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

VIAMBATANISHO
MAPATO KWA MUJIBU WA MAFUNGU YA BAJETI (KIAMBATANISHO NAM. 1)

MAPATO YALIYOKUSANYWA KWA MAFUNGU YA WIZARA KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA JULAI 2013 -2014 NA MAKADIRIO KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

FUNGU	JINA LA TAASISI	MAKADIRIO KWA MWAKA 2013/14	MAKUSANYO KWA MIEZI TISA	ASILIMIA YALIYOKUSANYWA	MAKADIRIO KWA MWAKA 2014/15
17	**JKU**				
	MAUZO YA MPUNGA	5,500,000	3,000,000	55%	5,500,000
	MAUZO YA MTAMA	2,000,000	2,000,000	100%	2,000,000
	MAUZO YA MAZAO YA BUSTAN	2,500,000	5,000,000	200%	2,500,000
	MAPATO MENGINEYO	15,000,000	6,500,000	43%	15,000,000
		25,000,000	**16,500,000**	**66%**	**25,000,000**
18	**MAFUNZO**				
	KAZI ZA MIKONO	7,500,000	2,000,000	27%	7,500,000
	VIWANDA VYA MAFUNZO	4,500,000	2,000,000	44%	4,500,000
	MAPATO MASHAMBA	9,000,000	10,000,000	111%	9,000,000
	MIFUGO YA MAFUNZO	4,000,000	0	0%	4,000,000
	MAPATO MENGINEYO	16,000,000	5,000,000	31%	16,000,000
		41,000,000	**19,000,000**	**46%**	**41,000,000**
29	**KMKM**				
	MAPATO YA KAZI ZA UJENZI	15,830,000	6,000,000	38%	15,830,000
		15,830,000	**6,000,000**	**38%**	**15,830,000**
32	**ZIMAMOTO NA UOKOZI**				
	UKODISHAJI WA VIFAA	3,500,000	2,100,000	60%	3,500,000
	VIFAA VYA KUZIMIA MOTO	1,500,000	900,000	60%	1,500,000
	MATENGENEZO YA VIFAA VYA	2,500,000	1,500,000	60%	2,500,000
	MAPATO YA KAZI ZA UJENZI	1,500,000	900,000	60%	1,500,000
	UTOAJI WA VYETI	1,000,000	600,000	60%	1,000,000
		10,000,000	**6,000,000**	**60%**	**10,000,000**
34	**KVZ**				
	ADA YA ULINZI	7,000,000	4,400,000	63%	7,000,000
		7,000,000	**4,400,000**	**63%**	**7,000,000**
37	**MKOA WA MJINI MAGHARIBI**				
	VIBALI MBALI MBALI				20,000,000
					20,000,000
43	**AFISI YA USAJILI NA KADI ZA VITAMBULISHO**				
	ADA YA VITAMBULISHO VILIVYOPOTEA	1,500,000	8,789,000	586%	1,500,000
	ADA YA VITAMBULISHO KWA WAGENI - UNGUJA	15,000,000		0%	
		16,500,000	**8,789,000**	**53%**	**1,500,000**
	ADA YA VITAMBULISHO KWA WAGENI -PEMBA	1,000,000	1,000,000	100%	1,000,000
	ADA YA VITAMBULISHO KWA WAGENI - PEMBA	5,000,000		0%	
		6,000,000	**1,000,000**	**17%**	**1,000,000**
JUMLA		**121,330,000**	**61,689,000**	**51%**	**121,330,000**

MAPATO YA SERIKALI ZA MITAA (KIAMBATANISHO NAM. 2)

MAPATATO YA SERIKALI ZA MITAA ZANZIBAR KWA KIPINDI CHA MIEZI TISA (JULAI 2013 - MACHI 2014)					
S/N	**JINA LA TAASISI**	**MAKADIRIO YA MAKUSANYO 2013/14**	**MAKADIRIO KWA ROBO TATU**	**MAKUSANYO KWA ROBO TATU**	**ASILIMIA**
1	BARAZA LA MANISPAA	2,743,140,580	2,063,536,962	1,317,063,132	64%
2	HALMASHAURI YA WILAYA YA MAGHARIBI	800,000,000	559,698,520	537,475,000	96%
3	HALMASHAURI YA WILAYA YA KASKAZINI - A	177,500,000	141,468,125	139,075,144	98%
4	HALMASHAURI YA WILAYA YA KASKAZINI 'B'	281,000,000	214,404,500	220,766,000	103%
5	HALMASHAURI YA WILAYA YA KUSINI	129,886,000	97,414,500	91,278,000	94%
6	HALMASHAURI YA WILAYA YA KATI	200,000,000	150,000,000	136,518,750	91%
7	BARAZA LA MJI MKOANI	40,000,000	30,000,000	52,965,700	177%
8	BARAZA LA MJI CHAKE CHAKE	100,000,000	79,084,600	107,391,300	136%
9	HALMASHAURI YA WILAYA YA CHAKE CHAKE	48,728,000	36,546,000	47,711,510	131%
10	HALMASHAURI YA WILAYA YA MKOANI	51,265,000	38,448,750	74,869,822	195%
11	BARAZA LA MJI WETE	65,000,000	42,375,000	42,467,890	100%
12	HALMASHAURI YA WILAYA WETE	66,424,000	51,741,000	67,419,000	130%
13	HALMASHAURI YA WILAYA YA MICHEWENI	80,400,000	65,420,000	99,236,650	152%
JUMLA YA MAKUSANYO		**4,783,343,580**	**3,570,137,957**	**2,934,237,898**	**82%**

MATUMIZI YA SERIKALI ZA MITAA

MATUMIZI YA SERIKALI ZA MITAA ZANZIBAR KWA KIPINDI CHA JULAI - MACHI 2013/2014					
S/N	**JINA LA TAASISI**	**BAJETI KWA MWAKA 2013/14**	**MAKADIRIO KWA ROBO TATU**	**MATUMIZI HALISI KWA ROBO TATU**	**ASILIMIA**
23	BARAZA LA MANISPAA	2,743,140,580	2,063,536,962	1,938,375,913	65%
24	HALMASHAURI YA WILAYA YA MAGHARIBI	800,000,000	537,475,000	625,074,814	82%
25	HALMASHAURI YA WILAYA YA KASKAZINI - A	177,500,000	141,468,125	108,902,650	77%
26	HALMASHAURI YA WILAYA YA KASKAZINI 'B'	281,000,000	214,404,500	220,766,000	103%
27	HALMASHAURI YA WILAYA YA KUSINI	129,886,000	87,672,075	60,640,901	69%
28	HALMASHAURI YA WILAYA YA KATI	200,000,000	137,871,502	100,939,188	73%
29	BARAZA LA MJI MKOANI	40,000,000	68,721,600	52,985,242	77%
30	BARAZA LA MJI CHAKE CHAKE	100,000,000	79,084,600	100,080,000	127%
31	HALMASHAURI YA WILAYA YA CHAKE CHAKE	48,728,000	36,589,750	45,711,510	125%
32	HALMASHAURI YA WILAYA YA MKOANI	51,265,000	38,471,500	70,398,625	183%
33	BARAZA LA MJI WETE	65,000,000	42,375,000	42,467,890	100%
34	HALMASHAURI YA WILAYA WETE	66,424,000	51,741,000	57,809,251	112%
35	HALMASHAURI YA WILAYA YA MICHEWENI	80,400,000	65,420,000	99,236,650	152%
	JUMLA	**4,783,343,580**	**3,564,831,614**	**3,523,388,634**	**99%**

MATUMIZI KWA MUJIBU WA MAFUNGU YA BAJETI (KIAMBATANISHO NAM. 3)

MCHANGANUO WA MAKADIRIO NA MATUMIZI KWA KIPINDI CHA MIEZI TISA (JULAI 2013 - MACHI 2014) PAMOJA NA MAKADIRIO YA MWAKA WA FEDHA 2014 - 2015

FUNGU	JINA LA TAASISI	JUMLA YA MAKADIRIO KWA MWAKA 2013/14	MATUMIZI YA OC NA MSHAHARA HADI MARCH	ASILIMIA	JUMLA YA MAKADIRIO KWA MWAKA 2014/15	TOFAUTI
	IDARA YA MIPANGO SERA NA UTAFITI	118,083,000	34,277,625	29	337,472,000	219,389,000
	IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI	1,084,726,572	611,170,504	56	1,135,796,000	51,069,428
	URATIBU TAWALA ZA MIIKOA	1,905,866,937	1,200,629,990	63	1,895,443,000	-10,423,937
9	URATIBU WA IDARA MAALUM	141,828,775	18,314,775	13	78,128,000	-63,700,775
	TUME YA IDARA MAALUM	46,636,975	20,991,500	45	68,500,000	21,863,025
	OFISI KUU PEMBA	508,084,350	333,869,300	85	521,061,000	12,976,650
	JUMLA	**3,805,226,609**	**2,319,253,694**	**61**	**4,036,400,000**	**231,173,391**
	AFISI YA USAJILI NA KADI ZA VITAMBULISHO	2,055,000,000	873,000,000	42	1,939,000,000	-116,000,000
43	**JUMLA**	**2,055,000,000**	**873,000,000**	**42**	**1,939,000,000**	**-116,000,000**
17	JKU	7,457,000,000	6,655,855,655	89	9,482,600,000	2,025,600,000
18	MAFUNZO	6,099,000,000	5,106,200,000	84	7,491,300,000	1,392,300,000
29	KMKM	10,693,819,480	7,770,035,258	73	11,766,800,000	1,072,980,520
32	ZIMAMOTO NA UOKOZI	3,113,000,000	2,567,500,000	82	3,787,500,000	674,500,000
34	KVZ	3,258,000,000	2,594,600,000	80	4,660,400,000	1,402,400,000
	JUMLA	**30,620,819,480**	**24,694,190,913**	**81**	**37,188,600,000**	**6,567,780,520**
37	MKOA WA MJINI MAGHARIBI	1,608,175,000	875,560,856	54	1,757,800,000	149,625,000
38	MKOA WA KUSINI UNGUJA	1,147,000,000	728,558,872	64	1,336,600,000	189,600,000
39	MKOA WA KASKAZINI UNGUJA	1,247,000,000	924,300,000	74	1,362,700,000	115,700,000
40	MKOA WA KUSINI PEMBA	1,871,000,000	1,477,000,000	79	1,916,900,000	45,900,000
41	MKOA WA KASKAZINI PEMBA	1,557,030,000	1,003,351,365	64	1,642,000,000	84,970,000
	JUMLA	**7,430,205,000**	**5,008,771,093**	**67**	**8,016,000,000**	585,795,000
	JUMLA KUU YA BAJETI YA KAWAIDA	**43,911,251,089**	**32,895,215,700**	**75**	**51,180,000,000**	7,268,748,911
MIRADI YA MAENDELEO						
09	MRADI WA MAGEUZI YA SERIKALI ZA MITAA	150,000,000	47,310,000	**32**	200,000,000	50,000,000
34	UJENZI WA MAKAO MAKUU KVZ	70,000,000	70,000,000	**100**	0	-70,000,000
17	KILIMO CHA MBOGA MBOGA	250,000,000	-	**-**	150,000,000	-100,000,000
18	UJENZI WA KITUO KIPYA CHA CHUO CHA MAFUNZO HANYEGWAMCHANA	300,000,000	30,000,000	**10**	200,000,000	-100,000,000
29	UJENZI WA HOSPITAL YA KMKM AWAMU YA PILI				350,000,000	350,000,000
29	UJEZI WA CHELEZO CHA UOKOZI				150,000,000	150,000,000
JUMLA YA MIRADI YA MAENDELEO		**770,000,000**	**147,310,000**	**19**	**1,050,000,000**	**280,000,000**
JUMLA KUU YA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MAENDELEO		**44,681,251,089**	**32,942,525,700**	**74**	**52,230,000,000**	**7,548,748,911**

MAKADIRIO YA : OC (13,794,780, 895), MISHAHARA (28,055,470,194), RUZUKU (2,061,000,000) NA MIRADI YA MAENDELEO (770,000,000)

HALISI : OC(7,681,145,551), MISHAHARA (23,568,862,349), RUZUKU (1,545,207,800) NA MIRADI YA MAENDELEO (147,310,000)

(KIAMBATANISHO NAM. 4)

MIRADI YA WANANCHI ILIYOFANYIWA UFUATILIAJI

am.	Jina la Mradi	Shehia	Hatua iliyofikia	Gharama zilizotumika	Gharama zinazohitaj
	Ujenzi wa kituo cha afya	Bumbwisudi	Kimefikia hatua ya kuezekwa, kitakamilishwa na Wizara ya Afya	13,236,300/=	20,154,000/=
	Ujenzi wa madarasa manne, ofisi, ghala na vyoo. Skuli ya Kihinani	Kihinani	Vyumba viwili na ofisi ya Mwalimu Mkuu vimeezwkwa.	25,673,800/=	16,121,600/=
	Ujenzi wa skuli ya chekechea	Chumbuni	Kimetiw milango na sakafu	34,000,000/=	5,800,000/=
	Ujenzi wa Skuli ya Chunga	Fuoni Kibondeni	Umefikia hatua ya linta	8,838,500/-	35,000,000/=
	Ujenzi wa kituo kidogo cha Polisi	Pangawe	Umekamilika, bado kuwekewa umeme	5,343,400/-	1,820,000/=
	Ujenzi wa barabara	Pangawe	Njia imekarabatiwa upya	50,300,000/=	-
	Ujenzi wa skuli ya maandalizi	Bweleo	Milango na madirisha imewekwa.	12,000,000/=	146,000/-=
	Ujenzi wa kituo cha afya Mtoni	Mtoni	Hakuna mabadiliko tokea ulipokaguliwa mwaka uliopita.	23,004,000/=	51,000,000/=
	Ujenzi wa kituo cha afya Mwanyanya	Mwanyanya	Hakuna mabadiliko tokea ulipokaguliwa mwaka uliopita.	13,180,000	90,000,000/=
	Ujenzi wa Skuli ya Msingi Sharifumsa	Sharifumsa	Inasubiri kuezekwa na kumalizwa kupitia Wizara ya Elimu	9,500,000=	65,000,000/=
	Ujenzi wa ukumbi wa mitihani Mwera	Mwera	Hakuna mabadiliko tokea ulipokaguliwa mwaka uliopita.	6,862,500/=	35,495,500/=
	Ujenzi wa ukumbi wa mikutano wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Magharibi	Mwera	Umebakia marumaru na kupakwa rangi.	20,000,000/=	6,000,000/=
	Ujenzi wa madarasa 4 skuli ya Kitongani	Kitongani	Vyumba viwili madarasa vya yametiwa sakafu na plasta	5,564,500/=	15,887,000/=
	Ujenzi wa skuli ya maandalizi madarasa 4	Dole	Inasubiri kuezekwa na kumalizwa kupitia Wizara ya Elimu	7,962,000/=	16,318,000/=

(KIAMBATANISHO NAM. 5)

MIRADI INAYOENDELEZWA NA WANANCHI KATIKA MKOA WA KASKAZINI UNGUJA

Nam.	Jina la Mradi	Pahala Ulipo	Hatua Uliyofikia
1.	Ukarabati wa mabanda ya skuli ya msingi	Uvivini Tumbatu	Umekamilika
2.	Mradi wa maji kutoka Kipange hadi Tumbatu	Kipange hadi Tumbatu	Unaendelea
3.	Ujenzi wa vyoo vinne Skuli ya Msingi Tumbatu	Uvivini Tumbatu	Upo katika hatua ya kuezekwa
4.	Uzinduzi wa boti ya wananchi ya kusafirishia wagonjwa	Tumbatu	Umekamilika na boti inafanya kazi
5.	Ujenzi wa maktaba Skuli ya Jongowe	Jongowe	Upo katika hatua ya kuezekwa
6.	Mradi wa ujenzi wa Kituo cha Skuli ya Maandalizi	Jongowe	Upo katika hatua ya kuezekwa
7.	Ujenzi wa nyumba ya walimu	Upenja	Umo katika hatua ya mwisho ya kupaka rangi
8.	Ujenzi wa nyumba ya walimu	Kiwengwa	Umo katika hatua ya mwisho ya kupaka rangi
9	Ujenzi wa Hospitali	Kiongwe	Umekamilika
10.	Ujenzi wa Soko la samaki	Muwanda	Umefikia hatua ya kuezekwa
11.	Mradi wa maji	Kiweshangwe Mkwajuni	Unaendelea
12.	Mradi wa kilimo ASSP	Kibokwa	Unaendelea
13.	Ujenzi wa Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya Kaskazini ‘B’	Kinduni	Umefikia hatua ya kuwekwa milango, madirisha na sakafu.
14.	Mradi wa ujenzi wa mabanda ya skuli ya msingi	Kidagoni	Unaendelea
15.	Mradi wa ujenzi wa kituo cha Polisi Jamii	Upenja	Unaendelea
16.	Mradi wa ujenzi wa kituo cha Polisi Jamii	Matetema	Unaendelea
17.	Ujenzi na uwekaji kifusi njia	Kinyasini/Ngava	Unaendelea

(KIAMBATANISHO NAM. 6)

MIRADI ILIYOANZISHWA NA WANANCHI KWA KIPINDI CHA MWAKA 2013/2014 KATIKA MKOA WA KASKAZINI PEMBA.

.	Jina la Mradi	Mahala Ulipo (Shehia)	Hatua Uliyofikia
	Kituo cha Afya	Bwagamoyo	Kimeshafunguliwa na kinaendelea kutoa hudum
	Banda la Madarasa manne	Skuli ya Chwale	Kutiwa sakafu
	Ujenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Wete	Bahanasa	Kuezekwa
	Ujenzi wa chumba cha Maabara na Chumba cha kompyuta	Skuli ya Gando Sekondari	Kuezekwa.
	Ukarabati wa Kituo cha Mkono kwa Mkono	Hospitali ya Wete	Kimeshafunguliwa rasmi
	Ujenzi wa daraja	Mkia wa Ng'ombe Shehia ya Makangale.	Umekamilika.
	Mradi wa SACCOS ya wanawake	Micheweni	Umeshazinduliwa.
	Ujenzi wa Wodi ya wazazi	Kiuyu Mbuyuni	Umeshafunguliwa.
	Mradi wa Kiwanda cha sabuni Wanawake	Miti Ulaya	Kimeshafunguliwa.
	Mradi wa SACCOS ya wajasiri amali	Kizimbani	Imeshazinduliwa.
	Ujenzi wa Skuli ya Maandalizi Shengejuu.	Shengejuu.	Ujenzi wa linta.
	Njia Mpya ya Umeme	Ukunjwi	Imekamilika na kufunguliwa.
	Mradi wa Tangi la maji safi na salama	Bahanasa	Unaendelea.
	Ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa Skuli ya Karume	Shumba Mjini	Umeshafunguliwa.
	Ujenzi wa Skuli ya Sekondari ya Wilaya Wete.	Skuli ya Sekondari Pandani.	Umeshafunguliwa.
	Ujenzi wa Skuli ya Sekondari ya Wilaya ya Micheweni	Chwaka Tumbe	Umeshafunguliwa.
	Ujenzi wa Kituo cha Afya	Kifundi	Kimeshakamilika na kufunguliwa
	Kituo cha Mkono kwa Mkono	Hospitali ya Micheweni	Kimeshafunguliwa.
	Ujenzi wa Ukumbi wa mikutano	Micheweni kwa Shaame mata	Bado kuezekwa.
	Ujenzi wa kituo cha Afya Simai	Wingwi mapofu	Kozi ya nne.

Mhe. Ussi Jecha Simai: (Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii adhimu asubuhi hii ya kuwasilisha maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kunijaalia afya njema na uzima wa kuweza kusimama mbele ya Baraza lako tukufu katika kutekeleza majukumu ya kulijenga taifa letu. Aidha, kwa moyo wa dhati nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii muhimu ya kutoa maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka wa Fedha 2014/2015.

Mhe. Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri wa Wizara hii, Mhe. Haji Omar Kheri; Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Tumbatu, pamoja na watendaji wake wote kwa juhudi zake anazochukua na hatimaye katika muda mfupi tu tokea ateuliwe matunda matunda ya juhudi zake yameanza kuonekana.

Mhe. Spika, Kamati katika kipindi cha utekelezaji wa majukumu yake ilifanya kazi nzuri ya kuzipitia bajeti za Wizara husika na kutoa maelekezo yenye lengo la kuleta ufanisi wa majukumu ya kila siku; ambapo Wajumbe wote walitoa ushirikiano wa hali ya juu katika kutekeleza wajibu wao wa kuikosoa, kupendekeza na kurekebisha pale panapohitajika.

Mhe. Spika**,** naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati kwa umakini wao wakati wa kazi za Kamati. Shukurani hizo pekee hazitatosha iwapo sitowataja Wajumbe wa Kamati hii kwa majina yao, Basi naomba kuchukua nafasi hii kumkaribisha rasmi Mjumbe mpya wa Baraza la Wawakilishi wa Jimbo la Kiembesamaki ambaye ameletwa katika Kamati hii.

Mhe. Spika**,** Wajumbe wa Kamati hii naomba kuwataja kama ifuatavyo:

1. Mhe. Ussi Jecha Simai Mwenyekiti
2. Mhe. Abdalla Juma Abdalla Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Bikame Yussuf Hamad Mjumbe
4. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo Mjumbe
5. Mhe. Nassor Salim Ali Mjumbe
6. Mhe. Suleiman Hemed Khamis Mjumbe
7. Mhe. Wanu Hafidh Ameir Mjumbe
8. Ndg. Aziza Wazir Kheir Katibu
9. Ndg. Khamis Hamad Haji Katibu

Mhe. Spika**,** Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ ni miongoni mwa Wizara za Serikali ambazo zina majukumu mazito ya kutoa huduma kwa wananchi ambao wana mahitaji mengi ya msingi yanayohitaji kutekelezwa kwa ufanisi wa hali ya juu.

Mhe. Spika**,** Wananchi walio wengi kipato chao ni duni, na hivyo mahitaji yao mengi ya msingi wanategemea kuyapata kupitia huduma zinazotolewa na baadhi ya taasisi za Serikali ambazo zinahusika na utoaji wa huduma hizo ambapo watumishi wa Serikali wanapaswa kutumia utaalamu na ujuzi wao wote kwa lengo la kuisaidia Serikali kufikisha huduma hizo kwa wananchi.

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Spika**,** Pamoja na majukumu mengine ya msingi, kazi kubwa ya Idara hii katika mwaka huu wa fedha ni kuandaa na kuhakikisha kuwa mpango wa kupunguza umaskini unatekelezeka. Aidha Idara ina wajibu wa kusimamia utekelezaji wa sera na sheria mbali mbali zilizo chini ya Wizara hii kwa lengo la kuhakikisha kuwa wananchi wananufaika na huduma zinazotolewa na Serikali.

Mhe. Spika, Mpango wa kuendeleza miradi mikubwa na midogo midogo ya maendeleo katika ngazi za Serikali za mitaa ni mizuri, hata hivyo Kamati inaishauri Wizara kutekeleza mipango hiyo kwa kasi zaidi na kwa wale wananchi ambao wanakiuka amri halali za Serikali katika utekelezaji huo wachukuliwe hatua za kisheria.

Mhe. Spika, Malengo makubwa kwa mwaka ujao wa fedha ni kuanzisha na kuzindua kamati ya uratibu wa shughuli za mipango katika ofisi. Kamati inakubaliana na wazo hilo la kuanzisha kamati ambayo itakuwa na wajibu wa kuhakikisha kuwa shughuli zote za Wizara zinatekelezwa kama zilivyopangwa jambo ambalo litasaidia kuondoa baadhi ya kero zinazowakabili wananchi hivi sasa. Aidha Kamati inazidi kusisitiza kuwa Idara ina wajibu wa kuhakikisha kuwa inafuatilia utekelezaji wa kila robo mwaka wa Bajeti kwa upande wa Pemba ili malengo yaliyopangwa kwa kila mwaka yaweze kutekelezeka.

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Mhe. Spika, Idara hii ina jukumu kubwa la kuhakikisha kuwa Wizara inaimarisha mipango yake ya upatikanaji wa rasilmali watu ambao watakua na ujuzi wa kutosha; ambao wataisaidia Wizara kutekeleza mipango yake iliyojipangia kwa ufanisi mkubwa.

Aidha Idara ina wajibu wa kuhakikisha inatoa mafunzo ya muda mfupi yanayowajengea uwezo katika utekelezaji wa majukumu yao. Aidha, Kamati inaishauri Idara kuweka mazingira mazuri ya kiutawala ambayo yatasaidia kuwa na maelewano baina ya wafanyakazi.

IDARA YA URATIBU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

Mhe. Spika, Suala kubwa ambalo kamati inataka kusisitiza hapa ni ushirikiano baina ya viongozi wa Mikoa na Wilaya ambao ni kiungo kikubwa katika maeneo yetu. Aidha Kamati imekubaliana na mpango wa Wizara uliowekwa kwa mwaka ujao wa fedha wa kuandaa vikao baina ya viongozi hao. Vikao hivyo vitasaidia kujua changamoto zilizopo baina ya viongozi hao ambao ni chachu ya maendeleo katika Serikali zetu za Mitaa.

Mhe. Spika, kumekua na changamoto kubwa hivi sasa ya kuibuka kwa bandari bubu katika baadhi ya maeneo mbali mbali ya Mikoa yetu. Hivi sasa kumekuwa na tabia ya baadhi ya wananchi kuzitumia bandari hizo kwa kuwasafirisha wananchi kutoka sehemu moja kwenda nyengine kwa kutumia majahazi na boti ambazo hazijasajiliwa kupakia abiria kutoka Tanzania Bara na Zanzibar. Jambo hili limekuwa ni chanzo cha kusafirishia silaha na magendo mbali mbali wakiwemo wanyama kutoka Bara kuja hapa Zanzibar.

Hali hiyo pia inahatarisha usalama wa afya za wananchi wetu kutokana na hao wanyama wanaosafirishwa kutofanyiwa uchunguzi wa kina, hatimaye kuingiza maradhi mbali mbali hapa nchini. Hivyo Kamati inaitaka Serikali kupitia Wizara kuzifunga shughuli zote zisizoruhusiwa katika bandari hizo, Kamati inaona kufanya hivyo kutaepusha mambo mengi ya kihalifu ambayo yamekuwa yakijitokeza hivi sasa hapa nchini likiwemo tukio la hivi karibuni la kukamatwa kwa silaha iliyoingizwa katika bandari ya Mkokotoni Wilaya ya Kaskazini “A”.

Mhe. Spika**,** Baadhi ya vipaumbele na mipango ya utekelezaji tunayoipanga na kuamua katika chombo hiki haitekelezeki siyo kwa sababu ya ufinyu wa bajeti peke yake, bali mengine inakwamishwa kutokana na aidha utendaji kazi uliochini ya kiwango na kutojali kwa baadhi ya watumishi wa umma katika utekelezaji wa majukumu yao ya msingi na ukaidi wa baadhi ya wananchi ambao mara nyingi wanapopewa amri na Serikali hukataa kutii amri hizo.

Mhe. Spika, Uporomokaji huu wa maadili kwa baadhi ya watumishi wa Serikali umechangiwa sana na mifumo yetu mibovu ya uajiri huko nyuma na baadhi ya wananchi kutegemea viongozi wanaowajua ambao mara nyingi huwatetea Serikalini. Kamati inashauri Wizara kupitia bajeti ya mwaka huu kufanya kampeni maalumu na kuchukua hatua za lazima inapobidi kwa mujibu wa sheria, kuwashughulikia watumishi wa umma wasiozingatia maadili ya utumishi na wananchi wote wanaokataa kutii amri ya Serikali.

Mhe. Spika**,** Sera na Kanuni za Serikali za mitaa ndio miongozo inayotumika katika utekelezaji wa mipango yote inayopangwa katika Taasisi hizo, hivyo ni wajibu wa Idara kuhakikisha kuwa inatoa mafunzo maalumu kwa

wananchi na taasisi zinazohusika kuhusiana na sera na kanuni hizo, kwa lengo la kuhakikisha kuwa mipango inayopangwa kwa wananchi inatekelezwa bila ya kikwazo cha aina yoyote.

Aidha Kamati inachukua nafasi hii kuipongeza Wizara kwa taarifa iliyoipatia Kamati kuwa wanategemea kuleta Mswada wa dharura wa marekebishio ya Sheria za Serikali za mitaa ambazo ni Mswada wa Sheria ya Tawala za Mikoa, Mswada wa Sheria ya Serikali za Mitaa na Mswada wa kuanzisha Shirika la Ulinzi la JKU.

Kabla ya hapo kumekuwa na kilio cha muda mrefu ambacho Kamati kila Wilaya na Mkoa inaoupita inapewa malalamiko ya kuwepo kwa mgongano wa tafsiri za Kisheria ambazo zimekuwa ni kikwazo cha utekelezaji wa baadhi ya mipango ya Mikoa na Wilaya. Hivyo kuletwa kwa Miswada hiyo ya kisheria Kamati inaamini kuwa itaondosha migongano ya kisheria iliyopo

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

Mhe. Spika, Kamati yetu kabla ya kupitia bajeti ya Wizara na kuipitisha ilipata nafasi ya kufanya kazi zake za kawaida na ilipata nafasi ya kukagua baadhi ya Wilaya na Mikoa ya Kisiwa cha Unguja ukiwemo Mkoa na Wilaya ya Kusini Unguja, Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazinia “A”, Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini “B”, na Halmashauri ya Wilaya ya Kati.

Katika ziara hizo Kamati ilipata nafasi ya kupokea taarifa ya utekelezaji wa Bajeti na kuelezwa mambo mbali mbali zikiwemo changamoto ambazo nyingi kati ya hizo zinasababishwa na ufinyu wa bajeti. Kamati ilielezwa kuwa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja inakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa usafiri wa uhakika kwa wafanyakazi, hali hiyo inasababishwa na bajeti finyu inayopelekwa ambayo haikidhi haja na hatimaye wanashindwa kununua hata gari ya Ofisi.

Mhe. Spika, Kamati pia ilipata changamoto ya malipo madogo ya wazee wanayolipwa kupitia Mikoa yao kila mwisho wa mwezi. Kamati ilielezwa kuwa posho la wazee hao ni shilingi 5000 kwa mwezi wanayopatiwa ambayo Kamati inahisi kuwa kima hicho ni kidogo na inaishauri Serikali ifanye utaratibu wa kuwaongezea wazee hao wanaoishi katika mazingira magumu angalau fedha hizo ziwe shilingi 10,000 kwa mwezi na kadiri Serikali itakapopata uwezo iwaongeze wazee hao.

Mhe. Spika, Kamati pia ilipata taarifa katika kila Mkoa na Wilaya iliyokuwa inakaguliwa kuwa Sheria nyingi zilizopo hivi sasa za Serikali za Mitaa zimepitwa na wakati. Aidha sheria hizo hizo pia zinagongana na sheria za taasisi nyengine jambo ambalo limekuwa linazikosesha mapato Halmashauri zetu. Hivyo Kamati inapenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Wizara kwa uamuzi wake huo wa busara ambao utasaidia kuondoa changamoto zilizopo kama tulivyoeleza mwanzo katika hotuba hii.

Mhe. Spika, Kamati inazipongeza Wilaya na Mikoa yote katika jitihada zao za kuhakikisha kuwa suala la ulinzi na usalama linaimarika kwa pia inazidi kusisitiza kuwa ulinzi shirikishi ni suala la msingi ni vyema likazidi kuekewa mkazo kwa kuwashirikisha wananchi kila panapohitajika.

Mhe. Spika, katika ziara za Kamati ilipotembelea Baraza la Manispaa ilipatiwa changamoto mbali mbali zinazolikabili Baraza hilo ikiwemo changamoto ya uchache wa wafanyakazi jambo ambalo linapunguza kasi ya utendaji kazi hasa kazi ya uzoaji wa takataka. Aidha Katika suala zima la kuweka mazingira ya maeneo yetu katika hali ya usafi, Kamati ilisikitishwa sana na taarifa kuwa kuna baadhi ya wananchi wamekuwa na tabia ya kukaidi amri ya kuzihifadhi takataka katika maeneo ya kuwekea taka hizo. Hali hiyo imekua ikizorotesha juhudi zinazofanywa na Baraza hilo na kusababisha kuzagaa ovyo kwa taka hizo.

Kutokana na hali hiyo Kamati inaishauri Wizara na Serikali kwa ujumla kuweka utaratibu maalum wa kuizuia hali hiyo na ikiwezekana mtu yeyote atakayevunja amri ya kuzihifadhi taka zake atozwe faini au adhabu yoyote itakayofaa ichukuliwe dhidi yake. Kamati inaipongeza Serikali kwa uamuzi wake wa kuwaingiza wafanyakazi wa Baraza la Manispaa katika “*Vote*” ya mishahara ya Serikali jambo ambalo litasaidia fedha wanazozikusanya kutokana na vyanzo mbali mbali vya mapato kununulia vitendea kazi.

Aidha Kamati inapenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Serikali kwa mpango wake wa kutaka kuliendeleza eneo la Darajani kwa kujenga maduka ya kisasa ambayo yatakuwa ni chachu ya maendeleo katika nchi yetu.

AFISI YA USAJILI NA KADI ZA UTAMBULISHO

Mhe. Spika, Bado kuna umuhimu mkubwa wa Idara kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusiana na umuhimu wa Vitambulisho ambapo baadhi ya wananchi hadi hii leo hawana vitambulisho hivyo. Hali hii inatokana na uelewa mdogo wa baadhi ya wananchi ambao baadhi yao vitambulisho vyao hadi hii leo kwa taarifa za awali hawajaenda kuvichukua.

Aidha Kamati inapenda kuchukua nafasi hii kuwahamasisha wananchi wale ambao hawana vitambulisho kufuata taratibu na kwenda kuchukua vitambulisho ambavyo ni utambulisho wa Taifa. Aidha katika kikao cha kupitisha Bajeti Kamati ilipewa taarifa kuwa Idara haikukadiriwa mapato yake kutokana na mjadala uliokuwepo hivi sasa juu ya suala la ada ya vitambulisho vya wageni ambapo suala hilo hivi sasa kutokana na Kanuni zake kutokamilika, hivyo suala hilo litakaa sawa hapo mjadala wa Kanuni hizo utakapokamilika. Vile vile Idara inakusanya ada ya wanaopoteza vitambulisho ambapo Kamati ilipotaka maelezo juu ya suala hilo ilipewa taarifa hiyo na Kamati iliridhika.

IDARA MAALUM ZA SMZ

Mhe. Spika, Kamati yangu inapenda kuchukua nafasi hii kuzipongeza Idara Maalum zote za SMZ kwa juhudi wanazozichukua katika kutimiza wajibu wao pamoja na changamoto nyingi wanazokabiliana nazo. Aidha Kamati wakati inafanya ziara zake katika baadhi ya Idara hizo ilijionea changamoto ya ukosefu wa makaazi ya kudumu ya watumishi hao ambapo baadhi ya nyumba wanazoishi hazifai kwa makaazi ya binaadamu, kutokana na hali hiyo Kamati inaishauri Wizara kuliangalia suala hilo kwa umakini mkubwa kwa kuhakikisha kuwa makaazi ya watumishi hao yanajengwa ili waweze kutimiza wajibu wao kwa umakini zaidi.

Mhe. Spika, Suala la ubunifu kwa Idara Maalum ni suala la kupigiwa mfano kutokana na miradi mingi ya maendeleo inayobuniwa na Idara hizo ambapo mingi ya miradi hiyo endapo itatengewa bajeti za kutosha itaimarika na kuziimarisha Idara hizo kutokana na fedha zitakazopatikana katika miradi hiyo.

Mhe. Spika, Kamati ilipokuwa katika ziara zake za kikazi katika Kikosi cha Valantia, ilikagua kiwanda cha kutengenezea viatu ambacho kinatengeneza viatu hivyo kwa uimara wa hali ya juu pamoja na hali ngumu iliyopo kiwandani hapo. Hivyo Kamati inaiomba Wizara ifanye mpango wa kukiendeleza kiwanda hicho kwa kuhakikisha kuwa anaajiriwa mtaalamu mwenye uwezo wa hali ya juu kutokana na mtaalamu anayetumika hivi sasa kutoajiriwa na Idara hiyo na anafanya kazi ya kuwafundisha vijana waliopo pale kwa makubaliano maalum. Aidha Kamati inaishauri Wizara kuwatafuta wafadhili hata nje ya nchi kwa ajili ya kuwaendeleza vijana waliopo katika kiwanda hicho ili wakajifunze mbinu nyengine nzuri zaidi ambazo zitawezesha kukiendeleza kiwanda hicho.

Mhe. Spika, Kamati ilipata nafasi ya kukagua mradi wa ujenzi wa skuli ya ufundi ya JKU iliyopo Mtoni ambayo ujenzi wake umefikia hatua nzuri hadi hivi sasa. Kukamilika kwa mradi huo kutaisaidia jamii yetu kupunguza tatizo kubwa liliopo hivi sasa la ukosefu wa ajira kwa vijana wetu ambao wengi wao hawana ajira za kudumu, hata hivyo katika bajeti ya mwaka huu fedha za maendeleo katika Idara hii zilizotengwa ni kwa ajili ya kilimo cha mboga mboga. Pamoja na umuhimu wake kilimo hicho, suala la ujenzi wa skuli hiyo pia ni muhimu zaidi, hivyo Kamati inatoa ushauri kuwa Serikali ifanye juhudi zake zote kuhakikisha kuwa skuli hiyo inakamilishwa hasa tukizingatia kuwa ujenzi wa mnara wa miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar fedha zake zilipatikana japokuwa hazikuainishwa katika bajeti iliyopita.

Mhe. Spika, Chuo cha Mafunzo ni miongoni mwa Idara zinazokumbwa na changamoto kubwa ya kutoa huduma kwa wananchi hasa wale wanaowekwa katika magereza yetu, hivyo Kamati inaishauri Serikali inapopanga bajeti za kila Wizara ihakikishe kuwa inatoa kipaumbele kwa Idara hii kutokana na huduma za msingi zinazohitajika katika Idara hii ikiwemo ya malazi, makaazi na chakula. Kamati inazidi kusisitiza kuwa ujenzi wa gereza jipya la Hanyegwa Mchana ni wa lazima, na Serikali haina budi kuhakikisha kuwa inatafuta wafadhili watakaoweza kutusaidia kukamilisha ujenzi wake.

Mhe. Spika, Kamati yangu inapenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Idara ya Chuo cha Mafunzo kwa juhudi zake za kuanzisha mradi wa ujenzi wa maduka ambayo kukamilika kwake na mapato yake yataisaidia Idara hiyo kukwamua baadhi ya changamoto zilizopo.

Mhe. Spika, Wito wa Kamati yangu kwa Serikali katika mwaka huu wa fedha ni kuitaka ihakikishe inatekeleza malengo waliyojipangia; ikiwa ni pamoja na kukamilisha mapitio ya huduma za sheria ya Idara Maalum, Sheria Namba 6 ya 2007 na Kanuni zake. Aidha Kamati inasisitiza kuwa Idara Maalum zote ikiwemo Idara ya Zimamoto na Uokozi, Kikosi cha Kuzuia Magendo, ni muhimu sana katika ustawi wa taifa letu, hivyo Serikali ina wajibu wa kuwawekea mazingira mazuri ya kazi ili vijana wetu waweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Spika, Kamati yangu inaendelea kusisitiza suala la kuwalipa mishahara mizuri watendaji wa Idara Maalum zote kutokana na kazi nzito wanazozifanya na zinazolingana na wenzao wa Taasisi za Muungano ambao wanalipwa vizuri zaidi ukilinganisha na wao.
Aidha Kamati haijaridhishwa na hali hii ya watumishi wa Idara Maalum kulipwa kiwango kidogo cha mishahara na inapendekeza hatua za haraka zichukuliwe na Serikali kukaa tena na Uongozi wa Wizara kujadiliana tena viwango vipya vya Mishahara inayolingana na wenzao wa Bara.

TUME YA UTUMISHI YA IDARA MAALUM

Mhe. Spika, Tume hii ina jukumu kubwa la kuhakikisha kuwa Idara Maalum za SMZ zinafanya zoezi la uajiri pamoja na kuweka mazingira bora yatakayoimarisha mazingira ya Utumishi kwa watendaji wa Idara hizo.
Kamati yangu inazidi kuisisitiza Tume kusimamia zoezi zima la uajiri kwa haki ili kuepusha malalamiko yanayotolewa na baadhi ya wananchi kipindi cha uajiri kinapofika.

Kumekuwa na taarifa zisizoridhisha kinapofika kipindi cha uajiri ambapo kumekuwa na baadhi ya maafisa wasiokuwa waaminifu kuwalaghai wananchi kuwa watawapatia ajira kwa urahisi na kinachotakiwa ni wananchi hao kutoa fedha kwa ajili ya kuwafanyia mipango hiyo, malalamiko hayo yamekuwa ni mengi sana, hivyo Kamati inatoa agizo kwa Afisa yeyote atakayepatikana na kadhia ya kufanya kitendo hicho achukuliwe hatua kali za kisheria ili iwe fundisho kwa wengine wenye tabia kama hizo ambazo zimekuwa ni kikwazo na zinachafua jina la taasisi zetu.

Mhe. Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Wizara kupitia Tume ya Utumishi ya Idara Maalum za SMZ kwa uamuzi wake wa kuwafundisha wapiganaji pamoja na maofisa wake Sheria mbali mbali za nchi ikiwemo Sheria ya Utumishi wa Umma pamoja na masuala ya Utawala na Uongozi ili kuhakikisha kuwa wanatekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa.

HITIMISHO

Mhe. Spika, mwisho naomba nichukue fursa hii kukushukuru wewe pamoja na Wajumbe wako wote wa Baraza hili tukufu kwa kunisikiliza kwa utulivu na umakini mkubwa.

Mhe. Spika, naomba Wajumbe wako wachangie bajeti hii, watoe mapendekezo yao panapohitajika na hatimae kupitisha baada ya kuafikiana kwa hoja mbali mbali watakazoziibua wakati wa mjadala.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Mwenyekiti, tunakushukuru na sasa naomba nimkaribishe Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, wakati Mhe. Hamza Hassan Juma anajitayarisha na hatimaye Mhe. Ismail Jussa Ladhu.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, nikupe baraka zote leo na wewe kuniruhusu asubuhi hii leo ili kuweza kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Spika, mimi natoa ushauri wangu, natoa ushauri huo hasa kutokana na muamko wa kichwa changu kinavyonieleza. Mhe. Makamu wa Pili wa Rais naomba unisikilize vizuri ili uweze kumsaidia Mhe. Rais katika hilo wazo langu nililolitoa.

Mhe. Spika, katika bajeti iliyopita nilieleza kuwa kuwepo na Waziri Maalum wa Vikosi hivyo vya SMZ, lakini kwa bahati nzuri Mwenyezi Mungu kajaalia imepatikana hivyo, lakini haikupata nilivyotaka mimi ni *full* ili kuweza kuvisaidia vikosi vyetu. Sasa leo nina mawazo, mawazo yangu natoa wazo la muundo wa Wizara nyengine ni hiyo hiyo, lakini *moderlity* ambayo itasaidia naanza kuitamka. Wizara ya Katiba na Sheria na Tawala za Mikoa, kwa nini nikasema hivyo?

Mhe. Spika, kwa sababu hizi Halmashauri zetu Mikoa, Wilaya zinakosa sheria na ndio maana zinashindwa kufanya kazi zake tutazilaumu bure kwa sababu hazina sheria za utendaji hasa uhalisia, kwa sababu sheria hawana, hawana meno na utakuta mirundiko ya matatizo mengi sana inawafika kutokana na sheria hawana. Sasa nimeona nitoe mawazo hayo kwanza kabla sijaingia ndani.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, hayo ni mamlaka ya Rais kupanga Wizara, endelea.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Sijakusikia Mheshimiwa.

Mhe. Spika: Nasema namna ya kupanga Wizara na Idara hayo ni mamlaka ya Mhe. Rais.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, hii sipangi, *just* kutoa mawazo, si kama mimi ndio *president* mwenyewe aaa, haya ni mawazo kusaidia kwa sababu sisi kazi yetu kusaidia viongozi na Rais, mimi Rais ananijua kama Mwakilishi wake, sasa natoa kama hii *moderlity* ya kusaidia.

Mhe. Spika: Endelea na hoja iliyopo.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ehee!

Mhe. Spika: Endelea na hoja iliyopo.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Niendelee eee!

Mhe. Spika: Naam.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, sasa umenielewa vizuri. Sasa namuomba Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Idara Maalum SMZ, ndio maana tukasema kuwa kwa sababu kichwa kimoja hakijengi na ndio maana mafya lazima yawe matatu. Sasa haya mawazo ambayo ni mazuri Mhe. Rais akiyasikia pamoja na watendaji inaweza ikatoa muundo ambao wakati huo Mheshimiwa wangu Shein akaingia tena madarakani awe na *briefcase* ya aina hiyo, ili tuwasaidie vikosi vyetu tuvipe heshima, viwe na *special budget.*

Mhe. Spika, huu ni mzigo, kwa sababu tukiwapeleka katika maidara mengi, tukiwakusanyia tunaikuta bado hatujavitendea haki vikosi vyetu hatujavipa heshima.

Mhe. Spika, sasa ndio maana tunang'ang'ania mishahara ile ya kizamani, ndio maana tukasema kuwa wakiwa na *budget* yao "*Special budget"* ndio *target* yangu niliyokuwepo mimi, kwa sababu hawa wanafanya kazi ngumu sana tukitaka tusitake lazima tuseme, lazima tuisaidie serikali kuishauri kwa sababu hawa ni askari wana *techniques* zote za kiaskari, lakini kuna mambo mengine ya kimaslahi yanakuwa madogo. Sasa mimi ndio nimeomba kuwa wakiwa na fungu lao, itawasaidia wao na watajisikia na wao katika hali halisi.

Mhe. Spika, hata muundo wa vyeo vita-*change*. Leo unamkuta JKU ana mawe mawili yale pale hayazidi, hata ya tatu kwa sababu sheria haimpi, bado yuko pale pale, lakini akiwa na *special office* yenyewe tutaweza kubuni vyeo vya kuweza kum-*primote* yeye awe juu. Kwa kweli hii inasikitisha sana. Ninaomba sana hilo tulikubalishe kweli Mheshimiwa kwa sababu huu muundo ambao utakuwa ni mzuri sana kuwasaidia askari wetu kwa sababu kila siku wanalalamika.

Mhe. Spika, sasa hiyo inakuwea haijuzu. Mimi naomba sana na ninamshukuru sana mara hii Mhe. Dr. Shein alilisikia wazo hilo na akaweza kukifanya hiki kitu, lakini tunapokwenda kumshauri Mhe. Rais hatumuendei *deep, either* kumpa ile taaluma yenyewe hasa. Kwa sababu Rais si mtu mkaidi na sisi hatujui ile hoja ya kumjengea Rais

tukamueleza ndio matatizo yetu yanayotukuta. Sasa mimi naomba sana mnapokwenda kwa Rais hebu fanyeni *friends* nae mumzungumze uzuri tu, mkimzungumza uzuri tu, atakufahamuni, lakini mkenda kule unaanza kubabaika, nakwenda kwa Rais, wewe mwenyewe unaanza kubabaika utamueleza nini akusikie Rais Shein.

Mhe. Spika, sasa hilo ningeomba mimi tukenda kule tumpe hoja nzito tumfahamishe, hebu mimi anite siku moja kama sikumpa hoja nzito, nitamueleza vizuri tu, nini *idea* yangu na hiyo itakuwa *reference* kwenye *Hansard* hata nikifa watoto watarithi. Kwa sababu ni vitu ambavyo unajaribu kuvitoa kwenye kichwa chenyewe hiki alichoniumba Mwenyezi Mungu. Sasa mimi naomba kuna mambo mengine lazima tuisaidie serikali kwa kuleta muundo ambao unaokwenda na wakati.

Mhe. Spika, maana ya kusema hii Mikoa wende katika Wizara ya Sheria, niseme sijui nimuulize Mhe. Waziri kama utakuja kunambia, nataka mmoja tu unambie Mkuu wa Mkoa ambaye zamani niweze kusema nisimnyime haki yake Mhe. Abdalla Mwinyi niseme ukweli, kila *TV* nikitazama namuona kenda kutembea sehemu fulani, sijui kama na wengine wana *moderl* ya aina hiyo.

Mhe. Spika, kwa sababu wangekuwa wana mtindo wa kutembea ziara kwenye Shehia, sehemu nyengine na Wilaya zao haya matatizo yanayokuja yasingefika kuja mjini na hii yanakuja kwa sababu Mhe. Waziri, sheria ziko *weak*, sheria tangu za Said Khalifa mpaka leo hii, ndio maana zinawakwaza wanashindwa kuyatekeleza, lakini mimi ningeomba kuwa tuwe na mfumo mzuri, sasa hivi wa sheria kutokana na hiyo Serikali za Mitaa kama unavyosema kuwa bado hazijafika, tunazizungumza tu hivi, ndio kwanza tunataka tuletewe tuzipitishe sasa, sijui zikoje ndani ya muundo wake.

Mhe. Spika, sasa mimi ningeomba sana kuwa kuna matatizo ya wananchi wanaoanzia Wilaya, wanaanzia Mkoa, lakini *finishing* yake Mkoa hana, angekuwa Mkuu wa Mkoa ana *finishing* nyengine ya kisheria au kama anazo anazitia kwenye *briefcase,* itakuwa ni wao wenyewe tu. Sasa mimi ningeomba sana kuwa hawa Wakuu wa Mikoa wetu tuwajazie sheria au tuwafanyie *transfer* ya kuwapeleka katika chombo ambacho chenye sheria ili kiwawezeshe vizuri kwa mujibu wa sheria, ningeomba hivyo na huu muundo wa kutembea katika shehia zao, Wilaya zao, tunaomba sana wakimaliza *budget* tu, waanze ziara hizo kwa sababu zitapunguza ule msongomano wa matatizo ya wananchi, malalamiko ya wananchi.

Mhe. Spika, mimi naomba sana wawe na *special day* ya kuwasikiliza wananchi matatizo yao waliyokuwa nayo na waliokuwa hawana, basi tunaomba wawe na muundo huo waweze kufanya sifa, lakini kama hivyo wengine watajitokeza, maana yake Mhe. Waziri tusiwe na mizigo katika serikali tu iliyokuwa haisaidii serikali mizigo tu, isiyoweza kusaidia serikali, hicho kitu sasa tunakikataa. Tunataka mzigo ambao utakaosaidia serikali katika kutatua matizo ya wananchi, lakini sio tu kwa kuwa wewe Mkuu wa Mkoa.

Mhe. Spika, lakini niseme tena hapa Mhe. Mkuu wa Mkoa Mjini Magharibi, nakumbuka kipindi fulani alipokuwa Dr. Mwinyi nilitia hata bajeti kutaka kuzuia, kwa sababu gani? Tuliomba kijisehemu kidogo tu, cha kuwajengea wale askari wetu Polisi Jamii katika mtaa wa Kwahani pale kwa ndani, kijiofisi kidogo tu, leo tuna miaka mingapi? Nilikwenda na mtawala wake tukaangalia na wakati huo alikuwa Katibu wake yula wa zamani nikasema *Alhamdulillahi* mambo mazuri, kumbe tumepigwa changa la macho, mpaka leo hii kijisehemu kidogo tu, Polisi Jamii cha kujenga Ofisi maskini ya Mungu wanakwenda kukodi nyumba ya mtu, wanatupa pesa chungunzima, sikupata jibu.

Mhe. Spika, bajeti yako mimi siizuii, lakini nakwambia siungi mkono hii kwa sababu hiyo tu, kwa sababu wale Polisi Jamii wanatusaidia ulinzi mzuri wanaofanya katika maeneo yetu hasa Kwahani, Kwahani nani asiyeijua? Kwahani ni sehemu moja hatari sana, vibaka vingi walaunga wetu, lakini wale wamepunguza namba ile haiwi kubwa, sasa hivi imekuwa ndogo, basi na Ofisi tu, inashindikana kijisehemu kidogo tu, maskini ya Mungu kifulio cha zamani tangu enzi hizo za Said Khalifa mpaka leo hii, wala hatetemeki. Kwa hili mimi sikubaliani nalo Mhe. Waziri, nataka unipe jibu zuri ili nikupitishie bajeti yako. Si mkaidi mimi, lakini mkaidi kwa jamii siku hizi, nimejitolea kabisa kuwasaidia jamii. Ni kisehemu kidogo, naomba sana na uniridhie leo litoke jibu tena uje kutoa jibu hapa.

Mhe. Spika, nimshukuru sana Mhe. Haroun, *Wallahi* Mwenyezi Mungu amjaalie kila la heri, wafanyakazi jana wamefurahi sana kwa majibu yake mazuri ametoa majibu mazuri. Hivyo, ndio tunavyotaka sasa hivi mawaziri

mgeuke, mawaziri musiwe mizigo kwa jamii na wewe njoo leo, uniambie utizame watu kama hawatofurahi watafurahi tu. Wamefurahi jana wafanyakazi, nikwambie jana watu wote wamefurahi sana, wameona kama Zanzibar, sasa hivi tutapata nafasi zetu zilizokuwa ambazo kama ikilipwa *foreigner* na sisi tutalipwa fedha zile zile wameshukuru wanasema *Alhamdulillahi Rabil-alamin*, ndio tunavyotaka namna hivyo.

Mhe. Spika, sasa na wewe njoo hapa wape vijana, nafasi hiyo ukitaka twende *physical*, wewe kazi yako unajua wajibu wako twende zetu niko tayari, lakini wale wapewe nafasi ili waweze kujiendesha.

Mhe. Spika, niingie katika Mkoa wangu wa Kaskazini. Mkoa wa Kaskazini kwanza nitoe pongezi za dhati kabisa hasa katika kuanzia Mkoa na Wilaya zake na Halmashauri zake. Matatizo yapo sikatai, matatizo lazima yatakuwepo kwa sababu huwezi kununua buti, usiwe na soksi inawezekana hiyo. Matatizo yanakuwepo hayo hapa na pale, sasa ndio maana nikasema kuwa nimuombe sana Mheshimiwa wangu Mkuu wa Mkoa na Wilaya zake zote mbili zishuke kwa wananchi kutokana na matatizo ambayo kuna matatizo tumeyatatua ninashukuru sana *Alhamdulillahi Rabil alamina* kwa asilimia ndogo kwa mashirikiano ikitokezea tatizo Mhe. Mkuu wa Mkoa anatutwita wawakilishi.

Mhe. Spika, namuomba sana hili suala aendelee atwite vile vile ili tuweze kumaliza kero kwa sababu kuna kero nyengine, tunaweza tukazisuluhisha sisi wenyewe Mkuu wa Mkoa na Wawakilishi, tunaweza tukazitolea uamuzi kabla kufika kunako jungu kuu tena mtu akitaka kwenda kukubwa shauri yake mwenyewe, lakini Mkoa unakuwa umeshafanya na nini?

Mhe. Spika, lakini la pili, nimwambie kuwa usimamizi wa miradi yetu, naomba sana Mhe. Mkuu wa Mkoa aendelee hivyo hivyo kutoa taarifa za miradi yetu na Tume zake za kweda ku-*check* kwa sababu sasa hivi miradi inatiliwa fedha, lakini wale wananchi wanaona hii miradi sasa hivi inakwenda katika msingi mengine tu watu wanazila vibaya sana. Naomba na hilo Mheshimiwa ajiwekee heshima ya kuweza kutuma hiyo *task force* kwenda kuangalia miradi, sasa hivi inatafunwa vibaya sana, hilo kweli tulikubaliana nalo na tuliseme ndio kutokana na hali halisi ilivyo.

Mhe. Spika, Halmashauri ya Kaskazini 'B' ni sehemu ambayo ninayoiona usoni na machoni, niipongeze sana wamepiga lengo kubwa sana *time three*, sivyo vile ambavyo wameekewa na malengo ambayo yaliyokusudiwa maalum. Niwashukuru sana kutokana na utendaji wao, hiyo wamevuka katika hali halisi ilivyo sana na niwashukuru sana, sana.

Mhe. Spika, wamejitahidi Halmashauri yangu.

Mhe. Spika, mimi kawaida yangu ninakuwa sina mradi mwingi, lakini nina vitu vyangu maalum, sasa naingia kwenye vikosi.

Mhe. Spika: Unazo dakika tano.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, zinanitosha kwa hapa nilipo sasa hivi. Niende katika Kikosi cha Valantia. Mhe. Waziri hapa pana matatizo makubwa, naomba sana ikiwa hujenda na umekwenda nenda. Kwanza hata na ile *ratio* yao ya chakula inakuwa ni ndogo sana, wanapewa chakula kidogo sana cha kusikitisha kweli. Nenda kaangalie, lakini isitoshe, naomba sana hawa wakuuu wa vikosi hasa hebu jipendekezeni kwa hawa maaskari wenu, msifike mkajiona nyinyi kwa kuwa mna mameja, maluteni mkawanyanyasa hawa askari wa chini, haifi jamani tumuogope Mungu wananyanyasika kusema la ukweli wananung'unika, nenda kafanye hesabu wewe Valantia, pale kaseme nani wanamtaka kiongozi huyu *Wallahi* utapata mtu mmoja ndio wanaomtaka pale.

Mhe. Spika, wanasema ukweli maskini ya Mungu wanasema ukweli na sisi ndio lazima tuwasemee, *Wallahilaadhim* tunatembea vikosi vyote, mote tuna rafiki zetu wanatwambia ukweli kwa nini wasitwambie ukweli na sisi ndio watumishi wao.

Mhe. Spika, mimi naomba sana pale pana matatizo KVZ, hapajatulia nenda kaweke sawa, mimi ninakuamini jamadari na ndio maana ukapewa kikosi hiki. Nenda kaweke sawa uwe *serious*, usifanye mchezo hii ndio muokozi hii, ndio roho, si mchezo kaiweke vizuri. Ulianza ziara vizuri watu wanatuletea *message* wanakusifu sana, tangu kuzaliwa vikosi vile, wamesema Waziri aliofanya ziara ni peke yake huyo hapo Mheshimiwa, CCM sifichi walisema hivi hivi walimpongeza sana walimpa *"Hi"* maneno ya vijana. Mheshimiwa tunakushukuruni sana.

Mhe. Spika, sasa nakuomba sana, hebu vikamate vizuri, waambie hawa viongozi kuwa jamani ee, hawa hawakuleta utumwa, hawa wamekuja hapa leo kujitafutia ajira kama mlivyojitafutia nyie ajira. Halafu kuna vyeo wanapeana kwa siri, hawapeani dhahiri, wananyimwa vyeo wengine kutokana na utaratibu, maana yake huyu Kamanda wetu hapa ana vyeo zaidi ya vitatu. Mtawala na Mhasibu yeye, sijui kamtoa wapi, sijui KMKM wakati wahasibu wamo mle mle ndani waliosoma, lakini hawana nafasi hawakupewa kwa nini? Mimi naomba sana Mhe. Waziri nakuomba sana sana, mimi sitaki kuipiga buti hii, njoo unipe maneno matamu leo uone hapa nitaridhika kabisa.

Mhe. Spika, namalizia dakika zangu 2 zilizobakia. Nimshukuru sana Mhe. Mkurugenzi wa vitambulisho kipindi kilichopita nilisema sana na alitualika tukashirikiana naye, lakini kubwa zaidi nataka nimwambie simu zake ziko *open,* huyu mtu haringi, ukimpigia simu tuna matatizo, njoo unione kuna hili na hili aa, mtaalam wa mambo kitaaluma bwana, anakuvutia *screen* pale pale rrrrr, angalia vitu hivyo. Nimshukuru sana Mkurugenzi huyu na nimsifu nimpe haki yake kwa nini tusimpe haki yake yeye binaadamu kaumbwa, lililokuwa baya nitalisema, mimi simfichi, nimemwambia sina urafiki katika jambo kama hili. Ukinikera mimi wakati jambo unalo, mimi nitasema na nitakuwa wazi, sitosema uongo hata siku moja.

Mhe. Spika, nilichosemea hapa aliunda Tume na tukaitwa Waheshimiwa, njooni wamekuja kule kwangu wakanambia vitambulisho vyako hivi hapa watafutie wenyewe, mpaka leo vimeshindikana sijawapata wenyewe, ndio mashirikiano haya. Ukenda Ofisini kwake Mheshimiwa kaja, mpitisheni haraka sana, lakini Wakurugenzi wengine mizigo. Hakupokelei simu hafanyi chochote anaiona hivi hivi simu ya Mheshimiwa, hatutaki pesa, sisi tunakwambieni Wakurugenzi, lakini kuna tatizo ambalo tunataka kukwambieni *before* kabla ya kulileta hapa na wapo Mheshimiwa mizigo hiyo na nitakuletea keshokutwa nitawasema hapa, huyu mzigo wala sitomfumbia macho nitakwambia hasa.

Mhe. Spika, sasa naomba sana kuwa Wakurugenzi jamani chukueni sifa kama Mkurugenzi wa Vitambulisho kwa sababu anakubali mashirikiano na wewe, hapingi na hakudharau ila wanatudharau Wawakilishi wako, tunadharauliwa hapa, Makatibu wengine hawapokei simu na hata mawaziri wengine hawapokei, wamo humu sijui kwa nini wanaona tabu gani? Sasa mimi naomba sana jamaa mtuheshimu kwa utekelezaji, tunataka kukwambieni jambo mapema kabla kuja kukuvueni hapa, hilo ninalisema sana na nitaendelea kulisema sitoacha mizigo kukaa nayo pembezoni ikaniumiza hata siku moja.

Mhe. Spika, nakushukuru sana.Kwa hayo, machache, nimesema sitounga mkono mpaka nione suala langu hilo la Kwahani Polisi Jamii jinsi gani limefaidika na nione hali halisi ili tuanze ujenzi, tumepata wafadhili wa kutujengea, sasa tunashindwa. Kama limefanikiwa *well and good,* nitakusifu sina tatizo nalo.
Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, na mimi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwamtipura, nakushukuru kunipa nafasi hii nikaweza kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ.

Mhe.Spika, tumeweza kupata vitabu viwili ambavyo kimoja kina mchanganuo wa masuala yanayohusu hizi Serikali za Mitaa jinsi ya utekelezaji wake.

Mhe. Spika, mimi sitaki kumuiga Mhe. Makame Mshimba kwamba sitopiga buti, mimi buti nitapiga kwa sababu naanza jimboni kwangu. Katika Jimbo langu la Kwamtipura wananchi wangu wana kadhia kubwa sana na kadhia waliokuwa nayo ni suala zima la mtaro wa Darajabovu unaopita Kwamtipura, Shaurimoyo mpaka kumalizia Saateni.

Mhe. Spika, kitu ambacho ninachosikitisha sana, nimeshasema na uongozi sana kuhusu jimboni na kila likipiga wingu la mvua, basi mimi ninaanza kupata homa na katika vitabu viwili vya wizara hii na labda huruma ndogo inaweza ikatokea kwa Mhe. Waziri, kwa sababu hii wizara ndiyo kwanza amekabidhiwa hili jukumu linalohusiana na Baraza la Manispaa, lakini bado serikali inafanya kazi kwa pamoja.

Mhe. Spika, mradi wa *ZUSP*, nimeuzungumzia sana mradi ambao tuliurithi tangu awamu ya sita ambao mimi baada ya kuona vitabu vya Mhe. Waziri karibu vitatu vinazungumzia mradi ule na mimi nilikwenda kifua mbele jimboni. Hivyo, wananchi msiwe na wasi wasi safari hii mnaogelea, lakini mwakani hamtaogelea.

Mhe. Spika, mtaro ule unanitishia amani na kwa kweli imefika pahala, sasa hivi ninaona haya hata kwenda katika yale maeneo, Mhe. Sheha akinipigia simu nikiona ile mvua inanyesha, Sheha wa Shaurimoyo anaponipigia simu, basi kwa kweli naanza kujiuliza mara tatu, nitakwenda kusema nini na mwaka 2012/2013, nilipokwenda pale wananchi wanaelea na nyumba zao kutokana na maji ambayo yanayoingia katika majumba yao kupitia ule mtaro wa Darajabovu unaopitia Shaurimoyo.

Mhe. Spika, niliwaahidi na nikawaambia ndani ya bajeti ya mwaka huu tayari maelezo yamo mradi huu kuanzia mwezi June, basi mtaro huu utaanza kujengwa.

Mhe. Spika, imepita June ya mwaka 2013/2014 na sasa hivi imekuja June ya mwaka 2014/2015, nashindwa hata chakwenda kuwaambia.

Mhe. Spika, ingawa nilivyoangalia katika huu utekelezaji wa Serikali za Mitaa, nimeona ameshatafutwa mshauri mwelekezi, lakini mwaka uliopita, niliambiwa hatua iliyofikia nikuitisha *Tender*, leo tunaambia ndiyo kwanza mshauri mwelekezi.

Mhe. Spika, haya maneno mengi mazuri wananchi wetu wanavyoyasikia kule majimbo kwetu, ndiyo pale wanapotuona hawa Waheshimiwa wanakuja kujifurahisha tu, mtu sisi tunazama huku anakuja kutwambia *ZUSP*, *ZUSP* wao wananchi hata hiyo *ZUSP* hawaijui wao, wanajua mtaro ujengwe.

Mhe. Spika, mimi naomba sana na sijui watendaji wa wizara hii walipokuwa wanaandika hiki kitabu hasa katika huu mradi wa *ZUSP* ambao unaojenga mitaro imetajwa hapa Kwamtipura, Sebleni, kwa Bintiamrani, kwa nani sijui kama walijaribu kuangalia hotuba za bajeti vitabu vilivyopita.

Mhe. Spika, sisi tunavikusanya hivi vitabu siku hizi wala hatuvitupi, tunaangalia hotuba ya mwaka 2012 ilisemaje, 2012/2013 ilisemaje na 2013/2014 inasemaje, ingelikuwa alau yale maneno yanaendelea, lakini yanakwenda mbele yanarudi nyuma, yanakwenda mbele yanarudi nyuma. Namuomba sana Mhe. Waziri katika eneo ambalo wananchi wangu hawaridhiki kwa utendaji wa Baraza la Manispaa kupitia mradi wa *ZUSP*, ni katika eneo la ujenzi wa mtaro wa Kwamtipura na sasa hivi tunaingia mwaka wa homa, nazungumza mwaka wa homa wa uchaguzi.

Mhe. Spika, jambo kubwa unalokwenda kuulizwa, kama Akhera ikifika tu unajua hili nitaulizwa, je, ulitwambia mtaro huu keshokutwa unajengwa, sasa twambieni mengine. Unaanza aah, maana yake waziri, unakwenda ooh, maana yake *ZUSP, ZUSP*! Unaulizwa *ZUSP?* Hatutaki *ZUSP*, sisi hapa ulitwambia mtaro utajengwa tunataka mtaro uko wapi? Unaanza maana yake nisameheni nishakoma.

Mhe. Spika, sasa mimi nadhani Mhe. Waziri, najua unacheka kwa sababu Tumbatu kule hakuna maporomoko, lakini Kwamtipura yapo. Sasa nilikuwa naomba sana maelezo na pamoja na maelezo utakayonipa, lakini safari hii kwa bahati mbaya hii bajeti ndiyo tunaipitisha mvua za masika zimeshapita, lakini ningelikuchukua na kuna jamaa zako wengi sana wa Tumbatu kule, wapo wengi kule siku moja, nataka nikakutembeze ukaone namna gani tunavyozama wakati wa mvua za masika.

Mhe. Spika, nikiondoka na hapo. Kwa hiyo, buti yangu ya mwanzo itakuja hapa kwenye Baraza la Manispaa.

Mhe. Spika, jengine nilikuwa nataka nimalizie utendaji wa Baraza la Manispaa kwa kweli Baraza la Manispaa mnakwenda mbele mnarudi nyuma. Kuna kipindi mlianza kuzishughulikia bustani hapa, tukasema sasa hivi baada ya muda mchache tutakuwa kama Rwanda. Matokezeo yake mlizikamata kamata pale Michenzani kidogo, njia ya kwenda Bwawani na huku mmeishia hatuoni. Sasa mimi nilikuwa nataka niulize Baraza la Manispaa limeshindwa kutengeneza bustani za mji wetu.

Mhe. Spika, mji mpaka ukauita Manispaa, una vigezo vyake, leo mji wetu ni aibu, zile sehemu za bustani ndiyo zimekuwa maeneo ya kutia ile michanga barabarani, barabara ni chafu michanga tele. Mimi nadhani safari hii kuna *PBB programme* inayoangalia utendaji, yaani ile bajeti uliyoiomba ambayo unaangalia matokeo.

Mhe. Spika, sijui kama Baraza la Manispaa kuna *PBB*, *PBB* itabakia kwenye vitabu. lakini katika utekelezaji haionekani, barabara ni chafu, michanga, leo barabara nusu ni michanga na nusu ndiyo barabara. Sasa basi labda sasa hivi tukijenga barabara labda Baraza la Manispaa wanashindwa kufyagia. tujenge barabara nyembamba inayoweza kupita gari tu. watu wasiwe na pakupita. Kwa kweli imefika pahala tunataka mji wetu uwe safi, barabara angalau ziwe zinavutia na kupendeza.

Mhe. Spika, vile vile, taa za barabarani. Katika mji wa mwanzo uliokuwa hauna taa za barabarani, ni mji wetu wa Zanzibar, ukiacha hizi za usiku usiku, tunakusudia zile za *traffic stop light*. Tuliweka *traffic stop light* mbili, zile zimetushinda, jamani hapa Baraza la Manispaa kuna wataalamu kweli pale, kuna watu wa mipango, maana yake mipango siyo leo unaweka kitu halafu kinakufa, hatuna watu wa mipango pale.

Mhe. Spika, hebu tunataka watengeneze kitu kama kipindi hiki wenzetu wa China wanatoa safari nyingi kule wenzetu mkienda, basi Manispaa na ninajua Baraza la Manispaa kupitia Meya wana *Sister cities*, hizi za miji mbali mbali ya China, hata juzi tulipokwenda Marekani na Balozi tuliwaombea Mji wa California kuwa *Sister cities* na Zanzibar na alikuja Meya wa California, sijui kama waliweza kuonana nae, lakini tulifanya jitihada tukamualika na alikuja hapo. Basi angalau mnapokwenda katika mikutano yenu ya *Sister cities*, basi angalau ombeni kupatiwa hii misaada.

Mhe. Spika, sasa nadhani labda kwa sababu hii sheria ya Serikali za Mitaa imechelewa, naamini Mhe. Waziri anapokuja kutujibu, atakuja na maneno mazuri sana ambayo yatatupa moyo. Kwa sababu tutakaporekebisha sheria za mitaa, tutakapoleta sheria ya kuweka Serikali za Mitaa, sasa hivi hizi Halmashauri na Manispaa tutazipa nguvu za kuingia mikataba, wataweza kukopa na wataweza kukopesha angalau kuweza kuboresha huu mji wetu.

Mhe. Spika, kuna Kampuni nyingi hivi karibuni, wako vijana pale Arusha tulipokwenda ile safari yetu Arusha, pamoja kwamba ni safari ya michezo, lakini tunakwenda vile vile tunakutana na watu mbali mbali ambao wanaweza kuja kuboresha maisha ya nchi yetu. Ipo Kampuni pale wamesema sisi tunataka mtupe *Tender* yakutia zile taa za barabarani (*Stop light*) pamoja na *CCTV camera*.

Mhe. Spika, lakini kwa huu utaratibu waliokuwa nao sasa hivi Baraza la Manispaa, mradi huo hawauwezi kabisa, lakini tukishaweka hii sheria ya Serikali za Mitaa, haya maboresho naamini Mkurugenzi atakuwa na uwezo tena Makampuni wanasema wao wako tayari kujenga kwa njia ya *instolment* mnawapa *instolment* ya mwanzo wanakujengeeni, halafu mnawalipa ndani ya miaka sita mpaka saba. Mimi nafikiri utaratibu kama huo, ndiyo utaweza kusaidia kuboresha hizi Halmashauri zetu.

Mhe. Spika, ujenzi wa *slab* za taka. Kwa kweli katika Jimbo langu la Kwamtipura katika Shehia ya Mkele katika eneo ambalo Baraza la Manispaa wamekuja kujenga *slab* ya taka. Kwa kweli nasikitika sana kwamba hatukupata mashirikiano ya kutosha, kwa sababu eneo lile maarufu tunaita Mkele bondeni pale nyuma ya *Government Press*. Eneo lile nimeshaliomba kupitia Wizara ya Ardhi kwa ajili ya kujenga shule ya sekondari. Kama unavyojua watu wetu wa Ng'ambo tunajaribu kujitahidi kuwasogezea huduma pale karibu na eneo lile tayari kuna *becon* limeshapimwa, lakini kitu cha kusikitisha kumejengwa ile *slab* ya kutupia taka, lakini ubaya zaidi pale tuna skuli yetu ya chekechea, *slab* ya taka ipo hapo na skuli ya chekechea ipo hapo hapo.

Mhe. Spika, mimi nadhani eneo lile tatizo letu hatuna yale maeneo yakuweza kutupia taka, lakini eneo lile kwa kweli siyo busara kwa sababu kwanza pana watoto wetu wadogo wa *nursery school* pale na darasa la kwanza na mvua zinaponyesha kwamba pale panajaa maji mengi na ule uchafu unakuwa upo. Kwa hiyo, mimi naomba sana watafute eneo jengine la kujenga *slab*, pale watuachie kwa sababu tunakusudia kujenga skuli ya sekondari na ndiyo kama hivyo tunavyohangaika, tunaposafiri tunatafuta wahisani wengine, wameshatwambia tuwapelekee michoro, tumewapeleka. Sasa leo mtu uchampelekea mchoro, akija pale anaikuta *slab* ya taka, mimi nadhani kidogo itatupunguzia kasi ya maendeleo katika majimbo yetu.

Mhe. Spika, sasa haya kwa upande wa Baraza la Manispaa, niliona nijaribu kuwashauri hivyo.

Mhe. Spika, lakini jengine nilikuwa nataka nije nipate tu maelezo, sasa hivi tunashukuru mnafanya ukarabati na katika mpango wenu humu mmeonesha katika kitabu chenu hiki cha *programme* ya Serikali za Mitaa, lakini mmehamia pale karibu na majumba wa wazee barabara ya kwendea Amani mmechukua Ofisi pale. Sasa nilikuwa nataka maelezo tu ile Ofisi mmekodi au mmepewa na serikali na kama mmekodi mmetumia kiasi gani na je, taratibu zile za maamuzi ya Baraza la Manispaa yalitumika au mambo tu yalifanyika kienyejienyeji. Sasa hili kidogo nilikuwa nataka maelezo kwa sababu sisi tunaposikia maneno maneno kidogo ambayo ya hapa na pale ambayo tunahisi hayako vizuri sana, huwa tunataka taasisi zetu zisiingie katika mambo hayo ya ajabu ajabu.

Mhe. Spika, bado nipo katika Serikali za Mitaa, lakini nataka nije eneo la Paje. Nashukuru kwamba Mhe. Waziri baada ya kupata Ofisi hii, kuna hoja niliijenga pale na tuliwahi kupanga safari, mimi na Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi pamoja na Mhe. Waziri wa Ardhi, pamoja na Mheshimiwa anayeshughulikia Serikali za Mitaa, kwamba kuna huyu mwekezaji ambaye mara nyingi huwa namtaja ambaye amesema yeye serikali ameiweka mikononi mwake na kwa mujibu wa vitendo anavyovifanya, inaonesha kweli serikali ameiweka mikononi kwake ambapo Mwalimu Nyerere lugha kama hiyo ilimkera sana, alimfukuza mtu nchini kwa ajili ya kuzungumza lugha kama hiyo.

Mhe. Spika, sasa huyu mwekezaji kule Paje, yeye kwanza ukiacha lile eneo alilopimiwa akapata kibali cha *ZIPA*, ameshirikiana na watendaji, siyo waaminifu kwa kuiba ardhi nyengine ya wananchi na akaweka kuta na kuta lile akawazuia baadhi ya wazalendo kuweza kwenda katika maeneo yao na kwa bahati nzuri hata Mheshimiwa aliyekuwa Waziri anayeshughulikia Serikali za Mitaa Dkt. Mwinyihaji Makame alikwenda akaona na akatoa agizo na barua tuliikuta kwamba ule ukuta au lile geti livunjwe mara moja.

Mhe. Spika, kwa bahati nzuri tulikwenda kipindi kile na msaidizi wake ambaye alikuweko katika Serikali za Mitaa, namshukuru Mwenyezi Mungu katika wizara hii, sasa hivi amekuwa ni Naibu Katibu Mkuu na yeye alikwenda akatoa maelezo akatoa na barua na yule mwanasheria wa Halmashauri kama alivyosema Mhe. Makame Mshimba, mwanasheria wa Halmashauri ya Wilaya ya Kusini alitoa barua kwa mwekezaji yule avunje geti, lakini kama alivyosema yeye mwenyewe kwamba serikali ameiweka mikononi, mpaka leo kauli ya waziri haikufatwa, kauli ya Naibu Katibu Mkuu haikufatwa na kauli ya Mwanasheria wa Halmashuri pia haikufatwa. Jamani tuna wawekezaji wa aina kama hii amejenga geti kuwazuia wananchi wasiweze kufanya shughuli baharini, lakini vile vile amemzuia mzalendo eneo lake asiweze kulitumia.

Mhe. Spika, isitoshe amejenga mpaka katika hilo eneo la huyo mwananchi mzalendo, hii jeuri hii inatokea wapi? Mawaziri wetu mpo, sisi Wawakilishi tupo tumeshakwenda. Tulipokwenda siku ile walikuja wananchi wa kijiji pale kama ile *CD*, nakumbuka niliihifadhi sehemu nitajaribu kuitafuta, uione jinsi wananchi wanavyo-*shout* kuhusu yule mwekezaji kibri anachowafanyia.

Mhe. Spika, nilikuwa naomba sana ile amri aliyoitoa waziri mwenzako, hebu isimamie itekelezwe, leo eti amri imeshatoka kwa waziri, mwekezaji gani anashindwa kuondoa? Yaani ni aibu.

Mhe. Spika, tunawaomba mawaziri wetu muwafanyie kazi wananchi. Nishaona unataka kuniambia bado dakika tano, nishasikia nazimalizia dakika zangu tano.

Mhe. Spika: Na kwa kweli siyo tano ni dakika tatu tu.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mtume, Mhe. Spika, bwana umenifanyia sivyo!

Mhe. Spika, nataka nizungumzie suala la Tume ya Utumishi ya Idara Maalum. Mwenzangu Mhe. Makame Mshimba amezungumza vizuri, kwanza tulikuwa tujiulize kwa nini hizi Tume za Utumishi zikawekwa *separate* katika kipindi kilichopita, kosa tulilokuja kulifanya kuja kuiweka Kamisheni ikawa ndiyo mkubwa wa Tume zote, hapa tulikosea sana. Tume ya Utumishi ya Idara Maalum imefanya kazi kubwa na wamepeleka *scheme* yao humu imeelezwa katika kitabu tunaambiwa tayari imeshaanza kazi, lakini *scheme* hata kama imeanza kazi, ina maana ile imetambuliwa tu, lakini bado haijawa kwa sababu *scheme* inaendana na yale mambo yake mengine.

Mhe. Spika, hawa askari wetu tusiwaone wapole kiasi hicho, wanafanya kazi wanaumia na wanasikitika, wanasikitika *Scheme of service* ya Idara Maalum iheshimiwe kama ilivyopelekwa Tume ya Utumishi na mimi ndiyo maana jana nilikuwa mkaidi sana na sikukubali ile bajeti kwa sababu bado hizi Tume hazihishimiwi kama vile zilivyokuwa zimetakiwa. Kutokana na muda hilo naliacha hapo, lakini nitakuja kuliendeleza na Mhe. Waziri anayeshughulikia Utumishi wa Umma kuhakikisha maslahi ya askari wetu,

Mhe. Spika, kwa sababu ukiangalia kama jana Mhe. Waziri alisema serikali isubiri mpaka ile sera, sera hazilingani na miundo ya taasisi, muundo wa serikalini na muundo wa taasisi nyengine, sera zinakuwa tofauti. Sasa hizi Tume ambazo tayari zimeshakamilisha muundo wake, hizi tunataka serikali i-*take off* zile za serikali, kule inakuwa bado wasubiri ile sera yao ili waweze kuendelea nayo.

Mhe. Spika, sasa hili nilikuwa najaribu kulizungumza, lakini vile vile nilikuwa nataka Mhe. Waziri ile *paragraph* uliyoifuta ile. mimi *paragraph* sikutaka uifute, kwa sababu lile gereza la Hanyegwa Mchana Chuo cha Mafunzo kile kilikuwa ndiyo kielelezo cha utawala bora kwa Zanzibar, leo mradi mnaposema mnaufuta duh! Hapa kidogo naomba sana, sisi tunataka mradi ule wa Hanyegwa Mchana uchukuliwe na serikali usiwekwe katika Idara ya Mafunzo, hata katika ripoti ya Wenyeviti Bajeti ya Serikali tuliishauri serikali iuchukue ule mradi na utafutiwe ufadhili, tena usijengwe tofali moja moja kama inavyofanywa sasa hivi, ule ujenzi mkubwa.

Mhe. Spika, sasa haya mengine nitajaribu kumuandikia kwa maandishi ili aone ni namna gani nimejaribu kumsaidia katika kuiboresha hii wizara yake, kwa sababu haya tunayoyasema akiyatekeleza tutakuwa tumemsaidia kuiboresha wizara yake. Nimebakisha mambo mengi, lakini nitajaribu kumuandikia kwa maandishi na nitaomba yale nitakayomuandikia kwa maandishi yakubaliwe vile vile kwenye *Hansard*.

Mhe. Spika, baada ya hayo, baada ya kusikiliza maneno ya Mhe. Waziri, sio maneno tu na utekelezaji utakuwa vipi, inawezekana pengine baadae nikaja nikaunga mkono.

Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu (*S.W*) kwa kutujaalia siku ya leo Ijumaa kuamka tukiwa hai na wazima kuendelea na shughuli zetu.

Mhe. Spika, nikushukuru na wewe kwa kunipa nafasi hii na mimi vile vile kuweza kutoa mchango wangu katika bajeti hii ya Wizara ya Nchi (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ. Nimpongeze Mhe. Waziri, kwa uwasilishaji wake mzuri wa hotuba hii.

Mhe. Spika, mimi nianze kwa masikitiko na nasema haya kwa unyonge sana kwa sababu katika watu ambao ni marafiki wa karibu sana na Mhe. Waziri, mmoja ni mimi na alipoteuliwa kuongoza wizara hii nilikuwa na matumaini makubwa sana, kwa sababu sitaki kuficha, tulichoka na ahadi hewa za waziri aliyemtangulia katika wizara hii. Kawaida yangu mimi huwa sitafuni maneno, nasema; "pauro nitaliita pauro".

Mhe. Spika, kama nilivyosema tulitegemea tutakuwa na mabadiliko makubwa sana, lakini bado hali ya utendaji katika maeneo yanayosimamiwa na wizara hii, kuna malalamiko mengi tena, ni yale yale ambayo bado hayajashughulikiwa.

Mhe. Spika, naomba nianze kwa Idara Maalum za SMZ. Mwaka jana nilisema na mwaka huu ninasema kwamba katika nchi yoyote vikosi vya ulinzi na usalama huwa ni kielelezo cha uzalendo na ni fahari kwa raia wa nchi hii na katika nchi yoyote raia akimuona askari, basi anaona kwamba kile ni kielelezo cha fahari ya nchi yake. Kwa hivyo, ni lazima tuwatunze na tuwaheshimu na tuoneshe kuthamini kazi wanayoifanya.

Mhe. Spika, tuliorodhesha mambo mengi sana katika bajeti ya mwaka uliopita, lakini nasikitika kusema bado hali iko vile vile na naomba nianze na hili ambalo wenzangu wamelitangulia kulisema.

Mhe. Spika, kwa kazi waliyoifanya hawa tulitegemea kuwa maslahi yao yawe yanatizamwa vizuri, kwa sababu sisi raia tunapolala tunalala kwa utulivu tukiamini kwamba kuna vikosi vinatulinda, lakini inasikitisha kwamba wengi wetu au wengi kati yao katika Idara Maalum bado maslahi yao ni duni.

Mhe. Spika, kwa taarifa tunazopewa wengi wao kile ambacho wanachukua nyumbani, bado kiko chini ya shilingi 200,000 kwa mwezi. Katika hali hii ya maisha tuliyonayo unategemewa uishi vizuri, ule vizuri na familia yako, usomeshe watoto wako, ukiumwa ujitibu na mahitaji mengine kadhaa wa kadhaa. Hivi mapato au mshahara ambao ni chini ya shilingi 200,000 unamuwezeshaje? Sisi mpiganaji wetu wa Idara Maalum za SMZ aweze kujikimu.

Mhe. Spika, mimi nadhani imefika wakati serikali ifanye maamuzi, kuendelea kuajiri wengine kila mwaka, lakini hawa tulionao bado maslahi yako duni, sidhani kama ni uamuzi sahihi, mimi nadhani imefika pahala turudi kwanza tuangalie maslahi yao hawa na imesemwa hapa na wenyewe wanatwambia, kwamba muundo wao wa utumishi tumeambiwa uko tayari, lakini unabakia uko tayari kwa maneno tu, bado utekelezaji wake hauonekani kuna malalamiko mengi sana.

Mhe. Spika, lakini vile vile nyumba zao wanazoishi ukienda ukiziangalia, tulipata nafasi nilipokuwa katika Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na mpaka leo hali iko vile vile, ukienda ukiangalia nyumba wanazoishi askari wetu zinahudhunisha, mtu anapewa uhamisho pengine kutoka Unguja kwenda Pemba, anapewa kijichumba kimoja kiko taabani chenyewe dongo tupu ndani, anatakiwa akae yeye na familia yake (mkewe na watoto wake), hata zile haki nyengine za kifamilia akizihitaji hawezi kuzipata kutokana na hali ile anayoishi. Nyumba ziko taabani, zinavuja hali ngumu sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hata maeneo ya kufanyia kazi na mimi sisemi katika makambi makubwa, mtu akitaka kuona mfano hai aangalie Kikosi cha Zimamoto, aende pale *Airport* ya Pemba, Chake Chake akaangalie yale mazingira, miaka mitatu mfululizo tunakwenda na tunatoa maelezo ukirudi hali iko vile vile, hata yale magorodo ya kulalia, lakini kuna maslahi yao mengine, kuna posho zao za uhamisho, bado malalamiko ya fedha unajua, kwa sababu mara hii muda umepunguzwa, lakini bado malalamiko yao yako pale pale.

Mhe. Spika, mimi nasema Mhe. Waziri, kapongeza katika hotuba yake kwamba wanainua michezo, lakini mimi nina wasiwasi hata hivi tunavyoshuhudia kwamba sasa kiwango cha michezo cha timu za vikosi vyetu kinashuka, ni kwa sababu mahitaji yao hayatoshelezi, ikiwa ya msingi hayawezi kutimizwa, sidhani kama watawaeza kushughulikia masuala ya michezo. Kwa hivyo, nasema tuna haja ya kuona kwamba huduma na maslahi yao yanaimarishwa ili yalingane na kazi ngumu ambayo wanaifanya ya kutulinda sisi, wakati sisi tukiwa tunaendelea na shughuli zetu.

Mhe. Spika, jengine katika vikosi vyote, basi vyote ni muhimu, lakini kuna kikosi kwa mfano cha KMKM ambacho hiki kwa Zanzibar kina umuhimu wake, kwa sababu sisi ni visiwa, hata zikitokea zile ajali tunategemea hiki kitusaidie, ajali za baharini, lakini sijui Mhe. Waziri anaweza kutwambia kwamba, ukiondoa aliyotutajia katika hotuba yake kwamba kuna boti mbili zimefanyiwa matengenezo na Kampuni fulani ya Uholanzi, tumefanya utaratibu gani kuwapatia boti mpya za kisasa kuja kufanya kazi zao za kulinda usalama wetu, lakini pia, kukitokezea mikosi ya ajali baharini waweze kutusaidia, kama hatuwezi kuwapa vifaa hivi tutakuwa tuna vikosi vinakwenda vikirudi, lakini vile vifaa muhimu vya kufanyia kazi havifanyi kazi.

Mhe. Spika, hata nikiangalia hotuba hii, naangalia ukurasa wa 63, kwa mfano natoa mmoja tu, na-*quote* katika Kikosi cha KMKM wanasema, "Kikosi kimeweza kuwapatia sare mbali mbali maofisa na askari wake zikiwemo *combat* jozi 150, viatu vya buti jozi 200, sare za sherehe za Miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar na fulana za fatiki jozi 3000". Fulana sio vifaa vya kazi hizi, ni kwa ajili ya shughuli maalum za sherehe, hivi vifaa vyao vya kazi kusema kwamba *combat* jozi 150 na buti josi 200, ndio tunasema kweli tunaweza kuhudumia vikosi vyetu?

Mhe. Spika, mimi najiuliza tatizo liko wapi? Kwa sababu ukitizama bajeti mtiririko wa kuingiziwa fedha wizara hii ni mtiririko mzuri kuliko wizara nyengine, nilikuwa naiangalia hapa kama nilalamike kama nilivyoilalamikia Wizara ya Nchi (OR), Kazi na Utumishi wa Umma, lakini hapa uingizaji wa fedha si mbaya. Sasa najiuliza kama fedha zimeingizwa kwa nini huduma kwa askari hawa haziwafikii, fedha hizi zinakwenda wapi? Naomba maelezo kutoka kwa Mhe. Waziri.

Mhe. Sika, hapo hapo nimalizie katika hili la idara kwa kuzungumzia lile alilolizungumza Mhe. Hamza Hassan Juma, mimi namuunga mkono. Mimi nimesikitika kumsikia Mhe. Waziri katwambia tufute katika malengo ya Chuo cha Mafunzo ujenzi wa Chuo cha Mafunzo kipya katika eneo la Hanyegwa Mchana.

Mhe. Spika, mimi na wenzangu nilipata nafasi nilipokuwa katika Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwenda kutembelea, eneo hili linahuzunisha kuwa linafutwa kwa sababu Mhe. Rais keshalitolea kauli hili na zikaoneshwa katika vyombo vya habari na akenda akakaguzwa kuwa huu ni mmoja katika miradi ambayo inataka kuonesha kwamba jinsi gani tunaimarisha huduma za Vyuo vya Mafunzo.

Mhe. Spika, sasa mimi nasema viongizi wetu hawa Waheshimiwa Mawaziri na watendaji wao kama jambo hawajakuwa na uhakika nalo wasiwachukue viongozi wetu wa Kitaifa wakawafanya kwenda kutoa kauli. Kwa sababu baadae inaonekana kama vile tunamdhalilisha Mhe. Rais mbele ya macho ya wananchi akitoa kauli, halafu jambo likawa halipo, leo tunalitangaza hapa katika chombo cha wananchi Baraza la Wawakilishi kwamba tunauondosha mradi ule, maana yake tumemdanganya Mhe. Rais na yeye akenda akatoa kauli ambayo kwa wananchi inaonekana kwamba hajui anachokifanya, si picha nzuri tunayoitoa.*(Makofi)*

Mhe. Spika, eneo jengine ambalo naomba nilizungumzie ni eneo hili la Mamlaka za Serikali za Mitaa, kwanza kabla sijaingia katika maelezo niliyokusudia kuyasema, nilikuwa namuomba Mhe. Waziri akija aje anipe maelezo katika mgao wa fedha za mikoa, mikoa mingi imevuka asilimia 70, Mkoa wa Kaskazini Unguja, Mkoa wa Kusini Unguja, Mkoa wa Kusini Pemba na Mkoa wa Kaskazini Pemba iko kwenye asilimia kama nakumbuka 64, lakini Mkoa wa Mjini Magharibi una asilimia 54, kilichoingizwa katika bajeti yake kulinganisha na makisio.

Mhe. Spika, sasa Mkoa wa Mjini Magharibi ndio wenye Makao Makuu ya nchi, ndio unaotoa huduma, hata katika wananchi wa maeneo mengine wanapokuja hapa kufuata huduma, lakini mkoa huu tunaambiwa una asilimia 46 ya wananchi wetu wa Zanzibar wanaoishi katika Mkoa wa Mjini Magharibi, tuna watu 593,678, lakini huu ndio umepewa bajeti ndogo kuliko yote. Naomba maelezo katika hili.

Mhe. Spika, kwa sababu ya muda, niende moja kwa moja katika eneo ambalo linanihusu Baraza la Manispaa. Pale mwanzo nilisema kwamba nimesikitika kuwa bado utendaji hatuoni mabadiliko. Mhe Hamza Hassan Juma kazungumza Mradi wa *ZUSP*, eneo jengine ambalo tunamfanya Rais wetu adhalilike mbele ya wananchi ni Mradi huu wa *ZUSP*. Niwakumbushe Wawakilishi wenzangu Mradi wa *ZUSP* ulipigiwa chapuo kubwa katika bajeti ya mwanzo ya Serikali ya Awamu ya Saba mwaka 2011/2012, wananchi wakajenga matumaini makubwa na Mhe. Rais akaubeba katika ziara yake ya mwanzo ya Mikoa, akawa anautangaza kila pahala ikafanyiwa tangazo maalum katika Televisheni ya Zanzibar. Wananchi wana kumbukumbu zile, akasema mji wetu utang'ara, utakuwa safi, aka! Kauli zile za Mhe. Rais zipo katika vichwa vya watu, leo inakata mwaka wa nne, Serikali ya Awamu ya Saba hakuna kitu kuna maneno *ZUSP*, *ZUSP* wananchi wanakula maneno ya *ZUSP*, hawaoni tija ya mradi huu.

Mhe. Spika, nimeangalia hiki kitabu cha pili tulichopewa mambo yote yamekamilika, ununuzi wa gari za Wakurugenzi wa Manispaa umekamilika, ununuzi wa vespa umekamilika, mahitaji yao yamekamilika, lakini kule kwenye huduma hasa za kwenda kwa wananchi kote kuna maneno tu, huwezi kuambiwa kwamba lengo la mwaka jana lilikuwa ni kuweka taa kwa sababu tumepata Mshauri Mwelekezi mwaka ujao, ndio kutaanza kuwekwa taa. Sasa hili lengo la mwaka jana limeishia wapi? Maana yake halikutimizwa.

Mhe. Spika, leo wananchi wengi wanadhani kwamba zile taa zilizotiwa katika barabra za Michenzani labda ni Mradi wa *ZUSP*, lakini tunaona pale kuna vibango vya *China Aid*, *ZUSP* ni mradi ambao umetolewa fedha na Benki ya Dunia mkopo, ule ni msaada wa Watu wa China, zile taa tulizoahidiwa za barabarani kupitia Mradi wa *ZUSP* ziko wapi? Na kwa nini taa zile ziishie huku kwetu sisi tu maeneo ya mjini? Maeneo ya ng'ambo kwani yamekosa nini? Tunapozungumzia kuongezeka kwa uhalifu moja ni kwamba kunapokuwa na kiza maana yake unakaribisha uhalifu, hatulioni?

Mhe. Spika, uzoaji wa taka bado tatizo kubwa sana. Kipindi kama hiki cha mvua kilichomalizika, lakini bado zinaendelea endelea, unakuta mataka yamerundikana na yanatoa uvundo, hayazolewi. Mimi pale ninapoishi mpaka najiuliza hii *style* mpya chini ya uongozi mpya wa Baraza la Manispaa na wizara kwamba ma-*tank* ya kuzolea taka sasa yanabiruzwa? Kwa sababu wanancni waliniuliza pale, kwamba hizi taka tutie wapi? Ninazo picha, hupiga picha katika simu yangu hii, mataka yamefurika mpaka nje.

Mhe. Spika, kuna eneo, kwa mfano katika Mji Mkongwe kuna Hoteli za Kitalii tunazotegemea zituingizie mapato, nje ya hoteli kwa mfano ile ya Ng'ome Kongwe pale kuna Hoteli ya Marumaru zile taka zinafurika mpaka zinamwagika nje, hakuna chochote, si Mji Mkongwe, si ng'ambo, kote sawa sawa.

Mhe. Spika, pia, pamezungumzwa mitaro ya maji ya machafu, makaro yote kila unapopita harufu, uvundo unapasuka, lakini ukija *ZUSP* unaona huduma zao wamejipatia wao katika masuala ya kuwahudumia wananchi hakuna kitu. Bustani zimezungumzwa pia, mpaka mimi napata wasiwasi, tunaposema kama hii inakuwa ni miradi ya watu fulani inathibitika wazi, maana yake bustani zimeweza kutengenezwa alipokuwepo mkubwa fulani na tulileta malalamiko yake katika ripoti ilichukuliwa na Baraza la Manispaa hapa, alipoondoka yeye imesita. Inaonekana kwamba ule mradi ulikuwa sio wa taasisi, ulikuwa wa mtu fulani, akiondoka kaondoka nao, ndio maana yake kwamba hatufanyi kazi kwa mipangilio.

Mhe. Spika, jengine ninalotaka kuzungumzia hapa ni suala zima la uamuzi wa serikali wa kuhamisha Kituo cha Daladala Darajani. Mimi sina tatizo kama serikali imeona pale palikuwa ni tatizo sawa, lakini serikali haionekani kama iko makini katika kujipanga na matokeo yake ni hii shaghala baghala iliyoko katika miji yetu katika kila kinachoitwa Kituo kipya cha Daladala. Pita pale uone wananchi wanavyoteseka, wanafunzi wanadhalilika ambao ni watoto wetu wadogo, wakija wakifanya vitendo vibaya wale, halafu serikali hii hii inakuja kutuletea ripoti katika Baraza hili kwamba kuna ongezeko la vitendo vya udhalilishaji, tutaviepuka vipi?

Mhe. Spika, mimi chini ya jumba ninalokaa Jumba Nam. 8 la Michenzani pamehamishiwa kituo cha daladala pale, *Zahma-l-karadis* iliyokuweko pale tunaijua sisi tunayoiona pale, wanadhalilika. Hivi Mhe. Waziri, anapojisifu kwamba kaliweza hili anaona fahari kudhalilishwa wananchi kiasi kile? Wananchi wanaotoka Hospitali, wanaotoka maeneo ya masoko, wanahangaika na miziko yao utasema kuna maandamano, ikifika jioni wanakuja maeneo ya pale, hakuna sehemu ya kutulia, hakuna sehemu ya kungojea daladala, ni fujo tu. Ukienda Baraza la Wawakilishi la zamani ni vile vile, kila palipohamishiwa kituo kipya cha daladala. Serikali haikujipanga, ikiri, lakini tatizo kubwa la serikali yetu kiburi, kukiri kwamba imefanya makosa haiwezi ikakubali.

Mhe. Spika, leo tunaambiwa panataka kuendelezwa, mimi nilichokiona Darajani sasa hivi kumefanywa *Parking* pale, lakini wewe unatengeneza *Parking* ya mabari, huku huduma muhimu ya wananchi ya daladala umeisambaza, wananchi wanadhalilika na wanapata tabu, wananchi wanailani serikali yao kwa udhalilishaji, unaowafanyia kwa kuhamisha vituo vya daladala, bila ya mpango maalum katika nchi yetu. Nataka maelezo katika hili.

Mhe. Spika, niseme moja, nilipolizungumza suala la taka, baada ya mmoja katika kufuatilia, si kazi zetu Wawakilishi kufuatilia mambo ya Manispaa, ni kazi ya Madiwani, lakini mambo yanapozidi tunafanya kazi za Madiwani, tunakwenda katika Baraza la Manispaa tunasema mbona taka hazizolewi, tunaambiwa hakuna malipo ya *overtime*. Kwa hiyo, *weekend* taka ikifika Ijumaa hazizolewi mpaka Jumatatu zinarundikana katika maeneo mbali mbali. Fedha hizi zinakwenda wapi? Huduma wale wafanyakazi wa Manispaa wenyewe wanafanya kazi zinazohatarisha afya zao, lakini hakuna huduma zozote ambazo wanapewa.

Mhe. Spika, kwa sababu ya muda, naomba nimalizie eneo moja tu, ni eneo hili la vitambulisho vya Mzanzibari. Tunasema kwamba vitambulisho kwa mujibu wa sheria ni suala la msingi, lakini bado wananchi wengi wanalalamika, hoja inayotolewa kila wakati ni kwamba vitambulisho vipo lakini wananchi hawendi kuchukua mimi siliamini, lazima kuna kitu kinafichwa hapa. Kwa sababu mwananchi huyu tumeona hapa vilipokuja kutolewa vitambulisho vya *NIDA*, wananchi wamefurika kwa maelfu mpaka wengine wamekata roho katika kituo cha kitambulisho Mtoni pale.

Mhe. Spika, kuna mtu kafa kwa kubinywa wakati anahangaika kupata kitambulisho, leo kweli atakuwa na kitambulisho chake katika Idara ya Mzanzibari asiende kukifuata, wakati anajua hawezi kupata huduma yoyote bila ya kitambulisho hiki, kuna mchezo gani unafanywa katika kuambiwa kuna vitambulisho havijachukuliwa, lakini huku wananchi kwa maelfu wanaendelea kudhalilika hawapewi vitambulisho. Tunataka maelezo katika hilo.

Mhe. Spika, kama nilivyosema bahati mbaya muda mara hii ni mchache, lakini maeneo hayo ambayo nimeyataja, mimi sitaki kusema kwamba nitaizuia bajeti hii, sisemi kama naizuia kwa sababu moja tu, kwa sababu naheshimu kwamba ndani yake kuna Vikosi vya SMZ ambavyo sasa hivi vinafanya kazi kubwa sana kwetu.

Mhe. Spika, lakini nataka kuona maelezo ya kina ya waziri katika maeneo ambayo tumeyataja. Hiki alichotuandikia katika kitabu chake huku chini kwamba tushirikiane kuleta mageuzi katika kuwahudumia wananchi, yasiwe maneno ya kauli mbiu tu katika vitabu vyetu. Kama alivyoisema Mhe. Hamza Hassan Juma, kukaa wakapiga maneno tu, wananchi wamechoka na maneno wanataka vitendo, kama tunawahudumia wananchi tuone huduma kweli.

Mhe. Spika tusidanganyane, unaweza ukanijibu mimi hapa, ukadhani kwamba imetosha, lakini wananchi wenyewe wanaona kwamba yanayosemwa na mawaziri wa serikali humu ndani ni maneno matupu au vitendo.

Mhe. Spika, basi mimi nasema nasubiri maelezo ya kina Mhe. Waziri kujibu hoja hizi ili wananchi waridhike kwamba kweli wanahudumiwa na serikali hii.Mhe. Spika. Ahsante.

Mhe. Spika: Mhe. Ismail Jussa Ladhu, tunakushukuru, Waheshimiwa Wajumbe muda umemalizika, twendeni Ijumaa na kikao nakiakhirisha hadi saa kumi na moja jioni.

(Saa 6:00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kwa jioni ya leo kunipa fursa ya kuweza kuchangia mawili matatu katika hotuba ya Waziri wa Nchi (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, nichukue fursa hii kuwashukuru Mhe. Waziri pamoja na timu yake ya watendaji kwa kazi kubwa na nzito ambayo wameifanya hadi leo hii kuweza kutuletea kijitabu hichi kizuri, chenye sura nzuri ambapo leo katika kitabu hichi kuna sura ya Mhe. Waziri mwenyewe akifanya ziara katika baadhi ya maeneo, lakini pia, tukiona kwamba alikuwa anahimiza mazingira yaweze kuchukuliwa hatua ili mji wetu uweze kuwa safi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze kwa kusema kwamba Wizara hii kwa sababu inajumuika na vikosi na vina ulinzi katika nchi yetu imekuwa mtihani mkubwa sana na kwa sababu hiyo nitaiunga mkono kwa asilimia 80, kwanza na asilimia 20 naweka pale ambapo Mhe. Waziri atanitosheleza kwa majibu mazuri ambayo nitakuwa nahitaji ufafanuzi wake pamoja na kujibiwa baadhi ya hoja ambazo zipo mbele yetu.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, nianze pale tulipopaacha juzi juu ya suala zima la magari ambayo yanakaa katika maeneo ya Kisiwandui. Mhe. Waziri juzi alipokuwa akitoa majumuisho hapa alisema kwamba ule utaratibu unaoendelea katika eneo lile sivyo ambavyo walikuwa wamefahamishwa. Pale hapakupaswa kuwa ni kituo cha kuweka madaladala, isipokuwa pale ni eneo ambalo yale magari yalikuwa yanapita kuchukua abiria na kwenda zake, lakini kwa sasa magari pale ndio yamefanya maskani yake.

Mhe Mwenyekiti, Sasa hebu akija Mhe. Waziri aniambie tuanze na pale kwamba wao katika Wizara na Serikali kwa upande wao wamejipanga vipi kuona kwamba yale matakwa yaliyokusudiwa kwa eneo lile yatimizwe na yatekelezwe kwa mujibu wa taratibu, ili tuweze kuepukana na yale matatizo ambayo tuliyazungumza juzi hapa, kwamba katika sababu zilizosababisha daladala ziondoshwe katika maeneo ya Darajani ni pamoja na kwamba wanafunzi walikuwa hawana amani na masomo yao, lakini Skuli ya Kisiwandui kuna wanafunzi ambao wana maumbile maalum, sasa yale magari yaliyokuwepo pale yanazidisha na kuleta matatizo pamoja na mitihani kwa wanafunzi wale.

Mhe Mwenyekiti, lakini ikiwa hiyo haitoshi, katika Baraza lako tukufu miaka mitatu, minne iliyopita nilikuja hapa kuomba katika Wizara husika kutokana na mazingira magumu ambayo tunayapata kwa pale. Tuliomba kwanza tuwekewe tuta, ikashindikana, tukaomba alama za barabara vile vile hatujaziona mpaka leo, sasa tunaona *opposite* yake, tumeletewa magari ya daladala ili mitihani iwe mikubwa zaidi. Tunaomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atuelekeze, ni namna gani kero lile na tatizo lile linaondoka pale na wananchi wa maeneo yale wanapata usalama wa maisha yao na shughuli zao ziweze kwenda vizuri?

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo nakwenda zangu moja kwa moja katika suala ambalo wenzangu walianza kulichangia na suala hili si jengine bali ni huu mradi wa *ZUSP*, mimi naelewa kwamba hii miradi inayokuja kuna baadhi inakuwa ina maeneo mengi, lakini kinachonishtusha na kunishangaza zaidi ni kuona kwamba pamoja na muda mrefu ambao mradi wa *ZUSP* umekuwa nao, lakini vile vile, tunashindwa kuelewa ni lini hasa mradi huu utaanza ku-*take off* na kuweza kuona kwamba yale mambo ya msingi ambayo tunayasubiri kwa muda mrefu yanaanza kuchukuliwa hatua.

Mhe. Mwenyekiti, sasa atakapokuja hapa Mhe. Waziri, nitamuomba atufahamishe hasa kwa kina, ni lini hasa mradi huu wa *ZUSP* hususan katika eneo la mitaro pamoja na maeneo ya misingi ambayo imejaa katika maeneo yetu?

Mhe. Mwenyekiti, hapa naomba ku-*declare interest* kidogo katika Jimbo letu la Kikwajuni. Katika Jimbo la Kikwajuni imekuwa kama ndio jalala kwa maeneo yote ya majimbo mengine. Maji machagu na maji ya mvua ambayo yanatoka katika maeneo ya Magomeni huko, Kwahani na maeneo mengine yote yanaishia katika maeneo ya Kikwajuni. Sasa na pale tulikuwa tuna misingi mingi na ya kizamani, ipo misingi ambayo imetengenezwa kwa gharama kubwa, lakini misingi ile haifanyi kazi.

Mhe. Mwenyekiti, na sasa hivi inapelekea kuhatarisha amani na usalama wa wananchi wanaokaa katika jimbo lile. Hususan tukiangalia wakati wa mvua ambazo zinakuwa ni kali zaidi maeneo ya Gongoni, Kilimani, Kilimani Mashariki na Kilimani Bar, kule inakuwa maji ni mengi na wakati mwengine yanasababisha hatari na vile vile maisha ya watoto kuweza kupotea kama ambavyo yamekwisha kupotea.

Mhe. Mwenyekiti, juzi tulifanya ziara na Mheshimiwa mwenzangu wa Jimbo la Mpendae, Mhe. Mohammed Said Mohammed tukaenda katika maeneo ambayo yale maji ya mvua yakitokea katika maeneo ya juu yanakwenda kwanza kukusanyika pale, halafu baadae yanakuja katika ule mtaro mkubwa ambao unaelekeza maji yake Kilimani Bar kushuka chini kabisa kule. Sasa cha hatari zaidi ambacho kinaonekana ni kuona kwamba hata ile *Simtank* yenyewe kila siku ambayo tunaambiwa itajengwa, itafanywa hivi, sasa hivi hali yake ni mbaya na hali imekuwa ngumu na imekuwa inahatarisha zaidi na hatari inayojitokeza sasa hivi, si lazima mvua zinyeshe. Hatari inayojitokeza sasa hivi, wakitoka watoto tu kwenda kucheza, basi inawezekana ikaja ikaleta maafa makubwa katika nchi na ikawa ni mtihani mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, sasa ningeliomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atusaidie hasa huu mradi ambao toka mwaka 2010 upo mpaka leo, bado hatujaona maendeleo yake ya kiutendaji, ni lini hasa mradi huu utaanza ku-*take off* na kuona kwamba wananchi wetu katika maeneo yetu wanafaidika na mradi huu.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni suala zima la taka ambazo zimejaa katika maeneo yetu. Katika eneo la Hospitali ya *Marie Stopes* kwa nyuma kule kuna jaa kubwa sana na kuna hali ambayo inahatarisha maisha hata ya watu wanaoishi katika eneo lile. Kusema kweli, hali ile kwa binadamu wa kawaida ni mtihani mkubwa na maradhi ya aina yoyote yanaweza kutokezea na watu wakaweza kupata maradhi mengi na kwa wingi na baadae Serikali ikapata hasara kubwa katika kuwatibu watu wale.

Mhe. Mwenyekiti, sasa tungeliomba kwanza nataka kufahamu ni lini hasa jaa lile litaondoshwa pale, lakini vile vile, ni utaratibu gani unachukuliwa ili kuona kwamba eneo jengine la kuweka takataka linawekwa na wale watu wanaokaa katika maeneo yale wanafaidika na hali ya kuweza kutupa taka zao baada ya matumizi yao ya kawaida.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo, nilisema kidogo niende katika ukurasa wa 26 kifungu 0201 Idara ya Utawala na Rasilimali Watu. Katika kifungu kidogo cha 211110 kwenye posho maalum ningemuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa aje kunisaidia, kwa sababu mwaka 2013/2014 aliomba na akaidhinishiwa milioni 141,508,000/=, lakini mwaka 2014/2015 ameomba milioni 239,000,000/=. Sasa hebu tusaidie kuna nini kilichozidi hata ikabidi kiwango hichi kimekua sana kwa namna fulani.

Mhe. Mwenyekiti, lakini tukiondoka hapo chini yake, hapa katika kifungu kidogo cha 211116 posho, vikao na Kamati mwaka jana aliomba milioni 10,680,000/=, mwaka huu ameomba milioni 29,640,000/=.Tukiteremka chini katika kifungu kidogo 2201000 gharama za vifaa, huduma ya mawasiliano katika *bullet* namba 220101 gharama za simu, mwaka jana Mhe. Waziri aliomba shilingi milioni 2,400,000/=, lakini mwaka huu Mhe. Waziri ameomba

shilingi milioni 9,800,000/=. Je, kuna huduma za simu ambazo zaidi zimeongezeka au simu zimekuwa nyingi ndani ya Ofisi yake? Akija atusaidie hapa.

Mhe. Mwenyekiti, lakini hapo hapo katika huduma za mtandao ambapo kwa sasa ndio jambo ambalo linakuwa linasaidia sana katika maendeleo ya nchi yetu hususan baada ya kwisha kupata mradi wa *E-Government.* Hapa chini katika *bullet* 220108 huduma za mtandao, mwaka jana aliomba milioni 24, lakini mwaka huu ameomba milioni 3. Je, yale malengo ambayo alikuwa amejipangia yamekamilika au kuna kitu gani cha ziada kilichosababisha hata hizi fedha zikashuka kiasi hiki. Kwa sababu utaratibu wa pesa huu ikizidi lazima iulizwe na inapopungua vile vile ipo haki ya kuulizwa.

Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu hicho hicho cha 0201 *bullet* 220300 gharama za safari, kwa mujibu wa maelekezo na hotuba kuu ile ambayo ilikuwa imesomwa hapa safari za nje zote zilikuwa zimepunguzwa kwa asilimia kubwa, lakini hapa katika Ibara hii 220302, safari za nje mwaka jana Mhe. Waziri aliomba milioni 27, mwaka huu anaomba milioni 29, inaonekana kwake yeye safari za nje zimezidi. Je, atueleze kwa sababu gani hata ikawa hivi, lakini jengine ukija chini huku kuna gharama za mahoteli katika *bullet* 220305 mwaka jana aliomba milioni 35,060,000/=, mwaka huu ameomba milioni 50,780,000/=.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo nakwenda ukurasa wa 28 ambapo napo vile vile kuna maeneo mawili nilitaka kuomba ufafanuzi, kuna ruzuku hapa ya *HIV*. Juzi tulipokuwa tunachangia hapa katika Kitengo cha Ofisi ya Rais Ikulu tulikuta pana ziro hapa tukaulizana vile vile, lakini leo katika Ofisi hii ya Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ katika *bullet* 263100 Mhe. Waziri, hapa katika kifungu kidogo cha 263178 mwaka jana aliomba milioni 2,400,000/=, lakini mwaka huu ameomba milioni 7,090,000/=. Sasa hapa kidogo hii hali inatisha itabidi atusaidie Mhe. Waziri, atupe ufafanuzi. Je, tuna matatizo makubwa katika maeneo yetu ya ulinzi huko na mambo mengine?

Mhe. Mwenyekiti, lakini kwa kumalizia katika kifungu namba 281400, kifungu kidogo 281402 gharama za kukodi kumbi, tulikubaliana katika bajeti kubwa kule kwamba gharama za kukodi kumbi zitakuwa zinapunguzwa badala yake tutakuwa tunatumia kumbi zetu za kawaida ili kuweza kupunguza matumizi ambayo yatakuwa sio ya lazima. Mwaka jana Mhe. Waziri aliomba shilingi 400,000/= kwa ajili ya kumbi, mwaka huu ameomba milioni 6,110,000/=. Tunaomba Mhe. Waziri akija hapa atusaidie.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo kwa heshima na taadhima narejea tena kuzungumzia suala langu la mwisho zito na pevu ambalo namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atupe mwelekeo wake.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa maoni yangu, nahisi kwamba wakati umefika sasa kwa Madiwani wetu ambao wanachaguliwa kusimamia katika Manispaa pamoja na Halmashauri zetu katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba na wao sasa kutengenezewa utaratibu wa kuanza kulipwa mishahara, kwa sababu Madiwani wanafanya kazi kubwa sana, wanafanya kazi nzito, huwa ni kiunganishi baina ya Serikali Kuu na Serikali za Mikoa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa msingi huo basi, ningeliomba na wao sasa wafikiriwe na waweze kupewa mishahara, isiwe wanapewa posho kama ambavyo tumeona katika kijitabu hichi ambapo maposho yao yanaboreshwa. Wakati wa kuondoshwa posho na Madiwani kuweza kulipwa mishahara kwa sasa hivi umefika na naiomba Serikali Kuu itutengenezee utaratibu wa kuweza kuona kwamba Madiwani katika mwaka wa fedha unaokuja huo wanatengenezewa mishahara na wao wanalipwa kama ambavyo Wawakilishi na Wabunge wanalipwa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelekezo hayo, kwa mara nyengine tena naunga mkono hoja hii kwa asilimia 80, asilimia 20 naweka mpaka nitakapokuja kuletewa majibu yatakayonitosheleza hususan suala la Kisiwandui.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nikushukuru kupata nafasi hii kuweza kuchangia jioni hii ya leo, mimi mchango wangu nitaanzia moja kwa moja katika Baraza la Manispaa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijatoa mchango huu, mimi nilikuwa nataka nimuombe Mhe. Waziri, kumtanabahisha kwa sababu wengi wa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuna imani kubwa sana na Mhe. Haji Omar Kheir katika utendaji wake wa kazi. Nasema hii kwa sababu baada ya kuona tu namna gani alivyokuwa akisimamia katika

Wizara ya Utumishi, tulijenga imani na tukajenga imani kubwa sana baada ya kutangazwa kuwa Waziri katika taasisi hii. Sasa nataka nimtanabahishe kuwa na tahadhari kwa sababu hii Wizara ni nzito na yeye mwenyewe naamini anaifahamu.

Mhe. Mwenyekiti, ni nzito katika utendaji wa kazi, lakini ni nzito kutokana na ukubwa wake. Hata Mhe. Makame Mshimba Mbarouk ndio akawa anataka kutoa pendekezo na baadhi ya Idara ziondoke, yeye alitaka zitoke vile vile na Waziri wake. Sasa tahadhari ninayotaka kumpa kwamba awe makini ili tusije kufika pahala ikaja ikamuondoshea ile sifa yake ambayo sisi tumejenga imani kwake yeye.

Mhe. Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu ya hali halisi tuliyokuwa nayo, hili kila mtu analizungumza na mimi naendelea kulizungumza. Tukitaka tusitake tatizo la uchafu katika Manispaa ya Zanzibar limekithiri kupita kiasi. Sasa hii tutamnyooshea kidole yeye kwamba anashindwa kuusimamia mji kuwa katika mazingira yaliyokuwa mazuri, kumbe kuna baadhi ya taasisi zimekuwa zimejenga ulemavu wa kutokutaka kubadilika na kufanya kazi katika umakini.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hii ndio tahadhari niliyokuwa nasema, mimi mara nyingi huwa nasema na huwa natoa mfano sana kwa wenzetu wa Tanzania Bara. Inakuwa kuwaje maana yake tunafika pahala baadhi ya viongozi au wasimamizi wanashindwa kazi wanashindwa kuwachukulia hatua na matokeo yake tunakuwa tunaendelea katika ule ulemavu wa kustahamiliana.

Mhe. Mwenyekiti, wenzetu wa Manispaa bado hawajajipanga kabisa katika suala zima la kuona kwamba namna gani wanaweza kukabiliana na matatizo ya usafi katika mji wetu. Kwa sababu majaa yetu katika Manispaa ya Zanzibar mengi yao mimi nitazungumzia jimbo langu, unayakuta karibuni ya yote yapo katikati ya mitaa. Jaa la Mikunguni lipo katikati ya mtaa kwenye eneo la Hospitali ya Imani pale, jaa la Kwaalimsha lipo katikati ya mtaa kwenye daraja, jaa la Muungano lipo katikati ya mtaa chini ya Madrasa na jaa la Kwahani Uwanja wa Farasi lipo katikati ya mtaa.

Mhe. Mwenyekiti, sasa inakuwa ni tatizo wakati kama huu wa mvua athari inakuwa kubwa, kwa sababu ule uchafu wote unatiririka na unaelekea majumbani na unaleta usalama mdogo wa maisha ya wananchi wetu. Sasa mimi nashindwa kufahamu tatizo ni nini? Sasa hivi umeanza kujitokeza utaratibu wa kuzoa taka kila baada ya siku mbili, tatu kwa kijiko. Sasa nakuwa napata tabu kwamba Manispaa hawa hawa wamejenga Slabi katika maeneo kuhifadhiwa taka, lakini baada ya kuona gari *track* kubeba zile taka kutia kwenye magari wanatumia vijiko, zile silabi ambazo zimejengwa kwa gharama kubwa wanaanza kuzibomoa. Sasa bado watu wetu hawajajipanga vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ninafikiri kuna haja ya kujipanga vizuri, labda ninataka niseme nimuombe sana Mhe. Waziri kama kuna tatizo tuambizane. Tunajua kwamba kuna mradi wa *ZUSP* tunafahamu sana, lakini inawezekana labda kuna maeneo yanachelewesha huu mradi kuweza kufanya kazi kwa wakati ili kuweza kuondosha hili tatizo, maana yake zamani ilikuwa tatizo ni magari. Magari kidogo, lakini tunashukuru sasa hivi tunashukuru tumepata magari yale ya kisasa baadhi, tumepata yale magari ya *open* baadhi. Sasa tuelezwe labda tatizo lipo wapi katika namna kuona kujipanga katika suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, na hili suala limekuwa linawapa taabu sana Waheshimiwa Madiwani wetu, Madiwani wa Manispaa wa Zanzibar wamekuwa hawana raha ya kutembea mitaani kwa sababu wanajua wakitembea tu wanaoneshwa majaa na wanaambiwa hawafanyi kazi. Sasa hivi Diwani kufikia pahala kuambia hafanyi kazi, afanye kazi gani kwa sababu yeye kazi yake ni kusimamia taasisi na anapiga kelele kwenye taasisi, lakini taasisi inaonekana imeshindwa kujipanga katika suala zima hili la uzoaji wa taka.

Mhe. Mwenyekiti, sasa kila siku inabidi Madiwani tunawakosesha sifa za kazi, wanaonekana Madiwani hawafanyi kazi, lakini kumbe taasisi yenyewe inaonekana haijajipanga vizuri katika suala zima hili la uzoaji taka. Sasa nimuombe Mhe.Waziri, kusimamia vya kutosha taasisi ya Manispaa ili kuona kwamba basi tunabadilisha *at least* kuona mji wetu kwamba unabadilika katika mazingira mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, lakini nimalizie katika taasisi hii ya Manispaa kwa kusema kwamba Baraza la Manispaa walianzisha utamaduni mzuri sana. Walianzisha utamaduni wa kuanzisha vikundi vya usafi wa mazingira katika Shehia. Ni jambo zuri na ninafikiri katika majimbo ambayo yanahitaji kupigiwa mfano kwa kuunda vikundi hivi,

ninafikiri ni Jimbo la Kwahani. Tuna vikundi kila Shehia na tayari walikuwa na zana na kufanya kazi kila baada ya muda, lakini tunachofanya kupata taabu katika vikundi vyetu ni ushirikiano uliokuwa mzuri baina ya taasisi ya serikali, yaani Baraza la Manispaa na vile vikundi vyenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, hapa panatokezea ugumu kutokana na kutokuwa na sheria nzuri kwa vile vikundi binafsi vya uzoaji wa taka kwa sababu vikundi vinazoa taka, lakini inaonekana baadhi ya wenye majumba au baadhi ya wafanyabiashara wanashindwa kulipia zile kodi, kuvilipa vile vikundi kwa sababu hakuna sheria nzito ambayo inawabana katika suala zima la kutozwa kodi. Sasa unakuta kwamba watu wanajituma, vile vikundi vya usafi vinajituma, lakini kutokana na ugumu wanaoupata kutokuwa na sheria yenyewe haijasimama vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, sasa unakuta kwamba mapato yenyewe yanakuwa ni madogo na baadae wale wananchi wale walioamua kujiunga katika vile vikundi wanaanza kukata matumaini, kwa sababu unamkuta mwananchi anazoa taka katika majumba, lakini mwisho wa mwezi anaambulia shilingi elfu kumi au shilingi elfu ishirini, matokeo yake anaacha.

Mhe. Mwenyekiti, sasa ile dhamira nzuri ya kuunda vile vikundi, mimi ninahisi itafika pahala huenda isifanikiwe. Sasa nimuombe Mhe. Waziri, ahakikishe kwamba zile sheria zinafanyiwa haraka kufanyiwa marekebisho ili vile vikundi vyetu viweze kupata imara na ninasema kwamba kama unataka kufanya majaribio ya vikundi kwa majimbo, basi ninakuomba uanze katika Jimbo la Kwahani kwa sababu vikundi vyake vimesimama vizuri, Madiwani wangu wamesimamia vikundi vyao, vikundi vimeimarika na vina zana nzuri na ninataka nikuhakikishie na sisi viongozi pia tumejipanga vizuri na karibuni tu, tunategemea tu kuja kukabidhi vifaa visivyopungua milioni thalathini pakiwa na gari ya usafi ya jimbo. Sasa ikiwa jimbo limejipanga vizuri, hakuna sababu na taasisi nayo kutokuunga mkono vizuri katika suala zima la usafi, kwa sababu tunajua dhamira ya usafi ni ya kila mtu na sisi kama ni viongozi kuna haja ya kutoa mashirikiano kwa nchi yetu. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, ninataka nije katika Idara Maalum. Wenzangu wengi wamezungumzia na mimi kama kiongozi ambaye nina wananchi ambao nao ni wafanyakazi wengi katika Idara Maalum, basi ninahisi kuna haja ya mimi kulizungumzia suala hili. Suala la maslahi kwa wafanyakazi wetu wa vikosi vya Idara Maalum.

Mhe. Mwenyekiti, nimeona katika kitabu chake Mhe. Waziri na nimefarijika kidogo nimeona hapa kwamba maslahi yameanza kurekebishwa kuanzia tarehe 1 Machi, 2014 na ndio maana niliposema kwamba Mhe.Waziri wetu ninamshukuru sana kwa jitihada ambazo anazozifanya na tuna imani na tunajenga matumaini yake, lakini hapa ninataka nimueleze Mhe. Waziri kidogo kwamba pamoja na usimamizi mzuri wa maslahi yao, lakini bado ninamuomba sana aendelee kusimamia suala zima la upandishaji wa vyeo katika vikosi hivi vya SMZ. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, bado tuna mashaka kwamba upendeleo wa kuangaliana sura, udugu bado haujaondoka katika suala zima la upandishwaji wa vyeo. Ninafahamu kwamba utaratibu umetayarisha kutaka kuuanza, ninachokuomba ni kuuharakisha ili hili zoezi likamilike ili mtu apande cheo kutokana na muda wake na sifa zake alizokuwa nazo na tuondoshe yale manung'uniko kwa wananchi wetu. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, chengine katika Idara Maalum, Mhe. Waziri hili ninataka nimuombe anisaidie. Ule utaratibu wa kuanzisha Kampuni ya ulinzi umefikia katika hatua gani? Kwa sababu sote tunakiri kwamba ajira zimekuwa ngumu kwa vijana wetu, tukisubiri ajira za serikali muda unakuwa ni mrefu na ajira zenyewe zinakuwa ni kidogo na kila siku vijana wanamaliza masomo, matokeo yake wanakuwa wanasubiri ajira mitaani na mitaani kwenyewe kazi zenyewe zinakuwa ni mashaka na zinapelekea wengine tena kufikia kujitumbukiza katika mambo yaliyokuwa hayana msingi.

Mhe. Mwenyekiti, sasa wenzetu kule walikuwa wanasema sana, wenzetu wameanza kupiga hatua ya kutosha kwa Kampuni binafsi za ulinzi kupitia katika vikosi vyao vya ulinzi. Kuna SUMA JKT kule wapo vizuri, sasa sijajua Mhe. Waziri, labda atakapokuja hapa na wao wajipanga vipi na wanategemea lini vijana wetu hawa wataanza kunufaika, kwa wale ambao wanakuwa wanakosa sifa au wenyewe watakapokuwa wanatoa maamuzi wa kufanya kazi katika maeneo ya makampuni haya binafsi.

Mhe. Mwenyekiti, la kumalizia katika Idara Maalum pamoja na maslahi mazuri ambayo yametengenezwa na serikali inaendelea kuyatengeneza, niombe kwamba suala la usafiri kwa vikosi vyetu, suala hili kwa vikosi vyetu

bado halipo vizuri. Magari wanayotumia bado hayana mazingira ya vikosi vya ulinzi. Sababu ya kusema hivyo, wakati mwengine unakuta vijana wetu hawa wanapanda mpaka vi-*carries* kwenda katika maeneo yao ya ulinzi. Sasa tunajua gari za wanajeshi ni gari maalum ambazo zinategemea katika masuala mazima ya kujenga usalama wao.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nimwambie Mhe. Waziri, aliangalie suala la kuhakikisha kwamba vikosi vinapata gari za kutosha ili kuwapa wepesi wa utendaji wa kazi zao.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo, ninataka nizungumzie suala dogo tu, ilikuwa ninataka nizungumzie suala la mikoa, kumejitokeza tabia ya watu kuanza kuvamia ya mabonde yetu kwa sababu niliona katika suala la mikoa namna walivyoelezea ya kilimo kwenye maeneo yao. Sasa kuna mabonde haya kipindi kirefu nilikuwa nikipigia makelele katika Mkoa wa Mjini/Magharibi. Bonde la Mwera na Kijito Upele. Haya mabonde tatizo lenyewe wapo wapi? Yaani sasa hivi watu wanajenga katika yale mabonde ambayo serikali ilikuwa imeyatenga kwa ajili ya kilimo, lakini sio tatizo kujenga kwamba kilimo tumeamua hatulimi tena, lakini tatizo baadae serikali yetu itakuja kupata mzigo yatakapokuja mafuriko, itabidi serikali ije ibebe gharama ya kuwalipa watu kwa kujenga mahala palipokuwa hapastahiki kujengwa.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nimuombe Mhe. Waziri, kama hili kaliona na kama kaliona kuna mikakati gani ambayo umeipanga katika kujitahidi kwenye suala zima la kukabiliana na watu ambao wamejenga katika mabonde yaliyokuwa yametengwa kwa kazi maalum ya kilimo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini jengine ambalo Mhe. Waziri ninataka nimtanabahishe kuna jambo hili la mwenge wetu wa uhuru. Mimi ni muumini wa mwenge wa uhuru, kwa sababu unamurika maadui zetu wa ndani na nje ya nchi na unaleta maendeleo kwa wananchi wake, lakini ninataka kumwambia Mhe. Waziri katika hili ni dogo tu, kuna baadhi ya wakuu wa Wilaya wamekuwa wanajenga utamaduni wa kuwataka Masheha wao kuwekewa kima maalum cha kuchangia mwenge.

Mhe. Mwenyekiti, sasa mimi ninafikiri si jambo la busara kwa sababu unapompa kima maalum, unampa kazi kwa sababu ile michango tunatoa sisi huku uraiani kwa wananchi mbali mbali na tupo tayari na tutachangia, lakini kusiwe na kima maalum kwa sababu unampa kima kama hajakifikisha Sheha anaanza kupata taabu. Tuambizane tu kwamba tujitahidi kuwahamasisha wananchi wetu wafahamu umuhimu wa mwenge na tusomeshe somo la mwenge ili watu wajue faida ya mwenge, lakini tusije tukatoa kima matokeo yake Masheha wetu wanaanza kupata taabu katika kufikisha hicho kima, kima kinakuwa hakifiki na anaanza kuwa mzito na yeye anamuhofia bosi wake asije akaonekana, labda yeye hakufanya kazi vizuri au labda yeye mwenge haupendi, lakini tatizo linakuwa gumu kwa upande wa Masheha wetu. Sasa niseme kwamba kuna haja ya kutoa taaluma na kuacha kuwapa Masheha shindikizo la kufikia kima maalum cha kwenye suala la mwenge.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kuna jambo nilisahau kidogo, ninataka Mhe. Waziri atakapokuja anieleze lilikuwa linaingia pale pale katika suala la Manispaa, lakini nilisahau ikawa sikuwahi kulizungumza, Serikali yetu ya Mapinduzi matukufu ya Zanzibar kwa nia njema kabisa walivyoweka *Site plan* ya Manispaa yake, waliweka katika mazingira yaliyokuwa mazuri sana, walieka maeneo ya makaazi na maeneo ya huduma, lakini waliweka maeneo ya wazi kwa ajili ya vijana wetu kuweza kuyatumia yale maeneo kwa shughuli zao mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, sasa mimi ninaanza kupata wasi wasi kabisa yale malengo na dhamira nzuri ya serikali yetu kuanza kutoweka. Ujenzi katika maeneo yetu ya wazi imekuwa ya kiholela sana. Sasa sijui hawa Manispaa wanakuwa wanatumia vigezo vya kutoa vibali, kwa sababu isije kuwa ardhi katoa kibali, kwa sababu watu wa ardhi imani yao inakuwa ndogo sana kwao, kwa sababu wameshazoea kutoa ardhi mpaka leo migogoro imekuwa mingi, lakini isijekuwa mwenzangu kaharibu na wewe ukaharibu hata kama ardhi katoa haki ya kumpa ardhi kama hapastahiki pale pahala mwambie hapastahiki.

Mhe. Mwenyekiti, ninasikitika sana ninapokwenda Darajani nikalikuta jengo lililojengwa katika eneo la wazi karibu na uwanja wa *basketball*. Hata kama ardhi walitoa kiwanja, lakini wewe kazi yako ni kulinda maeneo ya wazi. Hivi sasa ile njia haipitiki kumejengwa jengo atakuja kuniambia ni tajiri gani ambaye ana uwezo kujenga jengo mpaka kwenye njia. Hii serikali ipo wapi? Kama kaharibu ardhi, kwa nini wewe mwenye kibali usizuie? Mhe. Waziri, nambie jengo lile ni nini ambalo limejengwa Darajani kwenye njia, maeneo ambayo sasa hivi tunahangaika, maeneo

ya kuegesha magari hakuna, maeneno ya watu kupumzika hakuna, maeneo ambayo serikali imeyatenga watu wachukua kwa manufaa yao.

Mhe. Mwenyekiti, hili kidogo nitakuwa mgumu sana, Mhe. Waziri, aje anieleze nani kajenga na kwa misingi gani? Wakati sisi tunahangaika kujenga maeneo ya huduma za jamii yanatushinda. .(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa ninataka nimpongeze Mhe. Waziri, kwa jitihada ambazo amezifanya kwa makusudi ya kusafisha maeneo ya kufanya biashara barabarani. Tulikuwa tunapata taabu sana, nyakati za asubuhi ilikuwa ukitaka kupita Mwanakwerekwe, basi unataka kufika mjini saa moja utoke saa kumi na mbili.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, zimebakia dakika 3.

Mhe. Ali Salum Haji: Nitajitahidi nizimalize, kwa wakati wako ninakuheshimu sana.

Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa lile eneo huwezi kupita kwa muda nusu saa ilikuwa unataka kupita Mwanakwerekwe unaganda, lakini sasa hivi *Alhamdulillah* maeneo yale yapo safi, magari yanapita kwa murua, wanafunzi ambao wanaotaka kutumia njia zile hususan wanafunzi wa Mwanakwerekwe wanakata njia kwa utaratibu, askari wanafanya kazi zao vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nimpongeze sana kwa ile jitihada ambayo aliyoifanya na maeneo yaliyobakia, basi Mhe. Waziri, ujitahidi uyafanyie kazi. Maeneo kutoka Suma kwenda zako Mchangani, likija kuingia janga la moto maeneo ya Mbuyuni watu watakufa. Wafanyabiashara wanaweka biashara mpaka barabarani. Sisi tunaangalia maisha, hatuangalii athari ya wananchi. Leo umeshaingia moto, *fire* inataka kuzima watu wapo barabarani gari haiendi ni tatizo. Maliza wafanyabiashara wanaofanya biashara katika maeneo yaliyokuwa hayastahiki waondoke ili kutoa nafasi kwa wananchi wetu kupata huduma za kawaida.

Mhe. Mwenyekiti, lakini katika suala hilo hilo la Mwanakwerekwe sokoni, ninataka nikuombe sana bado eneo la nyuma ya soko, kuna soko dogo na kuna machinjio ambayo mazingira sio mazuri. Ninavyofahamu mimi tangu nilipokuwa Diwani, tuliwahi kufanya *Proposal* ya kutaka kujenga katika lile eneo limefikiwa wapi, tunakwama nini Mhe. Waziri, katika kulitanua soko la Mwanakwerekwe ili liweze kutoa huduma iliyokuwa katika hali nzuri, kwa sababu maeneo ya ndani pia kutokana na kuondosha watu nje, watu wameingia ndani, sasa ufinyu ndani umekuwa mkubwa, biashara ndani inabidi njia zile za kupita watu wanatumia huduma zao kwa ajili ya kufanya biashara zao.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia kabisa kwa kuheshimu muda wako, naomba sana kwa heshima zote nimpongeze Mkurugenzi wa vitambulisho kwa kazi nzuri anayoifanya. Yale matatizo au malalamiko ambayo mara nyingi tulikuwa tunapiga kelele ya kutotenda haki au kutokufuata utaratibu yameweza kufanyiwa ufumbuzi, hali sasa hivi ya vitambulisho ni nzuri, matangazo kila siku mitaani yanatoka kwa wale ambao hawajachukua vitambulisho vyao, Masheha wamepewa taaluma na hili Mhe. Waziri, aliyepita alifanya jitihada ya kwenda katika maeneo mbali mbali kwenda kuangalia. Sasa ni lazima nitoe pongezi na hili sio kama ninatoa pongezi mimi tu, katika kitabu chao wao wenyewe pia wameonesha namna walivyoweza kuvipata hivi vyeti mara nane ya ubora wa kazi zao katika Kampuni za Kimataifa.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, maliza muda wako umekwisha.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo, ninashukuru kwa dhati. Kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwahani ninaunga mkono hotuba hii. Ninashukuru sana. (Makofi)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mheshimiwa. Sasa ninamkaribisha Mhe. Mwanaidi Kassim na baada ya hapo atafuata Mhe. Asha Abdu Haji na baadae ajitayarishe Mhe. Salmin Awadh Salmin.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nikuombe radhi kwa sauti yangu, ipo kavu imekauka kwa sababu ya baridi, halafu nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia na mimi kuweza kuchangia hotuba hii jioni hii.

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kwa kutuwasilishia hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2014/2015.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, pia, niwapongeze watendaji wote kwa kuandaa hotuba hii, hotuba ambayo imejitosheleza. Nianze na Idara ya Uendeshaji na Utumishi. Idara hii ina jukumu kubwa la kuhakikisha kuwa wizara inaimarisha mipango yake ya upatikanaji wa raslimali watu. Naiomba idara hii kusimamia vizuri mipango yake iliyojipangia na jitihada ya kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wafanyakazi ili kufanya kazi zao vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika Idara ya Utaratibu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Pia, niipongeze idara hii kwa kufanya kazi zake vizuri, basi naiomba idara kuwa na mashirikiano baina ya viongozi wa mikoa na wilaya, lakini pia, idara hii ina changamoto nyingi kama vile tuseme bandari bubu.

Mhe. Mwenyekiti, bandari bubu ni tatizo, kama kitabu kinavyojieleza kuwa bandari bubu husafirishiwa magendo pamoja na wanyama ambao hawajafanyiwa uchunguzi. Hili ni tatizo, kusema kweli bado tatizo hili halijapatiwa ufumbuzi. Namuomba Mhe.Waziri, asimamie wizara hii hasa hususan kwenye bandari bubu.Kama tulivyoelezwa hapa, magendo kweli yapo yanazidi, wanyama wanaingizwa tukizingatia maradhi tele sasa hivi. Kwa hivyo, ninamuomba Mhe. Waziri, kuisimamia vyema idara hii ili kuona matatizo haya yanaondoka na pia kuhakikisha ulinzi uimara unapatikana katika maeneo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Nianze na Baraza la Manispaa. Baraza la Manispaa ni kweli, kama walivyosema wenzangu katika mji wetu uchafu umekithiri, majaa hayatambulikani, wapi pana jaa. Wana mipango mizuri walikuwa wamejipangia, lakini mipango hiyo ni vigumu sana kuitekeleza kwa sababu baada ya taka kuchukua kila siku, taka zinaweza kukaa wiki mbili, wiki tatu hazijachukuliwa. Sasa niambie taka zile kama hazijachukuliwa wiki mbili au wiki tatu zinakuwaje siku ya kuchukuliwa.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, kuhusu usafi kwenye njia. Kama alivyosema Mhe. Hamza Hassan kwamba barabara zetu nzuri, lakini zina michanga, nusu ya barabara unakuta michanga imejaa. Kwa hivyo, haileti mandhari nzuri katika njia zetu tunazopita kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nilipongeze Baraza la Manispaa kwa ukusanyaji wake mzuri wa mapato, pamoja na Halmashauri zake. Hawa madiwani pamoja na kazi nzuri wanazofanya, lakini bado wanapewa posho. Namuomba Mhe. Waziri aangalie vizuri Baraza la Manispaa na Halmashauri zinakusanya pesa zake vizuri, basi iwafanyie utaratibu wa mshahara na pale wanapostaafu kama hakuna kiinua mgongo, basi hata kifuta jasho wapewe. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea hapa hapa Baraza la Manispaa, nije kwenye nafasi za wanawake kwa madiwani. Suala hili tulilipigia kelele sana, tuliulizia hapa tukaambiwa inatayarishwa hiyo asilimia, kwa sababu kwenye Bunge tayari nafasi hizo zimeshapatikana, kwenye Baraza la Wawakilishi tayari nafasi hizi zimeshapatikana, lakini bado kama wanawake tunataka tufike 50 kwa 50, lakini kwa kupitia madiwani bado. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri, aniambie suala hili la madiwani limekwama wapi na utekelezaji wake kwa nini ni mgumu, mbona Bunge na Baraza la Wawakilishi tayari?

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo niingie katika Mkoa wa Mjini Magharibi. Mkoa huu nasikitika sana Ofisi ya Mkuu wa Wilaya wa Mjini, mara ile nilichangia kuhusu Ofisi ya Mkuu wa Wilaya. Mkuu wa Wilaya hana Ofisi. Mimi mwenyewe binafsi nilikwenda pale katika Ofisi ile, hapo Bwawani walipokuwa wamekodi, yaani nilisikitika. Kusema kweli katika hivyo vyumba ambavyo wamefanya Ofisi, kuna maofisa watano au sita wamekaa kwa pamoja. Sasa najiuliza hawa wanafanyakazi vipi, wakija wageni pale wanazungumza nao vipi. Ukizingatia hivyo, vyumba vyenyewe na choo kipo hapo hapo, mlango wa choo uko wazi, yaani ni matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri, basi suala hili mwaka jana nililichangia kwenye bajeti, lakini bado naona ile Ofisi iko pale pale katika hoteli ya Bwawani. Pia, tukizingatia pale wanalipa kodi kubwa. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri awatizame kwa jicho la huruma ili awatafutie jengo, pale wahame hawajakaa vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika Tume ya Utumishi Idara Maalum za SMZ. Naipongeza serikali kwa kazi zake nzuri zinazofanyika kila siku. Pia, navipongeza vikosi vyote vya SMZ, kwa kuhakikisha mipango yao wanayojipangia kusimamia vizuri, wanastahili pongezi kubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, pia, namuomba Mhe. Waziri, aliangalie suala la pesa za likizo kwa wafanyakazi wetu hawa wa SMZ. Pana malalamiko hapa wanapokuwa likizo wafanyakazi, hawa pesa zao hawapati kama inavyotakiwa. Mtu anakwenda likizo mpaka anarudi bado pesa yake ya likizo hajapata. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri ajitahidi kuliangalia suala hili ili kuondosha malalamiko ya wafanyakazi wetu hawa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa vile sauti yangu inazidi kudidimia, naunga mkono bajeti hii kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Mjini Magharibi kwa asilimia mia juu ya mia. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa. Anayefuata sasa hivi ni Mhe. Asha Abdu Haji, ajitayarishe Mhe. Salmin Awadh Salmin na baadae atafuata Mhe. Saleh Nassor Juma.

Mhe. Asha Abdu Haji: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kunipa fursa ya kuchangia bajeti hii. Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya njema jioni hii. Pili, napenda kukupongeza wewe kwa kunipa fursa ya kuchangia bajeti hii. Vile vile, nampongeza Mhe. Waziri na watendaji wake kwa kuleta bajeti yake mbele yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Halmashauri nyingi zilikusanya mapato makubwa na kuvuka malengo, kwa mfano Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni na ya Wilaya ya Mkoani. Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni ilipangiwa kukusanya shilingi milioni 80,000,000, lakini ilikusanya shilingi milioni 99,236,650 sawa na asilimi 123.

Mhe. Mwenyekiti, Wilaya ya Mkoani ilipangiwa kukusanya shilingi milioni 51,265,000, lakini ilikuwanya shilingi milioni 74,800,669 ni sawa na asilimia 146. Namuuliza Mhe. Waziri, je, mapato haya yanawafikia wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja ilipangiwa kukusanya milioni 129,886,000, lakini ilikusanya shilingi milioni 91,278,000. Je, Mhe. Waziri, ni sababu gani ambayo imepelekea kutofikia malengo ambayo yalikadiriwa kufikiwa au chanzo cha mapato hakuna?

Mhe. Mwenyekiti, choyo ni kuona, kuona choyo sio dhambi na mimi naona choyo kwa sababu Halmashauri za wenzangu zimefikia malengo, lakini Halmashauri ya Wilaya ya Kusini haikufikia malengo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, naiomba Halmashauri ya Wilaya ya Kusini iongeze juhudu ya kuingiza mapato ili bajeti ijayo wawe watu wa mwanzo. Katika Wilaya ya Kusini kuna mahoteli mengi ya utalii, je, mapato yanayokusanywa na uwekezaji huo, yanasaidia wananchi wa Wilaya ya Kusini?

Mhe. Mwenyekiti, ushauri wangu kwa kuwa asilimia fulani ya faida inayopatikana ningeomba iwafikie wananchi moja kwa moja, ili waone faida ya uwekezaji. Katika bajeti iliyopita iliwekwa ahadi kufanya mageuzi ya serikali za mitaa, lakini mageuzi haya yanakwenda pole pole, kwa mfano katika kitabu cha waziri kwenye ukurasa wa 91, kuhusu mageuzi ya Serikali za Mitaa, imepewa asilimia ndogo sana ya matumizi, je, mageuzi haya kweli yatafanikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, katika kitabu cha waziri hakuna kiambatanisho cha wafanyakazi waliopata nafasi za kwenda kusoma. Je, Mhe. Waziri, hana mpango wa mafunzo katika wizaa yake?

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono pamoja na wanawake wa Wilaya ya Kusini Unguja kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Asha Abdu Haji. Sasa ni zamu ya Mhe. Salmin Awadh Salmin, baada ya hapo Mhe. Saleh Nassor Juma utafuata na ajitayarishe Mhe. Hassan Hamad Omar.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii na mimi nikazitumia dakika zangu 20, ili kuzungumzia baadhi ya mambo yanayohusu bajeti hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nitumie nafasi hii kumshukuru na kumpongeza Mhe. Waziri wa wizara hii, kwa juhudi zake ambazo anazichukua baada ya kukabidhiwa hivi karibuni wizara nzito yenye mambo mazito. Kwa hivyo, tunamtakia kila la kheri aweze kufanikiwa na kusimamia jambo hili.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sina mambo mengi zaidi, isipokuwa kuna mambo ambayo na mimi niyaongezee nyama kwa wale ambao tayari wameshayazungumza na zaidi ni kwamba ni maeneo ambayo yananigusa.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la mradi wa *ZUSP*, wenzangu tayari wametangulia kusema kina Mhe. Hamza Hassan Juma na Mhe. Ismail Jussa Ladhu. Kwa hivyo, na mimi itakuwa sio vyema kuacha kuuzungumzia na zaidi ukizingatia kwamba mradi huu baadhi ya utekelezaji wake unagusa moja kwa moja wananchi wangu wa Jimbo la Magomeni. Mradi ambao mbali ya ahadi ya Mhe. Rais, lakini na mimi wakati nikipita katika yale maeneo ambayo yanatuama maji, basi nilipata nafasi ya kuwaomba wananchi watuvumilie, watupe kura na katika kipindi hiki maji hayo yataondoshwa kwa kupitia mradi huu ambao ulikuwa una matumaini makubwa, lakini matumaini sasa yameonekana yanafifia.

Mhe. Mwenyekiti, sisi tunapata shida au tunajiuliza sisi hasa Wazanzibari au serikali kwa ujumla juu ya utekelezaji wa hii miradi. Uzoefu unaonesha kwamba tumekuwa sio watekelezaji wazuri wa miradi ya maendeleo ya Taifa, hata ile ambayo tumepatiwa fedha. Wakati mwengine tunakuwa na tatizo la fedha, lakini hata pale tunapopatiwa fedha, basi tunakuwa na matatizo, kuna mifano ya miradi mingi tu ambayo haiendi vizuri. Sasa hatujui kwamba ni tatizo la utaalamu au ni tatizo la uwajibikaji, tunashindwa kufahamu, kwa sababu pale panapokuwa na tatizo la fedha, basi sote tunajua kwamba tatizo ni fedha, lakini hata pale ambapo fedha zipo, basi utekelezaji haupo.

Mhe. Mwenyekiti, mradi huu na Mhe. Waziri, pamoja na kwamba umeridhi, lakini umechukua muda mkubwa. Mradi huu ulikuwa kabla ya Dkt. Shein na Dkt. Shein akaupigia kidedea sana alipoingia madarakani na sisi tukapata nafasi kubwa ya kupigia kidedea, lakini lile jambo la muhimu la mradi ule bado hadi leo halijatekelezwa. Yanayotekelezwa ni yale yale ya gari, sijui vespa na yale mambo madogo madogo, lakini ule uliokusudiwa wenyewe wa mradi huu ambao imechukua fedha nyingi haujatekelezwa hadi leo. Suala la kuondosha maji katika maeneo mbali mbali, yakiwemo maeneo yaliopo katika sehemu ya Magomeni ni suala muhimu sana pamoja na maeneo mengine, lakini hadi leo na mwakani tunakuja katika uchaguzi mwengine, suala lile halijatekelezwa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi siamini kwamba ni tatizo la *World Bank*. Mara nyingi tukizungumza nao wanatuambia, maana yake *World Bank* hawajaweka *no objection*, maana yake tumekuwa tunakimbilia *World Bank, World Bank.* Kumbe utendaji wetu ni mbovu, mimi siamini kama matatizo haya yanasababishwa na *World Bank.* Fedha tayari zimeshakubaliwa na sasa hatari iliyokuwepo, kuna hatari fedha hizi ambazo tulikuwa tumekopeshwa baada ya muda sasa ikawa thamani yake imepungua na yale malengo tuliyokusudia yasiweze kufanikiwa. Kwa kweli Mhe. Waziri, suala hili linatusikitisha sana, linatusikitisha na linatusononesha, kumekuwa na maelezo mengi, ahadi nyingi kila bajeti inayokuja, Mshauri Mwelekezi, Mshauri Mwelekezi.

Mhe. Mwenyekiti, nimejaribu kupitia vitabu hivi vyote vya tokea mwaka 2010/2011, mpaka leo anazungumzwa Mshauri Mwelekezi kutoka Israel hajafika. Sasa mambo haya hayawezi kuvumilika, ni lazima tuhakikishe kwamba jambo hili linaweza kufanikiwa, kwa sababu pesa tayari zipo, kwa nini hakuna uwajibikaji katika masuala haya, tunasingizia *World Bank, World Bank.*Kwa kweli suala hili haliwezi kukubalika hata kidogo. Mimi sisemi kama nitazuwia bajeti ya Mhe. Waziri, lakini nataka wananchi wafahamu na waelewe juu ya utekelezaji mbovu wa jambo hili *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, nataka Mhe. Waziri, atakapokuja kutoa ufafanuzi, hebu atueleze tatizo liko wapi ili lituridhishe, ni kitu gani kilichopo? Kuna nini katika mradi huu? Kwa nini haya maeneo makubwa ambayo ndio muhimu katika mradi huu yameachwa na badala yake yametekelezwa yale mengine? Taarifa tulizokuwa nazo ni kwamba katika utekelezaji wa mradi huu, kumekuwa na safari nyingi za nje, watu wanakwenda nje wakibadilisha, huyu anakwenda huyu anarudi, huyu anakwenda na huyu anarudi, masafari ya nje ni mengi tu na fedha nyingi zinakwenda kwa ajili ya safari za watu mbali mbali, lakini lile jambo muhimu, mbona halitekelezwi, watu wanakwenda safari tu. Utasikia maofisa fulani 15 wamekwenda sehemu fulani na wote wanatumia fedha za mkopo huu kutoka *World Bank*, lile jambo la muhimu halifanywi kwa nini?

Mhe. Mwenyekiti, jengine nilikiangalia hiki kitabu cha Mhe. Waziri, hiki kitabu kinachozungumzia masuala ya miradi hii, kuhusu utekelezaji wa mradi huu ambao unasema kuna Mshauri Mwelekezi. Yametajwa baadhi ya maeneo ambayo yanategemewa kutekelezwa katika mwezi huu wa Julai, lakini kuna eneo moja la Magomeni ambalo tokea mwanzo linazungumzwa, lakini humu halikuorodheshwa. Sasa sijui kama limeshaanza kutolewa au vipi. Uondoshaji wa maji katika wodi ya Magomeni kuunganisha katika Ziwa la Kwa Bitihamrani na kupeleka baharini, ni eneo ambalo tokea mwanzo na ndio maana tuliwaita wananchi wa Magomeni tukawaeleza kwamba serikali ina mpango wa kuyaondosha maji hayo, lakini kwenye kitabu chako hiki eneo hilo halikutajwa. Sasa nimekuwa na mashaka, pengine limeshaanza kutolewa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, uje unieleze Mhe. Waziri, unipe maelezo ya kutosha kwa nini eneo lile ambalo nalo lilikuwa kwenye mpango, lakini kwenye kitabu chako halikuoneshwa, ama kwa bahati mbaya au tupate maelezo ya kutosha juu ya eneo lile, kwa hapa nitakuwa mkaidi. Katika eneo hili la wananchi wa Magomeni ambao tayari tumeshawaahidi, hapo nitakuwa mkaidi, kwa sababu tokea mwanzo wa mradi huu, eneo hili lilikuwa limo, ramani zilikuwa zimeshachorwa na tumeshawaonesha wananchi wa eneo lile kwamba tayari maji haya yataondoshwa, lakini matokeo yake katika kitabu chako cha mwaka huu, eneo hilo halikutajwa kabisa. Kwa hivyo, nitahitaji maelezo ya kina, ili tuone kwamba tunakwenda vizuri katika utaratibu huu. Hilo ni moja.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nije katika Baraza la Manispaa la Zanzibar. Baraza la Manispaa ndio kiyoo cha mji, ambapo watu wengi wamekuwa wakizungumzia usafi, uchafu wa maeneo na mambo mengi yamekuwa yakizungumzwa na kwa sababu ni mji, lakini ninachotaka kusema kwamba mimi nina mashaka juu ya uendeshaji wa taasisi hii na matokeo. Baraza la Manispaa limeundiwa sheria namba 3 ya mwaka 1995, ilipitishwa na Baraza hili la Wawakilishi la Zanzibar, lakini kinachoonekana sasa sheria hizi zimekuwa hazifuatwi. Sasa kutokufuatwa kwa sheria hizi za Manispaa, zinasababisha mambo mengi ambayo sasa kila wakati tunasema uchagu, kuna hivi na hivi, huku ni kutokana na kutofuatwa sheria.

Mhe. Mwenyekiti**,** tuliunda Kamati Teule hapa ya Baraza lako, na kwa bahati nzuri mimi nilikuwa Mwenyekiti, kwa bahati nzuri taasisi ile naijua nje ndani na tulitoa mapendekezo mengi katika kitabu hiki cha ripoti ile tulitoa mapendekezo mengi na tukasema hasa kuna kifungu hapa katika mapendekezo ya ujumla namba 10 inasema ripoti hii ibakie katika maktaba ya Afisi ya Baraza la Wawakilishi, ili iwe rahisi kwa kila mtumiaji wa maktaba hiyo kuipata kwa wepesi, ili wajue haya yaliyopo.

Kwa kweli kuna tatizo la ufuataji wa sheria, tulilazimika kuunda Kamati Teule wakati ule kwa sababu ilionekana Mkurugenzi hafuati sheria na tukatoa maelezo ya kutosha na kwa nini tukasema hivyo tukaelekeza na vifungu vya sheria ambavyo Mkurugenzi anatakiwa afanye. Kwa bahati inaonekana bado tatizo lile katika Manispaa lipo, Mhe. Waziri tunakuomba ulisimamie sana jambo hili, pengine ndio sababu ya kufanya mambo yote haya ambayo yanalalamikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, Sheria Nam. 3 ya mwaka 1995 kifungu cha 4 (2) cha sheria kinazungumzia muundo wa baraza la Manispaa ambapo muundo huo uliotajwa pale katika Baraza la Manispaa, unaeleza kwamba ni pamoja na Meya, Naibu Meya, na Madiwani ndio Baraza la Manispaa. Sasa nadhani wenzetu hawaelewi na ilielezwa kwamba Mkurugenzi pale atakuwa yeye ndio mtendaji wa Baraza la Manispaa, hiyo ndio *composition* ya Baraza la Manispaa.

Sasa kinachooneka ni kwamba wale Madiwani wanaonekana wao si chochote si lolote katika taasisi zile, lakini kumbe kutokuwepo kwao maana yake Baraza la Manispaa halipo kwa mujibu wa Sheria. Pale Darajani ile ni Ofisi ya Baraza la Manispaa lakini Baraza la Manispaa hawapewi nafasi ya kusimamia taasisi ile, hili ni kosa la kisheria.

Isitoshe kifungu cha 5 cha sheria hiyo kinazungumzia kwamba Baraza la Manispaa ni bodi *cooperate*, ni taasisi inayojitegemea na kwa nini tukasema bodi *cooperate* tunataka iweze kuendesha mambo yao bila ya kuingiliwa na mtu yeyote ndio bodi *cooperate*, lakini inaonekana haiko hivyo, tayari Baraza la Manispaa linachukua maelekezo kutoka Wizarani. Kwa nini Mkurugenzi anachukua maelekezo kutoka Wizarani? Anapopitisha maamuzi hawezi kuamua mpaka aende kwenye Wizara, hiyo sio bodi *cooperate* bodi *cooperate* ni taasisi ya kisiasa inayoongozwa na wanasiasa na Mkubwa wao pale ni Waziri kwa sababu ni mwanasiasa mwenzao sio Wizara ni Waziri anayehusika. Ukiangalia hata hiyo sheria yenyewe hapana hata mahala pamoja palipoandikwa *Ministry* ni *Minister*, *minister* ni kwa sababu *minister* Waziri ndio mwanasiasa anayewaongoza wanasiasa wenziwe madiwani ambao

wamechaguliwa katika maeneo yao. Leo inakuwaje kwamba taasisi ile inaongozwa na Wizara, Mkurugenzi anakwenda kupata maelekezo ya Wizara, hawa Madiwani wanafanya kazi gani, hili ndilo tatizo liliopo hapa. Kwa hivyo Mhe, Waziri lazima uhakikieshe hili unalisimamia.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, badala ya lile kwa mujibu wa sheria hii kifungu cha 49 kimezitaja *Committees* za *Council committees* ambazo Madiwani watagawika katika *committees* lakini pia kumetajwa habari ya *departments.*

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa Salmini umebakiwa na dakika mbili.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: ...hapana mimi nimeangalia nimechangia kasorobo, nina dakika sita zimebakia, kwa hivyo Mheshimiwa Mwenyekiti naangalia saa, nina dakika sita.

Mhe. Mwenyekiti: Niombe usiseme hivyo, niombe.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Dakika sita nimeangalia saa mimi nikichangia naaza kuangalia saa, sasa kama unanipunguzia haya lakini dakika zangu ishirini bado dakika sita.

Mhe. Mwenyekiti: Endelea.

Mhe. Salmin Awadha Salmin: Mhe. Mwenyekiti kuna *committees* halafu pia kuna na *departments* ambazo hawa *committees* ndizo zinazoshughulikia masuala yale ya shughuli za kila siku kupitia *departments* zao, Madiwani wanagawika katika *committees* kusimamia shughuli zile lakini inaonekana sasa hivi masuala hayo hayapo, kumekuwa na vurugu. Kwa hivyo Mhe. Waziri usimamie hili, uhakikishe kwamba sheria hii Nam. 3 ya mwaka 1995 inafuatwa tuwaachie madiwani wafanye kazi zao, wajigawe katika *committees* katika Idara ili kuona wanasimamia maamuzi yao.

Nilikuwa nikikisoma kitabu hiki cha Mhe. Waziri, kitabu cha pili kimeeleza humu kimeeleza vizuri sana, nimesoma pahala inasema kwamba Madiwani ndio wenye maamuzi katika taasisi yao. Hiyo *statement* kumbe ni maelezo tu, utekelezaji hamna. Imo humu *statement* ya Waziri kasema ukisoma na nimesoma, mimi nimeona sasa atuwaachie madiwani wafanya kazi zao, watakapokosea tupate fursa ya kuwalaumu, ile sio Idara ya Serikali na kama tunataka iwe Idara ya Serikali basi sheria anayokuja nayo Mhe. Waziri hapa atwambie Mhe. Waziri sasa Manispaa ni Idara ya Serikali.

Kwa sababu sheria inasema kwamba Rais atamteua Mkurugenzi kwa mujibu wa sheria na Mkurugenzi huyo atawajibika kwa Baraza la Manispaa ndio sheria inavyosema, Baraza la Manispaa limetwajwa hapa kwamba ni fulani na fulani lakini nimeambiwa ni *body cooperate*, sasa hawa tutakapowaingilia ingilia katika shughuli zao, maana yake tunakosea. Tutalalamika mji mchafu, kwa sababu hatuwapi fursa zao za kufanya kwa mujibu wa sheria. Sheria hii inaelekeza vizuri lakini inaonekana inashinda, kwa hivyo nimuombe sana kama Mkurugenzi yupo na Mhe. Waziri tujaribu kufuata sheria, tukifuata sheria iliyopo tunaweza kupata mafanikiyo kwa sababu sheria hii imepitishwa na kwa malengo.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, jambo ambalo ni tatizo kifungu cha 23 cha sheria hii Nam. 3 kinazungumzia juu ya kuundwa *standing committee* ambayo shughuli yake itakuwa ni kusimamia matumizi kila mwaka. Manispaa inatakiwa iunde kamati ambayo itakuwa kazi yake ni ku-*control* matumizi wao ndio watakuwa wanatoa taarifa za matumizi sasa kamati hiyo Mhe. Waziri atakapokuja hapa nataka anambie ipo haipo, imeundwa haijaundwa na kama haijaundwa kwa nini na sheria hii inaelekeza kwamba kuwe na *standing committee* hii ambayo kazi yake ni ku- *log late fines* fedha zile ili zionekane zinatumika kwa kadiri zilivyopangwa katika bajeti, lakini hili linaonekana halipo.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie muda wangu wa dakika sita.

Mhe. Mwenyekiti: Umebakiza dakika tatu Mheshimiwa.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Nazimalizia Mhe. Mwenyekiti, zinatosha mimi nataka kuzungumzia suala la maslahi ya askari wa vikosi. Hili Mhe. Mwenyekiti tumekuwa tukilisema sana kwamba askari wetu wa vikosi vya SMZ bado

hatujawapa maslahi yanayostahiki ya kiaskari. Tumekuwa tukiwa-*treat* kama wafanyakazi wa Serikali, wengine tumekuwa na vipimo vya kuwafanya kama wafanyakazi wa kawaida. Kazi ya uaskari ni kazi nzito si kitu cha mas-hara lazima wawe ni tofauti na wengine, wanafanya kazi kubwa bahati nzuri na mimi mwenyewe nilikuwa ni askari najua. Hebu angalieni wenzetu wanafanya nini kule pamoja na ufinyu wetu wa bajeti, hivi tunawalipa askari mishahara yao sawa sawa na raia! Kazi ya askari ni kazi nzito, kazi ya kulinda nchi ni kazi nzito na hili tumekuwa tukilisema kila siku, jamani hebu Serikali iangalie maslahi ya askari wetu wa vikosi, kila siku wanalalamika.

Mbali na mambo mengine ambayo yanafanywa katika vikosi lakini Serikali lazima iangalie na hili tutaendelea kulisema, nasema mpaka tuhakikishe kwamba linarekebishwa maslahi ya askari wetu wa vikosi yamekuwa madogo mno yanasikitisha, na wala tusiwalinganishe pamoja na *scheme of service* inayozungumzwa kwamba kila siku *scheme of service* lakini hakuna utekelezaji wowote. Kwa hivyo hili Mhe. Waziri na naamini wewe utaliweza, lisimamie na uhakikishe kwamba kuna maaskari wetu wanapata maslahi ambayo ni afadhali, ili na wao waweze kufanya shughuli zao mapema.

La mwisho Mhe. Mwenyekiti, suala la mazingira na Tawala za Mikoa, tuwaombe sana wenzetu Serikali; Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya watusaidie katika suala zima la mazingira, utunzaji wa mazingira hali yetu ya mazingira sio nzuri pamoja na kwamba kuna Wizara inayoshughulikia mazingira lakini hawa hawawezi kufanikiwa kama wakuu wa Wilaya na Mikoa ambao uchafuzi wenyewe unafanyika katika maeneo yao hawatoshirikiana na taasisi hii katika kukabiliana na mazingira.

Tunapozungumzia uchimbaji wa mchanga, ukataji wa miti na mambo mengine yote yanafanyika katika Wilaya zetu na Mikoa yetu. Sasa kama hatutotoa ushirikiano wa kutosha katika maeneo yetu nchi hii itaangamia kimazingira, kwa hivyo tuwaombe sana wakuu wa Mikoa mambo haya yanapofanyika yanafanyika katika Mikoa yao, katika Wilaya zao na wanayaona na wanashindwa kuyazuia. Nchi hii itaangamia katika masuala ya mazingira, kisiwa hiki kinakwenda zake, na viongozi wetu hawa wasipoweza kushiriki katika jambo hili la uchafuzi wa Mazingira itakuwa inasikitisha.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti, mimi naunga mkono hotuba hii na Mhe. Waziri naamini yale niliyomuuliza atanipatia majibu, ili bajeti yetu hii iende vizuri. Ahsante nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutusaidia na kutujaalia kuwa hai na kuweza kuingia katika jengo hili na kuendelea kupumua hadi sasa. Hii ni hazina kubwa aliyotujaalia Allah na kwa vyovyote vile hatuna budi kumshukuru.

Nadhani Mhe. Mwenyekiti, nitakuwa mchache wa shukurani kama sikutumia fursa hii kwanza kukushukuru wewe kwa kunipatia fursa hii, halafu kumpongeza Mhe. Waziri kwa jinsi alivyokuja na hii hotuba yake ya bajeti na jinsi alivyoitiririsha vizuri. Kwa kweli watu wengi humu tumefahamu dhamira ya bajeti yako, tafsiri na vile ulivyotafsiri juzi wakati nachangia ulipodhani kwamba nimewaambia Watumbatu kwamba wao kazi ya kupanda majani, wao sikuwataja katika mambo ya utaalam. Kwa kweli Watumbatu wanaweza kweli bila ya kuwezeshwa. Mimi hawa ni shemeji zangu, sithubutu kuwakera, kwa vile mnaweza, nafurahia sana kuwa nanyi.

Mhe. Mwenyekiti sasa niende katika hoja nianze na ukurasa wa 88 wa hiki kitabu. Kuna jaduweli hapa katika ukurasa wa 88 ameongelea mapato ya Serikali za Mitaa. Niangalie katika hili Baraza la Mji wangu wa Chake Chake; Baraza la Mji wangu wa Chake Chake katika kutafuta mapato kwa mwaka 2013/14 lilikadiria kukusanya milioni 500, na makadirio yalikuwa katika robo ya tatu, yalikuwa yawe 79,084,6000. Lakini katika robo ya tatu tu jamaa zangu wa Baraza la Mji Chake Chake; mji ninaotoka wameweza kukusanya 117,391,500 kwa hivyo wamevuka lengo na kufikia asilimia 136.

Kwa niaba yangu na kwa niaba ya wapiga kura wa Jimbo la Wawi napenda nitumie fursa hii kuwapongeza hawa jamaa wa Baraza la Mji la Chake Chake , kwa kweli Mhe. Mwenyekiti makadirio wamevuka lengo sambamba na matumizi maana wamesema wangetumia milioni 79,084,600 lakini wametumia milioni 180,000 sawa sawa na asilimia 127, sasa matumizi yamevuka lengo mapato yamepunguka lengo.

Mhe.Mwenyekiti lazima tujue mji wa Chake Chake ni miongoni mwa miji muhimu sana katika visiwa hivi vya Unguja na Pemba. Mji wa Chake Chake wataalam tunauwita *it is a connective rank* katika kisiwa kile cha Pemba ni

kiungo baina ya wale wanaotoka Mkoani wakaenda Wete, wanaotoka Wete wakaja Mkoani kwa kusafiri na wanaotoka Unguja wakaja katika maeneo mbali mbali ya Pemba, lazima wafike Chake Chake kupitia *airport* pale Mheshimiwa, huu ni mji muhimu. Kama mji huu ni muhimu unatakiwa upate viongozi makini mahiri, waadilifu na ambao wanafanya kazi za kutukuka sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti katika kisiwa cha Pemba ule ndio uso wa kisiwa cha Pemba. Kwa hivyo unapatikana kila wakati, mtu akikuangalia tu hakuangalii mguuni anakuangalia usoni. Kwa hivyo lazima ukitokeza tu uso uwe safi wakati wowote. Sasa pamoja na mapato yote haya, pamoja na matumizi yote yaliyofanywa na Baraza la Mji inaonekana Baraza la Mji hawana umakini wa Baraza la Mji wa Chake Chake, katika kutumia mapato wanayoyakusanya kwa kushindwa kuweka vipaumbele.

Mhe. Mwenyekiti, inasikitisha sana kuona hadi leo hii katika Mji wa Chake Chake hauna *stand* ya dala dala. Sisi hapa ni tofauti sana na nchi nyengine kama kule Oman wao hawana *public passport* lakini sisi hapa tuna-*public transport*, pale Pemba lazima upande dala dala, ukishapanda dala dala unahitaji dala dala ipate *stand.*

Leo madereva wa dala dala pale Pemba wamekuwa kama paka na watoto wake leo anawachukua anaweka hapa, kesho anawachukua anawaweka pale, keshokutwa anawachukua anawaweka pale, ni tatizo watu wanalipa kodi na tumeiona humu sioni sababu ya kuona mji mzuri na ulipo kati kati kama wa Chake Chake unakosa *stand*. Hili ni tatizo wana-*park park* tu pembezoni mwa barabara.

Hivi juzi wakati nataka kusafiri nilikuwa nakwenda kununua halua hapa kwenye kituo cha mafuta Chake Chake chini ya Muembe pale, sasa natokeza hivi kumbe ndio wameweka *park* pale barabarani, basi mimi pale nilikwaruzwa na *sight mirror* ya dala dala mpaka leo bega linaniuma Mheshimiwa. Sasa ikiwa mimi muwakilishi ninayejulikana nakwaruzwa na *sight mirror* je, mkulima wa nyanya anayetoka Vitongoji kule akiwa na tenga lake, hili ni tatizo.

Sasa nataka Waziri unieleze una mpango gani endelevu kwa kushirikiana na Baraza lako hili; mpango wa muda mfupi na wa muda mrefu sio muje hapa mutuchapie chapie maneno tu, tunataka maneno yaende na vitendo, watu wanalipa kodi. Leo mlipa kodi anakuja kuuza nyanya kesho anaparurwa na vioo vya dala dala kwa sababu hamna *stand*. Kama hamuwezi kujenga msiwatoze kodi madereva wetu.

Mhe. Mwenyekiti, kama kuna watu wanaobughudhiwa katika Baraza la Mji wa Chake Chake ni madereva wa daladala, ukifunga *brake* tu ameshakuja na risiti yake, umpe shilingi mia tano, leo mnawakata kodi hamuwawekei *stand*, inakuwaje jasho lao haliwarudii huu ni unyonyaji, mimi ninakuomba Mhe. Waziri tangu tuingie humu tunazungumzia *stand, stand, stand* na ukija unachapa maneno,. Nataka unieleze hivi huu mradi wa kujenga *stand* katika mji mkubwa wa Pemba yaani Chake Chake utaanza lini? That is (a).

Mheshimiwa (b) katika hili Baraza letu la Mji wa Chake Chake kuna soko linaitwa Qatar ni miongoni mwa masoko makubwa yaliyo Kusini mwa Jangwa la Sahara. Bahati mbaya linaongoza kwa uchafu Mheshimiwa pamoja na kodi yote ile inayokusanywa, hapana vyoo, juzi nilishikwa na mkoja, samahani Mheshimiwa kwa lugha chafu. Juzi nilitaka kwenda haja nafuta yale maneno niliyoyasema hapo nyuma, ikabidi nipige mbio hospitali ya Chake Chake nikaombe choo cha wagonjwa, hili ni tatizo kubwa sana. Ikiwa makusanyo kama yale mumeshindwa kuweka *public toilets* basi waruhusuni watu waweke *private toilets* ili watu walipe japo shilingi mia moja muwape sehemu watu wawekeze. Nyinyi hamna uwezo eti, musiwe kama vile joka la mdimu. Joka la mdimu halili ndimu lakini akenda binaadamu anataka amtafune. Hamna uwezo wa kujenga pale wapeni wawekezaji wajenge vyoo kusudi. Mhe. Mwenyekiti kuna wateja pale wanatoka Mombasa katika soko la Qatar pale, kuna wateja wanatoka Tanga, hata Wataliana nawaona pale siku nyengine wanakuja kufanya *shoping*, sasa akibanwa na haja ende wapi?

Mheshimiwa Baraza la Mji mnieleze mtajenga lini vyoo, ikiwa hamna uwezo wa kujenga hivi vyoo mnambie ni lini mtampa muekezaji kama hamna tutawapatia muekezaji humu humu ndani. Mheshimiwa kama umepita kwa siku za karibuni katika soko la Qatar na gari mbovu mbovu hivi basi lazima utafute *bulldozer* lije likuinue kwa sababu kuna matope pale, hizi siku za mvua na mashimo kadhaa pale karibu na soko.

Sasa Mheshimiwa mimi nataka aniambie huyu Waziri mashimo, matope pamoja na mashaka mashaka yale ya matungule mabovu mabovu yaliyochawanyika pale ni kwa sababu ana upungufu wa watumishi wa Baraza la Mji au

ni khulka ya uchafu tuliyonayo wazanzibari? Ikiwa ni watumishi basi wewe ndio muajiri unaetoa ajira hicho kitengo cha ajira, sie kumbe ni Mwalim Haroun. Mwambie jirani yako Mwalim Haroun hapo akuajirie watu wa Baraza la Mji ikiwa huna watumishi. Lakini kama ni khulka ya uchafu waliyonayo wafanyakazi wako basi hawa hawafai kufanyakazi, watafutie maarifa mengine Mheshimiwa lakini kwa Baraza pale wanatuua kwa magonjwa.

Mheshimiwa niendelee Mkoa wa Kusini Pemba. Hapo Mkoa huu ni katika mkoa ambao muhimu sana katika nchi hii na tumebahatika katika Mkoa wetu tunaongozwa na Meja Mstaafu wa Jeshi la Wananchi kama mtatupa jicho juu mtamuona kama yupo na yuko makini sana, sio tu katika kufanya kazi lakini hata katika kusimamia kazi Meja Tindwa. *(Makofi)*.

Sasa Mheshimiwa nilidhamia Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa kwa sababu inaongozwa na Meja Mstaafu wa Jeshi la Wananchi ingekuwa makini lakini napata wasiwasi sasa Mheshimiwa. Napata wasiwasi kwamba Kamati yetu ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa ina mapungufu kutokana na kuongezeka kwa vitendo vya uhalifu katika Mkoa wetu. Mheshimiwa vitendo hivi vinatisha hasa katika Wilaya ya Chake Chake.

Mheshimiwa kwa mfano matukio ya uvunjifu wa amani yaliyofanyika katika Mkoa wetu katika kipindi cha karibuni kuna kijana mmoja mbichi juzi juzi hivi katika eneo la Machomane aliuwawa na akakutikana maiti yake imetelekezwa tu hivi, sidhani kama mwezi unatimia tena tukio jengine la uhalifu kijana mwengine mdogo sana aliuliwa na maiti yake ikatelekezwa katika eneo la matrekta hapa karibu na msikiti wa kadiria.

Kama haitoshi kuna kijana mmoja pale ni mteja mmoja anaitwa Faridi kenda kunajisi msahafu kama miezi 6 iliyopita katika eneo la Wawi pale kwa kuutia sijui mikojo si lugha nzuri lakini aliutia najisi msahafu.

Sasa Mheshimwa inasikitisha sana, ninasikitika sana kwamba mambo haya yanatokea na tunayo Kamati ya Ulinzi na Usalama inayoongozwa na Meja Mstaafu, mambo mabaya kama haya yanatokea. Namuomba Meja sasa awe makini sana hii ni hatari, sasa tuangalie tatizo liko wapi? Tatizo ni Kamati ya Ulinzi na Usalama haiko makini au tatizo ni nini? Naomba mnisikilize kidogo Mhe. Mwenyekiti, pamoja na waheshimiwa wajumbe.

Katika miaka ya 1970 mimi wakati niko *Advanced level* pale *Fidel Castro* ilikuwa ninakuja *cinema* pamoja na *disco competition* hapo hapo *Starling Mace*, siku hizo ni kijana mdogo mbichi, ilikuwa nakuja hapa kwa miguu saa saba usiku naondoka *Starling Mace* kuelekea *Fidel Castro* sio sasa nimezeeka. Mheshimiwa nilikuwa sipati tatizo lolote na ilikuwa naondoka pale peke yangu saa saba mpaka nafika *Castro* siguswi hata na mbu lakini pale siku zile ilikuwa hakuna mabaa ya pombe. Lakini sasa hivi Mheshimiwa kuna baa tatu katika maeneo ya karibu pale, kuna ile *Starling Mace* ya Jeshi, kuna *Mace* ya JKU pale pale Kisunzi na kuna *Mace* moja inaitwa *mortuary*. Hiyo *mortuary* ndio hatari huko.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Saleh umebakisha dakika 2 malizia.

Mhe. Saleh Nassor Juma: ...dakika tano, sasa Mheshimiwa, mimi nadhani ongezeko la mabaa katika Wilaya yetu ya Chake Chake ni tatizo na naomba sana Mheshimiwa Kamanda huyu wetu Mstaafu wa Jeshi afanye kazi kubwa na Kamati yake ya Ulinzi ili aweze zile Baa kuzidhibiti ili kupunguza mauaji. Mimi naamini Kamati yake iko makini sana lakini tatizo ni zile baa, zinatuletea vibaka, walevi ni tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye vikosi. Kwanza katika kitu ninachopenda kukupongeza na msinishangae zamani nilikuwa navichukia sana hivi vikosi, sasa nasema hivi vikosi vina maana sana na mtu yeyote atakaejaribu kuvisema vibaya hivi vikosi huyo mimi ni adui wangu wa mwanzo kabisa. Hawa wanaoanza kusema kwamba kwa nini majeshi sijui wana jeshi lao, hawa si ndugu zetu wa damu hawa ni wabaya wetu hawa.

Mimi ninamuomba Mhe. Rais ikiwa atahitaji kuunda kikosi chengine kuongezea nguvu hawa aunde na tuko pamoja nae. Kinachonisikitisha Mheshimiwa hawa vijana hatuwawezeshi hawa wanafanya kuliko Polisi, wanafanya kazi kuliko jeshi hebu tuangalieni kipindi cha maafa. Hawa ni wafanyakazi katika uokozi, JKU, KVZ, KMKM, Mafunzo wanashirikiana katika uokozi na wanalipwa shilingi laki moja na hamsini, laki mbili *sham!* Mhe. Waziri wasaidie. Hebu angalia Mheshimiwa hata vifaa hawana, kwa mfano hivi yakitokea maafa tunategemea KMKM wasaidie, leo KMKM hawana *diving chamber* kama atazama *diver* kule akirudi hana chombo cha kumsaidia kupata pumzi anakufa, lazima tuwatafutie *diving chamber*, tuwatafutie *diving suit* na mambo mengine.

Mheshimiwa tuwaangalie hawa vijana wetu wa JKU na KVZ hawa wanajitahidi vile vile, siku zote nikiamka mimi kwenda mazoezi wao alfajiri wanaamka kulinda maofisi, kulinda majumba ya viongozi wetu na kulinda usalama wetu, leo wanalipwa pesa mbovu sana, nakuomba mafao yao yaongezwe.

Tuangalie Mafunzo hawa, Mafunzo hivi sasa wanafanya kazi nzuri kule jela niulizeni mimi nimeshawahi kwenda jela, zamani ilikuwa tunatumia Mtondoo lakini sasa mule jela mna vyoo vya bure bure ndani jamani, dogo hilo. Ninampongeza Kamishna na Makamanda wote. Nampongeza Kamishna wa Mafunzo, nampongeza Komodoo, nawapongeza wana kamanda wote hao, wanafanya kazi nzuri wapatieni mafao hao.

Juzi Mhe. Mwenyekiti, nimalizie na hawa Mafunzo. Hawa Mafunzo juzi walinileta boga niliomba kipindi cha Ramadhan ile iliyopita, sampuli wanazozalisha maboga, nimetembea katika nchi nyingi zilizoko Kusini mwa Jangwa la Sahara na zile zilizopo UAE na hata juzi juzi nilikuwepo China nikala maboga, lakini boga nililolila kutoka Mafunzo sijapata kuliona kwa utamu wake, tuwawezeshe hawa. Ahsante. *(Makofi).*

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti, na mimi ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuwasilisha hotuba yake kwa muda mfupi kitaalam, ninampongeza sana. Lakini vile vile nisiwe mwizi wa fadhila, nimpongeze aliyemuachia urithi Mhe. Mwinyihaji Makame kwa kazi nzuri aliyoifanya, naomba afuate nyayo zake.

Mimi la kwanza leo katika kuzungumza ni katika ukurasa wa 16 Idara ya Usajili na Kadi za Utambulisho. Mhe. Mwenyekiti, nampongeza sana Mkurugenzi wa Idara hii kwa kweli kajitahidi kufanya kazi nzuri lakini bado changamoto zipo nyingi sana. Mwaka jana tunakumbuka sote hapa Waziri akiwa Mzee wetu Mwinyihaji Makame tulifutana nae na tukafanya mkutano mzuri sana pale Benjamin Mkapa Wete, watu wengi walishiriki walioalikwa, wakiwemo Waheshimiwa Wawakilishi, Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya, Madiwani, Masheha na kufahamisha namna ya kuwapa watu haki zao za kupata vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini inasikitiha sana na inatia aibu sana kuwa mpaka leo changamoto bado zipo kwa baadhi kwa masheha. Nadhani Waziri tuliyempata ni Waziri Kijana atazidi kufatilia jambo hili. Mheshimiwa kama inavyozungumza sheria kama mzanzibari anayetimiza umri wa miaka 18 ana haki ya kupata kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi, awe mzanzibari na sehemu yake awe anakaa katika makaazi yake. Lakini tunajua historia kwamba wazee wa zamani wetu waliotangulia walikuwa hawana vyeti vya kuzaliwa lakini hawa imekuwa kikwazo kwao kupata kitambulisho hiki cha Mzanzibari Mkaazi.

Nitoe mfano ulio hai ndani ya jimbo langu tena Kisiwani Kojani. Mimi hivi unavyoniona nina umri wa miaka 52 nimezaliwa mwaka 1962. Lakini kuna baba mkwe wangu niliyemuolea mwanawe hata dago lile dago la wakojani hajawi kwenda yupo pale Kisiwani Kojani, kapata msafara tu wa kwenda kumjulia mwanawe Dar es Salaam yeye na mke wake, kwa sababu alikuwa anaumwa. Mwaka 1965 kapiga kura, 2000 kapiga kura, 2005 kapiga kura mpaka 2010 kanyimwa kupata kitambulisho. Hawa ikumbukwe kama ni wale waliotobolewa vipande vyao pale kilimo, waliitwa siku moja pale, vipande vile vya zamani vikatobolewa hapa na mpaka leo hajapata ufumbuzi. Ninamuomba Mhe. Waziri pamoja na Mkurugenzi afuatilie kuwapa haki zao.

Kwa sababu ni wazaliwa, wametimiza umri tatizo hana cheti lakini hizo taratibu nyengine wamezitimiza, kwa hivyo unaambiwa kama ukiwa na umri wa miaka18 unapata kitambulisho, mtu ana zaidi ya miaka 70 yuko pale pale Kisiwani. Leo ananyimwa kitambulisho, Mhe. Waziri ukiwataka hawa nitakuletea mkononi.

Sasa mimi ninapata shida kweli kweli kuna tatizo gani na sheria inasema hivyo. Jambo la kusikitisha waliokuwa si wazalendo wa nchi hii *wallahi* wanatucheka, wanakwambia wewe mzanzibari nipe kadi yako ya utambulisho, wapo tushakutana nao ndani ya mahoteli wakitwambia hali kama hizo na sehemu nyengine mbali mbali. Sasa Mheshimiwa kwa sababu mtu wa kisiwa mwenzangu wa Tumbatu na mimi mtu wa kisiwa cha Kojani, suala hilo ulifuatilie kwa kina ili shughuli iende vizuri.

Hii haki ya utambulisho ni haki ya kila mzanzibari, sasa hivi ukiwa huna kitambulisho kile ajira hupati. Kama huna kitambulishe kile tiketi unanyimwa. Sasa itakuwaje watu wale wasipate haki zao za msingi, nadhani Mheshimiwa huyu atafuatilia kwa kina.

Mheshimiwa nikiendelea na mchango wangu nikitoka hapo niende katika Baraza la Manispaa Mkoa Mjini Magharibi, katika *stand* ya Darajani iliyoondolewa na ikawekwa pale Kisiwandui na sehemu nyengine kama Baraza la Wawakilishi la zamani. Mheshimiwa hapa pana matatizo makubwa sana, ukiangalia kwa kina na mimi nakuomba utembelee uzione shinda watu wanazozipata. Mheshimiwa imekuwa ni adha kubwa sana kwa wapita njia na wengine wanaopita na gari zao. Kwa sababu hata kuwa wamewekwa kwa muda lakini utaratibu haufuatwi.

Mimi nashangaa askari wa Usalama Barabarani wako pale pale lakini unakuta gari zina-*park* jinsi wanavyopenda na askari yupo hapo hapo, kuna nini? Hebu Mhe. Waziri tueleze siku moja tena utembee kwa miguu uone zile shughuli lakini ukipita njia za kati pale hupiti utaona kadhia tunazozizungumza sisi si kweli, lakini *wallahi* pita.

Leo nimejaaliwa na Mwenyezi Mungu kutoka Baraza la Wawakilishi, nimesali katika msikiti wa Kisiwandui pale. Kutoka msikitini pale ninakuja zangu sehemu za *garden* barabara imejaa, nafasi haina kuna watoto wako katika sehemu za taa zile watoto wawili wadogo, *wallahi* kuna pikipiki au vespa imetoka na *speed* huko katika njia hiyo iliyokuwa siyo halali kasoro kidogo awachukue watoto wadogo wawili wa umri wa miaka sita na miaka minne.

Mhe. Mwenyekiti, ni hatari na wafanyabiashara nao wameshajisogeza pale, ukienda pale pana *Carry* zinasababisha vurugu nazo, panauzwa machungwa, panauzwa mahindi na shughuli nyengine kadhaa zinazofuata pale, hebu Mheshimiwa tembelea pale.

Katika kadhia hii kana kwamba haitoshi bado kuna *parking* pale kuelekea katika benki ya FBME pale pana *parking* lakini *wallahi* daladala utakwenda kuzikuta zime-*park* pale tena zime-park ovyo na askari wako pale pale, hili ni jambo la aibu na fedheha. Mhe. Mwenyekiti, ukitaka kutengeneza mji utengeneze katika mazingira mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, nikamuuliza yule anayechukua kodi pale, nikamuuliza hawa daladala wanalipia, akaniambia pale Mstahiki Meya amesema wasilipie, lakini hapa hawaruhusiwi ku-*park, wallahi* Mheshimiwa pale tembelea ukaone habari ilivyo. Pale, gari za kawaida zinazo-*park* hazina nafasi na ukipita ile njia wanaikabasa inakuwa taratibu zote zinakiukwa. Mheshimiwa tunaomba adha ile utuondolee.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu tumeambiwa kituo kile ni cha muda basi tunaomba huo muda ujuilikane, unaweza ukaambiwa cha muda ikafika hiyo 2015 hapajaondokwa pale, itakuwa si muda tena ni pakudumu pale. Lakini *wallahi* Mhe. Waziri ufanye kazi kubwa kutafuta maeneo mengine, hasa nyie viongozi wa Chama cha Mapinduzi kwani pana ofisi kuu ile ya Chama cha Mapinduzi, si vizuri kwani wanakuja viongozi mbali mbali wa kitaifa pale. Mhe. Mwenyekiti, bado wamekwenda kuijengea wigo mbaya mimi, naomba jambo lile litekelezwe mara moja kwa kufanya ufanisi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo nielekee Baraza la Mji la Wete. Mheshimiwa Baraza la Mji Wete ni sehemu ambayo ina wafanyabiashara wengi na watu wanatembelea katika maeneo yale, ukiliangalia soko la Wete ni la siku nyingi na ni kongwe lakini chakavu na chafu sana. Hii siyo siri ni chafu kupita kiasi ndani na nje, hebu jamani angalieni kwa jicho la huruma hili soko ni la siku nyingi, hata siku moja halijafanyiwa ukarabati. Mhe. Mwenyekiti, naomba mliangalie kwa jicho la huruma.

Mhe. Mwenyekiti, tuliambiwa *stand* ile itajengwa kiwango cha lami kama wenzetu mfano pale Darajani, lakini *wallahi* mpaka leo. Pale eneo ni zuri sana na ni kubwa likijengwa na kuwekwa katika mazingira mazuri basi patapendeza, itakuwa mji wa Wete umependeza. Tuliangalie kwa jicho la huruma lile soko na mandhari yake ya nje yote tukifanya hivyo itakuwa tumefanya shughuli kubwa ya maendeleo.

Mhe. Waziri kuna tetesi pale kama kuna mvutano kati ya wafanyabiashara na Baraza la Mji na Bwana mmoja anaitwa Mapete, naomba hilo suala nasema ni tetesi lifuatilie na kuna mgogoro mkubwa kwani unapunguza shughuli za maendeleo. Mhe. Mwenyekiti, huyu bwana anasema hilo eneo ni lake, kwa hiyo tetesi hiyo ifuatilie kufanya uchunguzi wa kina na ukigundua ulifanyie kazi, lakini huo mvutano upo na unarudisha nyumba maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia barabara iliyojengwa selemu ya pale na hapa Kilimandege pamejengwa kiholela sana, maji machafu yamerundikana ambayo ni mazalia ya mbu, hebu piteni muangalie pale kama kweli mnataka kuufanya mji uwe safi na uwe wa kuvutia.

Mwaka jana vile vile tulizungumza kuwa taa za Mjini Wete na Chake chake haziwaki, Mhe. Mwinyihaji Makame alitwambia na mradi huu ulioko huku Unguja wa zile taa za mjini na kule utafika lakini mpaka leo hatujaona chochote kinachoendelea. Kule wananchi nao wanataka wapendeze wakitembea barabarani wakishapata rizki yao ya mihogo wanajisikia kidogo, wawe wanapita barabara kwa mikogo na barabara zinang'aa, lakini *wallahi* ukifika usiku giza tupu kunatisha. Hapo ukikutana na watu wabaya msalie Mtume.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni kwamba Wilaya ya Wete kumezuka wizi mbaya sana; kuna wizi wa kuiba baiskeli na televisheni katika majumba ya watu. Namuomba Mheshimiwa uliangalie kwa kina ulinzi uzidishe. Kuna Mheshimiwa alizungumza sana ulinzi wa hawa polisi jamii, basi vikundi vile kama vipo viimarishwe ili kuweza kulinda wananchi wetu wasipate hatia.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho na mimi nivipongeze vikosi vyote vya SMZ; hawa wanafanya kazi nzuri sana kwani ni walinzi wetu wanaotulinda raia na mali zao usiku na mchana. Kwa hivyo, hawa ni wakuongezwa posho la mazingira magumu siyo mbaya na halafu mishahara yao kuongezwa, siyo vibaya kwani wana kazi nzito.

Mhe. Mwenyekiti, ukizingatia kama nchi yetu ni ya visiwa tunamuomba Mwenyezi Mungu atuepushie mbali lakini mara kwa mara tunapata maafa ambayo huwa hatuyategemei. Lakini ukiangalia hivyo vikosi kama kikosi cha KMKM basi hata hizo zana za kwenda kuokolea hawana. Sasa mimi naomba mambo haya yasiishie katika vitabu hivi, wafanyiwe ufanisi mzuri wa kupata zana ili waweze kufanya kazi kwani wana uwezo vijana hawa.

Mhe. Mwenyekiti, hata ukiangalia katika jimbo langu pale kituo cha KMKM Kojani tunao muda mrefu tangu bado mdogo nasoma mpaka leo tunao na tunaishi nao vizuri na wanafanya kazi nzuri kwa kushirikiana na wananchi na mpaka leo haijatokea hitilafu yoyote, tunawashukuru sana na tunawaomba waendelee kushirikiana na wananchi ndiyo wanapata mambo mazuri yakufanya ulinzi.

Mhe. Mwenyekiti, mengi yapo lakini kwa kuokoa muda wako nasema nashukuru na nimuombe waziri atakapokuja hapa haya niliyomueleza anipe ufafanuzi wa kina kabisa, kwa sababu ni mambo yanayohusu na sisi ni wawakilishi wa wananchi wakisikia wenyewe huko watajua kama kweli mambo yetu yamezungumzwa. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti nakushukuru sana naomba nikae na mimi nitaunga mkono baada yakwishakupata majibu ya hoja zangu nilizozitoa. Ahsante sana.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nakushukuru kwa kunipatia nafasi yakuweza kutoa mchango wangu katika hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nachukua nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii yakuweza kutoa mchango, lakini la pili nataka nichukue nafasi hii ya kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kazi nzuri ambayo wametuletea pamoja na mashirikiano mazuri waliyokuwa nayo baina yao na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala.

La tatu nataka vile vile nichukue nafasi hii yakuwapongeza Halmashauri za Wilaya ya Kusini pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuleta makusanyo ya hali ya juu kabisa ukilinganisha na Wilaya nyengine. Pia nataka nichukue nafasi hii kwa hizi wilaya zilizobakia, najua hii ni kazi nzuri wameifanya na wao na naamini kipindi kilichobakia wataweza kufanya vizuri zaidi. Najua hii ni kwa sababu ya mikakati ya Mhe. Waziri ambayo anaiweka kwa watendaji wake, bila shaka waziri anafanya kazi kubwa sana ya kuweka *strategies* maalum za kiutendaji. Pia nashukuru kwa hilo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nichangie mwanzo kwenye sera na kanuni za Serikali za Mitaa. Mheshimiwa taasisi zetu zinahitaji miongozo ambayo miongozo hii itaweza kusaidia kutekeleza mipango yao ya maendeleo, yaani kuwepo kwa sera na kanuni za Serikali za Mitaa ni jambo la msingi kabisa. Kwani mipango itakayopangwa kwa wananchi itatekelezwa bila ya vikwazo, hivyo ni jambo la kufurahisha, kwa hiyo nampongeza tena Mhe. Waziri kwa kuleta mswada wa dharura wa marekebisho ya sheria, ambao ni Mswada wa Sheria ya Tawala za Mikoa, Mswada

wa Sheria ya Serikali za Mitaa na Mswada wa Sheria wa Kuanzisha Sheria ya Ulinzi wa JKU. Hili ni jambo zuri sana na nampongeza Mhe. Waziri kwa kutuletea mambo haya.

Mambo haya yakifika kwetu sisi itakuwa ni mazuri kwa sababu tunategemea kwamba sheria hizi zitapunguza malalamiko, kwa sababu kulikuwa na malalamiko mengi katika sheria zetu. Kwa hivyo, moja itapunguza malalamiko na la pili ile migongano ya tafsiri za kisheria. Nafikiri hili suala likija migongano itakuwa hakuna tena, wala malalamiko itakuwa hakuna. Pia makusanyo yatakayopatikana kila mtu atajua sehemu yake; mimi nakusanya wapi na yule anakusanya sehemu gani. Kipindi kilichopita ilikuwa watu wanalalamika kwamba huyu anakusanya ambayo ilikuwa ni yetu sisi.

Jengine ambalo wakati tulipata nafasi Mhe. Mwenyekiti, tulitembelea Halmashauri tatu. Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "A", Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "B" na Halmashauri ya Wilaya ya Kati. Mhe. Mwenyekiti, changamoto ambazo zilijitokeza katika Halmashauri hizi ni ufinyu wa bajeti; hilo halitaki tochi ni kweli kabisa kwamba hizi Halmashauri zinalalamika kwamba katika mgao wanaopewa ni mdogo sana ambao haukidhi haja. Kwa hivyo, huu ufinyu wa bajeti unachangia mambo mengi yasiweze kutekelezwa vizuri wakati wao wameshaandaa malengo yao.

Mhe. Mwenyekiti, kwa Wilaya ya Kusini vile vile wao wameeleza pamoja na ufinyu wa bajeti walikuwa na matatizo ya usafiri. Hilo tumeliona na vile vile walikuwa na uhaba wa wafanyakazi. Kwa hivyo, ningelimuomba Mhe. Waziri katika haya malalamiko ya Halmashauri tatu hizi Kaskazini "A", "B" na Wilaya ya Kati wajaribu kuwasaidia, ili waweze kupunguza matatizo yao.

Mhe. Mwenyekiti, nikitaka nizungumzie suala la hao wazee ambao wanapata malipo madogo; kwa kweli watu wakishakuwa wazee wanahitaji kusaidiwa na tumepata malalamiko kwamba kipato wanachokipata ni kidogo sana ambacho hakiwezi kukidhi haja ya maisha. Kwa hiyo, ningelimuomba Mhe. Waziri hawa wazee wanaopewa huo mchango kidogo wa kusaidiwa saidiwa katika maisha yao wasaidiwe kwa kuongezwa kwani mchango wanaopewa ni mdogo sana, ambao hauwezi kukidhi maisha. Tatizo hili si hao tu hata wale ambao wanapata pensheni pia ni ndogo sana ambayo hiyo wakiipata ni nauli ya kufika huko wanakokwenda kuchukua pesa zao. Kwa hivyo, hilo ningelimuomba Mhe. Waziri akalifikiria.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, nataka nizungumze kuhusu Baraza la Manispaa. Mimi nataka niseme kwa uhaki kabisa kwamba Baraza la Manispaa wanakabiliwa na uhaba wa wafanyakazi, jambo ambalo linarudisha nyuma maendeleo yao na ya nchi kwa ujumla. Watu wakiwa kidogo katika ofisi ambayo inataka kufanya kazi basi maendeleo hayawezi kupatikana. Mhe. Waziri napenda nikuulize huu upungufu wa wafanyakazi unahitaji watu wangapi na kwa bajeti ya mara hii unategemea kuajiri wangapi?

Jambo jengine Mhe. Mwenyekiti, nataka nizungumzie juu ya usafi wa mji, mji wetu bado haujafikia *standard* ya kusifiwa kwamba mji ni safi kabisa, pamoja na jitihada za Manispaa na waziri mwenyewe ana mikakati mizuri sana lakini bado hali ya usafi haujaridhisha. Kwa hivyo, pamoja na upungufu wa magari ambao naona kwa jitihada za Mhe. Waziri tunategemea labda mwezi wa *June* kupata magari mengi yakuweza kutusaidia kufanya usafi wa mji wetu tujitahidi sana.

Pia ninalolifikiria zaidi ya hilo ni suala la namna jamii yetu katika kubadili tabia ya usafi. Suala hili Mhe. Waziri nataka ulivalie njuga kidogo ili kuona namna gani jamii inaweza kubadilika mpaka jamii yetu iweze kuona kwamba usafi ni suala muhimu. Kwa hivyo, linavyojitokeza ni kwamba kila mtu hana wasiwasi kutupa taka ovyo nje ya majumba. Kwa hivyo, sisi wanzibari sehemu ya mjini hapa au sehemu nyengine zote hatujawa na utamaduni mzuri wakuweka usafi wa mji wetu.

Kwa hivyo, pamoja na mashirikiano mazuri ambayo mliyonayo ya watu wako lakini vile vile naomba kwamba elimu iweze kutolewe, itolewe kama vile wanavyotoa madaktari. Madaktari wa afya mara nyingi wanapokuwa na matatizo au haja kwa wananchi wanapita katika majumba nyumba baada ya nyumba kueleza hili na hili, kwa nini sasa na sisi hatuchukui nyayo za watu wa afya tukapita katika majumba yale pamoja na vikundi ambavyo mnavyo; vikundi vya usafi.

Mhe. Mwenyekiti, nilitaka nizungumzie eneo la darajani; nataka nimuulizie Mhe. Waziri ni lini eneo la Darajani litajengwa maduka ya kisasa. Mji uweze kumeremeta tujue hasa hii *Zanzibar Town* iko wapi? Tunausubiri kwa hamu kwa sababu ukimuuliza mtu hapa Mjini Unguja ni wapi, mtu hana jibu. Kwa hivyo, tunakuomba Mhe. Waziri tunataka huu mji wa Darajani uupambe kwa sababu maneno yameshakuwa mengi.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo ninahitaji kuzungumza ni suala zima la vitambulisho vya uzanzibari ukaazi. Namuomba Mhe. Waziri mimi nakubali kwamba vitambulisho viko vingi sana katika ofisi za Wilaya zetu, na vitambulisho hivi bado havijachukuliwa. Sasa mimi Mhe. Waziri nikitaka nizae fikra tu katika suala hili. Hii kila siku kuleta takwimu kwamba hawendi kuchukua vitambulisho ni kwa sababu ya hali ngumu ya kimaisha ya watu wetu. Hawana fedha za kupanda magari kila siku wakenda wakachukua hivyo vitambulisho vyao. Kwa hivyo hivi vitambulisho ili viweze kupunguzwa katika Halmashauri zetu za Wilaya tuweze kuweka utaratibu wa magari kama vile tunapofanya Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, tunawafuata wananchi sehemu waliko. Nafikiri tukienda mara moja tu vitambulisho hivyo vyote vitakwisha, lakini kwa mtindo ulioko sasa na taarifa tulizonazo ni kwamba vitambulisho viko vingi sana, watu hawajenda kuvichukua.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nizungumzie juu ya Vikosi Maalum. Vikosi hivi kwa kweli ni vya taifa letu na vina kazi ngumu sana, hawa ni walinzi wa taifa letu la Zanzibar tukitaka tusitake wanafanya kazi ngumu na wanaishi katika maeneo yao kwa hali ambayo si nzuri. Kwa sababu hawa ni binadamu na wengine wanakuwa na wake zao, wanakuwa na watoto wao, lakini maeneo ambayo wanaishi askari wetu sio mazuri. Haya ni mambo ya stara mke na mume na watoto. Kwa kweli maisha yao sio mazuri vinahitaji vikosi vyetu hivi viwekwe maeneo ambayo mazuri sana yatakayowaridhisha.

Pia nataka niseme kwamba hawa wasaidiwe wawe na mishahara yao mizuri kwani sasa ni midogo, kiasi ambacho ukilinganisha mishahara ya vikosi vyetu hivi na vikosi vyengine vya Tanzania Bara utakuta hawa mishahara yao midogo sana wakati nao ni walinzi.

Sasa mimi nitatoa hoja nyengine ambazo sio dhaifu na ambazo zinaweza zikamfanya Mhe. Waziri akaona umuhimu wa watu hawa na wakapata mahala pazuri pa kukaa na mishahara minono. Kwa mfano, hivi vikosi vyetu vina kazi kubwa sana, wakati linapotokea janga la moto popote pale basi vikosi vyetu vinafika, ikiwa moto ule ni wa nyumbani, ikiwa moto ule umetokea wa magari, kwenye misitu au athari ambazo zinawapata vijana wetu za kutumbukia ndani ya visima, kazi ile inafanywa na vikosi vyetu. Je, haijawa sababu muhimu ya kuona kuwa hawa watu ni muhimu?

Jengine wanafanya kazi za amali katika kusaidia uchumi wa nchi yetu. Je, haijawa sababu nyengine ya kusaidiwa watu hawa? Pia hatuoni sababu nyengine kwamba vikosi vyetu wanatoa ulinzi wa taifa letu, tukapata usingizi mnono, hilo si jambo dogo.*(Makofi)*

Vile vile tusisahau wakati vikosi vyetu ni waokozi ikitokea ajali na ajali ziko za namna nyingi; inaweza kuwa ajali ya ndege haraka wamefika, ikiwa ajali ya mabwawa pia, na ajali za aina yoyote watu wetu hawa wako tayari.Je, hazijawa sababu za kutosha kwamba hawa wana kazi ngumu?

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hilo jengine ni kwamba hawa ni watu ambao wanalinda rasilimali za taifa letu. Mtu kulinda rasilimali zetu bila ya kuiba hilo si jambo dogo na ulinzi kila pahala askari wetu wanagawiwa. Mimi naona magari kila dakika wanateremshwa hapa na pale, hiyo ni kazi kubwa hawalali na familia zao.

Mhe. Mwenyekiti, tuone kwamba ulinzi unafanywa kwa wanafunzi walioko katika Chuo chetu cha Mafunzo, wana kazi kubwa sana ya kulinda watu wale waliomo ndani, watu ambao takriban wameshakata tamaa ya maisha, watu ambao wamefanya vitendo vingi vya uhalifu, bado askari wetu wana kazi kubwa sana ya kuwalinda hawa; mambo yote wanayo wao.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri kazi yao ni kubwa sana, tuangalie pia doria ambayo wanaifanya, doria zinafanywa katika bahari, katika kulinda magendo na mambo mengine, yote hayo yanafanywa na askari wetu. Vile vile wanafanya doria katika nchi kavu kuona kwamba ulinzi umekuwa mzuri.

Mhe. Waziri katika hayo yote nafikiri yanatosha kuonesha kwamba kazi walizonazo ni ngumu, maisha yao ni dhaifu na tusiwafanye askari wetu wawe sugu kama vile mtoto kumpiga sana. Mtoto ukimpiga sana tunasemna *difficult child*, mtoto sugu. Sasa na hawa tusiwafanye kuwa na maisha haya, wakija wakibadilika kwa njia nyengine tusije kuwalaumu kwamba askari wetu wanafanya vitendo vilivyokuwa si vizuri. Mimi nasema njia nzuri ni kuwawezesha askari wetu wakapata maisha bora kwa sababu wao ni wananchi wa Zanzibar na wanatusaidia Zanzibar yetu kutulinda. Mishahara yao ni midogo Mhe. Waziri, linahitaji suala hilo kama kuna *scheme of service* wafanyiwe na wao wajisikie.

Hata tunapokuwa tunawatembelea wanakuwa wanyonge sana. Hawa wanafanya kazi kubwa ya ujenzi, wametuonesha katika nchi hii kwamba askari wetu ni wajenzi wakubwa sana, tumepita kuona skuli za sekondari wanazojenga tena za ghorofa. Hiyo ni sifa kubwa sana tuliyonayo ambapo askari wetu hawana kazi moja wana kazi namna kwa namna kulisaidia taifa hili. Kwa hivyo, kama wao wamejitolea katika kufanya kazi zile kwa ajili ya taifa hili, kwa nini na sisi hatufanyi jicho la huruma tukawasaidia, kuna kosa gani walilofanya watu hawa kwa miaka yote. Mhe. Waziri, *for having sake, please I beg you* hawa watu uwaone kwa jicho la huruma.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, ahsante naunga mkono.

Mhe. Farida Amour Mohammed: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii ya kutoa mchango wangu katika hotuba ya Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ.
Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijaalia akanipa afya njema kufika hapa katika ukumbi huu na nikasimama mbele ya Baraza lako tukufu. Pia nimshukuru sana Mhe. Waziri na kumpongeza kwa dhati kabisa jinsi alivyotoa hotuba yake na tumeifahamu. Pia nikushukuru wewe Mwenyekiti kwa kunipa nafasi jioni hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nianze moja kwa moja katika Mkoa wa Kaskazini Pemba, katika kuanza kwangu naomba nipongeze mashirikiano yaliopo baina ya wananchi wa Mkoa wa Kaskazini Pemba kwa namna wanavyoshirikiana katika kufanya shughuli zote za maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, nasema haya kwa sababu mfano mzuri unajionesha kwamba watu hawa wana mashirikiano mazuri, bila ya kujali itikadi zao za vyama vya siasa ni katika kufanikisha Sherehe za Mapinduzi ya miaka 50. Katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa pamoja na Mkuu wa Wilaya mwenyewe wa Kaskazini Pemba aliwashirikisha vijana wote, wananchi wote, katika shughuli zote za uzinduzi wa miradi ya maendeleo katika Mkoa huo wa Kaskazini Pemba. Kwa bahati nzuri sana watu wamemkubali wananchi wameitikia wito huo. Sasa katika hili matumaini yangu ni kuwa hatua hizo zitaendelea zaidi katika kushirikiana kwa ajili ya kutafuta maendeleo ya Mkoa wetu wa Kaskazini Pemba.

Katika hilo naomba Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kama mwenye dhamana ya maendeleo ya Mkoa wa Kaskazini Pemba, ajue kwamba kukosekana kwa usafiri wa meli kutoka Bandari ya Wete kunadhorotesha maendeleo na biashara na kiuchumi katika eneo letu la Wilaya ya Wete au Mkoa wa Kaskazini kwa jumla.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niwafahamishe viongozi wa Mkoa wa Kaskazini Pemba kwamba maendeleo ya Mkoa wa Kaskazini ya kijamii yanaletwa na ofisi hii ya Mkuu wa Mkoa na wao ndio dhamana wa shughuli hii. Sasa hapa nina swali au masikitiko kidogo, baada ya kuzama kwa *MV. Spice* Pemba imekuwa imezama na bandari pia? Viongozi hawa wa mkoa wamekaa kimya tu, naomba nimuulize Mhe. Waziri katika hili uongozi wa Mkoa wa Kaskazini Pemba umechukua jitihada gani za kuhakikisha angalau ile bandari pale inafufuka na kutafuta angalau mfadhili wa aina yoyote au kwa njia yoyote kuleta meli nyengine, kwa ajili ya kuleta maendeleo na ajira kwa wananchi wetu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, kiukweli Mkoa wa Kaskazini ndio mkoa unaotoa vitu vingi, biashara nyingi, watu wengi kutoka mkoa huo na hata wanaotoka Kusini baadhi yao biashara zao zilikuwa zinashukia pale. Kwa bahati mbaya sana ni makadirio ya Mwenyezi Mungu baada ya kuzama ile meli imekuwa tena hakuna ile bandari, hakuna lolote lile linalofanyika wala hakuna hatua inayochukuliwa katika kutafuta angalau maendeleo ya wananchi wetu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Kwa hiyo, namuomba sana Mhe. Waziri kupitia ofisi za Mkoa wa Kaskazini Pemba waliangalie hili kwa jicho la huruma. Wananchi wa Mkoa wa Kaskazini Pemba ni wafanyabiashara sana kwa hivyo wahurumiwe katika

kuwatafutia angalau wafadhili kutafuta japo kiboti chengine kidogo kitakachowafanya wafanyabiashara wetu wakafanikiwa katika kutafuta maisha.

Mhe Mwenyekiti, sasa naomba niendelee katika Mkoa huo huo wa Kaskazini Wilaya ya Wete katika Baraza la Mji na Halmashauri za Wilaya; hizi sio za Wete peke yake ni kwa Zanzibar nzima. Mheshimiwa hapa pana kilio cha muda mrefu sana cha watendaji wetu hawa Madiwani, ambapo suala hili nalizungumzia kila bajeti na leo pia nitaendelea kulizungumza mpaka Mwenyezi Mungu awajaalie viongozi wetu wafanikiwe kulitekeleza hili.

Mhe. Mwenyekiti, nakumbuka katika miaka yote tunafanya chaguzi tano, uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, uchaguzi wa Rais wa Zanzibar, Mwakilishi, Mbunge na Diwani. Madiwani wanafanya kazi za ziada, wanafanya kazi za kuwaunganisha watu katika majimbo na mawilaya yao, wanafanya kazi kubwa ya ukusanyaji mapato, lakini kwa bahati mbaya sana bado serikali haijawaona madiwani.

Jamani tuwaoneeni huruma madiwani wetu na wao angalau wasisubiri posho kila baada ya vikao, Waswahili wanasema: "Mcheza kwao hutunzwa", hawa watu jamani wanafanya kazi za ziada ya kukusanya, ya kulinda na kufanya kila kitu waonewe huruma Madiwani wetu angalau na wao wajisikie kama wamo katika *group* la watu wanaofanyiwa uchaguzi wa halali.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye Baraza la Mji wa Wete. Baraza la Mji wa Wete kuna malalamiko na malalamiko haya ni yale yaliyotokana na uvamizi wa eneo la soko la Mji wa Wete. Baraza la Mji wa Wete linamiliki kiwanja nambari 226 kilichopo Soko la Wete na ni mali ya Baraza la Mji na kimo katika mradi wa ujenzi wa soko kwa ufadhili wa Benki ya Dunia. Chakusikitisha, eneo hili limevamiwa na bwana Ahmed Abdalla Salim wa Kitutia, Wete kwa madai kuwa kapewa na Baraza la Mji mwaka 1994. Bwana huyo ameshazungusha uzio wa mabati kwa ajili ya kukitumia kiwanja kile wakati eneo lile ni eneo la soko la Baraza la Mji wa Wete.

Mhe. Mwenyekiti, hapa nitaomba maelezo, kwa sababu Madiwani wenyewe wa Baraza la Mji hawajaridhika na uchukuaji wa eneo hili kupewa bwana huyo. Sasa naomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa anipe maelezo ya kutosha yatakayonifanya mimi niridhike kwa nini na ni kwa vigezo gani na ni nani aliyepewa eneo hili kumpa bwana huyu.

Mhe. Mwenyekiti, katika eneo hili limepimwa zamani na hii ni hadithi na ni nyimbo ya muda mrefu kuwa panataka kujengwa soko kwa huyu mfadhili wa Benki ya Dunia. kwa bahati mbaya ndio kuna mtu tayari keshalizunguushia uzio wa mabati, kwa ajili ya matumizi yake mwenyewe binafsi, hatujui kwa nini.

Sasa tuseme ikiwa tayari hizo pesa za wafadhili zipo na nina imani pesa zipo katika ujenzi huo na katika kitabu hiki nimeona eneo lililosema kuna ukarabati, ninavyofahamu mimi toka nyuma ni ujenzi, sasa hata kama ni huo ukarabati basi unatakiwa uwe mkubwa kwa sababu soko lile eneo ni kubwa litafanywaje wakati pale pana mtu tayari keshadhibiti lile eneo. Mhe. Waziri namuomba sana katika hili awaonee huruma watu wa Wilaya ya Wete eneo lao hili lirudi kwa wenyewe wahusika wa Baraza la Mji wa Wete, ili kitakachofanyika pale kiwe ni kwa maslahi ya wananchi wote wa Wilaya ya Wete na Mkoa wa Kaskazini kwa jumla. Sitokubali kupewa majibu yasioridhisha katika hili kwa kupewa mtu, kunyang'anywa eneo lile Baraza la Mji kupewa mtu binafsi. Naomba majibu ya kina Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa niingie kidogo kwenye ulinzi katika sehemu za watalii. Ulinzi ni kitu muhimu na watalii ni tegemeo letu, lakini kuna matukio kama walivyozungumza wenzangu ya kutisha sana yanayotokea kwa watalii wetu hawa ambao ndio wanatuwezesha katika mambo mengi, wanatuingizia mapato. Mheshimiwa yanatokea mambo ya maajabu, Wazungu wanauliwa wakatiwa ndani ya visima, wengine wanamwagiwa tindi kali, hivi kweli Mhe. Waziri suala kama hili wageni wetu hao watakuwa na imani kweli ya kuja hapa?

Halafu tutalalamika mapato hayaongezeki kwani watakuwa wana hofu kuja. Kwa sababu katika watu walio na woga ni hawa wageni wetu wanaokuja hapa. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri anieleze wizara yake imejipanga vipi na ulinzi katika maeneo haya wanayozunguka wageni wetu ambao ni tegemeo letu kwa kutuingizia mapato.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niingie katika sifa za mji. Sifa za kuitwa mji, mji unatakiwa uwe na barabara na barabara zile za ndani zote angalau ziwe za kuridhisha. Mhe. Mwenyekiti, bado inaonesha barabara zetu za ndani

hazijawa na mwelekeo mzuri, bado zina mashimo, zina madimbwi, uchafu mtupu na ukiangalia pesa zipo katika Mfuko wa Barabara. Sasa hapa naomba anielimishe kidogo Mhe. Waziri, hivi hawawezi kushirikiana hawa Baraza la Mji pamoja na ule Mfuko wa Barabara kwa kutengeneza baadhi ya barabara hizi za ndai angalau mji wetu ukaonekana mzuri?

Mhe. Mwenyekiti, na mimi sitokuwa mwinzi wa fadhila lazima niwapongeze sana Vikosi vyetu vya SMZ. Waswahili wanasema kwamba: "Mtu bwana huitwa kwao", sasa hivi vikosi vyetu vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar vinafanya kazi ya ziada, vinafanya kazi ya kulinda wananchi, kulinda mali za wananchi, vinajitolea usiku na mchana, watu wanalala majumbani kwao wenzetu hao wanahangaika, lakini bado mishahara yao haijaridhisha.

Kwa hivyo ninaomba sana kwa sababu hawa vijana wetu bado na wao wanahitaji kutufanyia kazi na sisi bado tunaridhika na kufanyiwa kazi na vijana hawa. Basi lazima na sisi tuwaangalie vizuri ili na wao waweze kutulia na kufanya shughuli zao kwa ufanisi zaidi. Vyenginevyo wakiona wenzetu Polisi wa hapa hapa Zanzibar lakini kwa sababu wao wameshirikiana na Muungano wanapata mishahara mikubwa na ukitizama kazi zao wao ni ndogo sana ukilinganisha na kazi wanazofanya vikosi vya SMZ, hapo tutakuwa hatuna la kuwalaumu, vijana wetu ni wasikivu, watulivu, lakini bado hatujawatizama kwa jicho la huruma.

Mhe. Mwenyekiti, vikosi hivi hivi vya SMZ wana uhodari wa kubuni baadhi ya mambo. Kuna kikosi kimoja kama sikosei sijui JKU au KMKM wana viwanda vyao wenyewe vya kutengeneza viatu, lakini sasa wanahitaji kuwezeshwa ili wapate kuongeza ile miradi yao angalau wapate mafanikio zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, nimeona katika kitabu hiki nilikuwa na kesi kubwa kuhusu Idara ya Zimamoto, Pemba. Ni kweli kwamba Pemba Kusini pana Kituo cha Zimamoto, lakini pia tuelewe kwamba kutoka Kusini kwenda Kaskazini ni masafa kiasi fulani na inapotokea maafa ni tatizo. Kipindi cha karibu Mhe. Mwenyekiti unafahamu yalitokezea maafa makubwa ya moto Kaskazini Tumbe/Micheweni na athari iliyotokea ni kubwa mno, gari itoke Chake Chake mpaka ifike Micheweni ni hatua. Sasa Mhe. Waziri niliona katika kitabu chako kama kuna malengo ya kujenga Kituo cha Zimamoto Kaskazini Pemba. Nakuomba sana Mhe. Waziri hili isiwe hadithi, ikawa kila siku tutajenga, tutajenga. Nakuomba sana katika hili ulifikirie na ulipe kipaumbele kwa sababu kama unavyojua mazingira yetu na majumba yetu ya kimaskini yalivyo, na ujenzi wetu ulivyo, ikitokezea maafa dakika 20 hazitimii nyumba zote zinateketea. Kwa hiyo angalau kile kituo kikiwepo karibu kitawasaidia, lakini kituo kikiwa mbali mpaka wakifika kule hamna tena kitu. Mhe. Waziri katika hili naomba uliangalie kwa jicho la huruma.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache naunga mkono bajeti hii lakini namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa anifahamishe kuhusu kiwanja namba 226 kilichopo sokoni Wete, kilichokuwa ni mali ya Baraza la Mji ambacho kimechukuliwa na mtu binafsi nipate majibu ya kuridhisha. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kutoa mchango wangu mdogo katika Wizara hii. Kwa kuanzia nataka nianze na Baraza la Manispaa.
Kwanza nataka niwapongeze Baraza la Manispaa kwa juhudi zao za kutengeneza miundombinu ya usafi. Moja kati ya kero kubwa katika mji wetu wa Zanzibar ilikuwa ni kutuama kwa maji machafu hasa siku za mvua. Kuna mradi mkubwa ulianzishwa wa kutengeneza mitaro ile ambayo kama ungefanikiwa vizuri tungefanikiwa sana kuyaondosha maji ya mvua kwa haraka sana katika Mji wa Zanzibar.

Katika hili Mhe. Mwenyekiti, nataka nitoe nasaha zangu kidogo kwa wananchi wenzangu wa Zanzibar. Unajua nchi haiwezi kupata maendeleo kama wale wananchi wenyewe hawajali maendeleo. Nasikitika mitaro ile baada ya kujengwa tu basi haikuchukua muda ilianza kuziba na haikupaswa kuziba kutokana na ile hali ilivyokuwa. Ilikuwa mikubwa ya kutosha kabisa na ingeweza kufyonza maji yote ya mvua kwa wakati muafaka. Kutokana na wananchi kuwa hawajazingatia vizuri maendeleo ya nchi yetu ikawa wanatupa taka ovyo ndani ya ile mitaro, matokeo yake kana kwamba sasa haifanyi kazi vizuri. Kwa hiyo nilikuwa naomba nichukue nafasi hii kuwanasihi sana wananchi wenzangu wa Zanzibar yale maendeleo ambayo wenzetu wanajitahidi kutufadhili, ule ni mradi tulifadhiliwa kwa pesa nyingi sana, basi tuoneshe kuzijali zile pesa za wenzetu.

Wale wenzetu wanatufadhili pesa zile wanalipisha kodi huko kwa wananchi wao ndio wanatuletea sisi, kwa hiyo na sisi tuoneshe kuzitunza. Lakini leo tukiwa hatujali chochote, kwa kweli nchi yetu haitafikia maendeleo siku zote

tutakuwa tunaomba omba na tukitizama tupo pale pale hatwendi mbele. Kwa hiyo moja ni hilo nilikuwa nataka niwanasihi wenzangu tujitahidini sana misaada tunayopewa tuijali, tung'arishe mji wetu kwa uzalendo kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine soko la Mombasa ni chafu sana na siku za mvua huwezi kupita hata mle ndani. Kana kwamba lile soko halikuwa tayari kuhamiwa. Yaani tumewahi sana kulihamia likiwa halijafikia matengenezo mazuri. Sasa ikinyesha mvua mle ndani hamkaliki inakuwa ni uchafu, na kwa sababu ya uchafu ule wale wafanyabiashara hawakai mle ndani wanahama. Matokeo yake wanakuja kukaa huku barabarani, wanajenga vibanda vyao wanafanya biashara, jambo ambalo kwa upana wa lile soko wote wangeweza kukaa mle ndani.

Sasa Manispaa hapa hamjafanya vizuri na nilikuwa naomba sana mjitahidi kutengeneza zile sehemu za ndani mle, ili wafanyabiashara wapate mazingira mazuri ya kuweza kufanya kazi zao mle ndani na hata mteja nae apende kwenda mle ndani. Vyenginevyo hata huyo mfanyabiashara akikaa ndani ya matope namna ile mimi siendi kule nitatafuta soko jengine niende. Kwa hiyo naomba sana Manispaa walizingatie hili na bahati mbaya sijaliona katika malengo yao ya kuliimarisha soko lile.

Kwa sababu hiyo sasa hata wale wafanyabiashara wengine wameanza kuona kama pale hawapati wateja na wameanza kukimbia, kwa hiyo makusanyo ya soko lile hayafikii, lile lengo ambalo limekusudiwa. Sasa ili kurudisha haiba ya lile soko inafaa litengenezwe vizuri, wafanyabiashara wavutike kwa sababu na wateja nao watakuwa wanavutika, ili yale makusanyo yaliyokusudiwa kukusanywa kwa soko lile yaweze kupatikana kama yalivyopangwa.

Jambo jengine kuhusu Manispaa. Mhe. Mwenyekiti, malengo ukifungua kitabu hiki cha pili cha Mhe. Waziri ukurasa wa 3 kuna malengo ya Manispaa ya mwaka 2013/2014 ambayo makisio yao ilikuwa ni kukusanya bilioni 2,743,140,580/=. Lakini ukija kwenye makusanyo halisi ya utekelezaji wamekusanya bilioni 1,317, 063,132/=. Hiyo ni kasoro ya malengo kwa bilioni 1,426,077,448/=. Sasa hii ni kasoro kubwa sana Mhe. Mwenyekiti, sijui makisio yao walikosea wapi. Lakini hii ni kasoro ambayo kwa kweli inaharibu bajeti nzima ya Manispaa. Kwa sababu Manispaa wanakusanya ndio wanaotumia. Sasa ukiona kasoro ya bilioni 1.4 ni kasoro kubwa sana.

Sasa lazima wakiri kwanza hapa wamefanya kosa kubwa sana kwenye *projection* ambayo hawawezi kuifikia. Nilitaka kuona mara hii wangefanya makisio namna gani lakini bahati mbaya hawakueleza. Sijui kwa nini mara hii hakuna makisio ya makusanyo. Sijui tutawaidhinishia kitu gani, maana sioni mimi humu. Kama hakuna makisio Mhe. Mwenyekiti, maana yake watakachokifanya hakitakuwa halali, maana Baraza hili halitapata kuidhinisha hayo makusanyo ambayo wanakusudia kukusanya hayakuelezwa humu, ni kasoro nyengine hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo niende ukurasa wa 18 wa kitabu hiki pale kuna Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi. Mhe. Mwenyekiti, mara hii Halmashauri ya Wilaya imefanya vibaya sana na si kawaida yake sijui kuna nini. Lakini walituomba idhini ya kukusanya milioni 800, walichokikusanya ni milioni 537.4. Napo hapa pana kasoro kubwa sana. Sasa sijui watueleze wamefeli wapi Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi. Halmashauri moja nilikuwa naisifu sana kwa makusanyo lakini mara hii wamerudi nyuma sana.

Halafu kilichonitisha zaidi ni kwamba walikuwa na makisio ya kukusanya milioni 800 wakakusanya 500, mwaka huu wanaomba wakusanye milioni 950. Hebu watwambie watafanya miujiza gani mpaka wafike huko. Mimi nilikuwa nadhani tusiwaruhusu maana watakuwa wanatudanganya hawana uwezo huu, au watupe maelekezo mazuri kwamba wameongeza kodi gani, wameongeza ufanisi gani watoke kwenye 500 mpaka 950. Vyenginevyo kama sijaridhika mimi nitakuwa siruhusu makusanyo haya.

Mhe. Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "A" wao walisema watakusanya milioni 177, wamekusanya milioni 139 kidogo afadhali. Ukienda kwenye malengo ya mwaka 2014/2015 wanasema watakusanya milioni 295. Sasa ikiwa kule hawakufikia lengo, hivi kweli wataweza kuzipata milioni 295 hebu atueleze kidogo ana mipango gani.

Mhe. Mwenyekiti, hiyo ni mifano michache ya Halmashauri za Wilaya za Unguja. Sasa ukenda Pemba kuna tofauti kidogo, kule wao wamepita asilimia 100. Kwa mfano, Baraza la Mji Mkoani waliweka makisio ya kukusanya milioni 40 lakini wakakusanya milioni 52, sasa hii kidogo inatia moyo. Kwa hiyo hawa wakiomba kufanya zaidi ya milioni 52 mimi nitakubali kwa sababu wamevuka malengo, na wameweka hapa watakusanya milioni 70. Ukenda

Halmashauri nyengine vile vile utakuta kuna ongezeko. Sasa nadhani niwaombe Halmashauri za Unguja zikae na wenzao kule Pemba tuone wanaweza kuwasaidia nini, ili wafikie malengo au ikiwezekana wavuke malengo waliyojipangia.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo kwenye Serikali za Mitaa sasa naomba niende kidogo kwenye Idara Maalum. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nilikuwa najiuliza mimi hizi Idara Maalum ambazo zinaongozwa na Makamanda, na ulimwengu mzima Makamanda wanaongoza majeshi, wanaongoza vikosi. Kuziita Idara Maalum si kuvidhalilisha vikosi vyetu? Maana yake Idara inaongozwa na Mkurugenzi. Lazima tujiulize hasa kwani tunaogopa nini kuviita vikosi. Zamani vilikuwa vinaitwa vikosi hivi, ni vikosi; vina majeshi na silaha, vinatoa mafunzo ya kijeshi, vinaongozwa na Makamanda, ni vikosi. Kwa nini tuite Idara Maalum. Mimi nadhani bora turudie jina lile lile la vikosi, kama kuna kasoro za kisheria, kuna kasoro za kikatiba nadhani tuzirekebishe lakini tuviite vikosi vinafanya kazi za kijeshi.

Mhe. Mwenyekiti, vikosi vyetu vina hali mbaya wenzangu wamesema hapa na mimi nataka niongeze. Kwa kweli vikosi vyetu vina hali mbaya majengo yao ukenda ukiyaangalia hayaridhishi, na huko yalipo hakuna miundombinu ya barabara, wana tatizo la maji, wana tatizo la umeme, wana kila aina ya mashaka. Sasa niungane na wenzangu kuiambia Serikali kwa kweli hawajavitendea haki vikosi. Ukija kwenye mishahara yao ndio kabisa wapo taabani kweli kweli.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu ya Katiba, Sheria na Utawala ndio inapita humu kwenye vikosi. Tumewahi kupita kwenye vikosi maana yake wale watu kwa vile ambavyo hali zao ni dhalili wakatwambia maneno kana kwamba ile mishahara tunaitoa sisi tukiwapa wao. Unafika pahala unakaribia kuwalaumu kwa nini mnasema maneno hayo, lakini ni kutokana na hali yao ngumu. Kwa hiyo naomba sana Mhe. Waziri ufanye juhudi za ziada kuhakikisha kwamba vikosi vinaongezwa maslahi, vikosi vinapata pahala pazuri pa kukaa, vikosi vinapata unifomu nzuri.

Halafu kikosi cha JKU wamebuni mradi mzuri sana pale ambao ukikamilika utaweza kuwasaidia wao wenyewe kwa kuzalisha. Wameanzisha ujenzi wa skuli ya ghorofa tatu, wakimudu watasomesha watoto pale mpaka sekondari. Nashangaa mpaka leo Serikali haijaweka *input* yoyote pale wanatumia *other charges* na askari wao kuendeleza lile jengo. Wamekamilisha ile *floor* ya chini sasa wanataka kunyanyua juu, nilidhani mara hii ningeona pesa ya maendeleo humu, lakini wametiliwa pesa ya maendeleo shilingi 150 milioni kwa ajili ya mradi wa mboga mboga, hili jengo halina kitu kwa nini. Wakati wenzao pale KMKM walipokuwa wanajenga hospitali kila mwaka kulikuwa na milioni 300, milioni 200 mpaka hospitali imekamilika. Hata mwaka huu kuna milioni 15,300 kwa ajili ya kuanzisha *phase II* ya ile hospitali. Lakini kwa nini JKU hawaongezwi hizi pesa, hawatiliwi na wao mradi ule wanakauka damu wenyewe tu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nizungumzie Chuo cha Mafunzo. Ni kituo cha mafunzo kama kinavyoitwa, zamani ikiitwa hii jela, lakini Marehemu Muasisi Mzee Abeid Amani Karume akasema hapana tusiite jela tuite chuo cha mafunzo, kwa maana kwamba tunakwenda kuwarekebisha watoto tabia ili wakitoka wawe wazuri ndio malengo yake.

Mhe. Mwenyekiti, Chuo cha Mafunzo kuna kasoro mbili; kasoro ya kwanza mimi nadhani si vizuri kusema lakini watoto wakienda pale ndio wanaharibiwa zaidi. Mimi ni mdau na siku nyingi huwa napenda kusema hivyo, ni mdau kule Chuo cha Mafunzo nimeshawahi kwenda, na niliyoyakuta Mhe. Mwenyekiti, si mazuri. Kwa sababu badala ya kumrekebisha mtoto tabia ndio unamharibu zaidi. Niligundua watu wanauza bangi mle ndani, sasa ikiwa kijana aliyekuwa huku nje anavuta bangi halafu unakuja kumvutisha bangi akitoka mule atakuwa vipi, si ataendelea tu. Nadhani wawepo *serious*, madhumuni ya chuo kile ni kurekebisha tabia, kwa hiyo wale askari wanaoshughulika na mahabusu na wanafunzi kule ndani hebu waache huo mtindo si mzuri. Sasa hilo ni jambo moja ambalo halibadilishi tabia.

La pili hiki chuo ni maskini sana hakina pesa, hakina miundombinu ya kuwasaidia wale wanafunzi. Maana tulitarajia mle muwe na *workshop, carpentry, electricity, mechanic,* ili wale watoto kama nje walikuwa hawana kazi ya kufanya ndio maana wakaiba wakenda mle wapewe ule ujuzi, wapewe utaalam. Kama mtu anakuwa fundi mwashi, fundi umeme, fundi bomba, akitoka anaweza kujitegemea ndio malengo ya kile chuo. Lakini leo chuo kile hakina hata jengo moja la kufanya shughuli kama hizo halafu unasema unarekebisha tabia, unarekebisha tabia vipi.

Sasa mimi naomba sana Mhe. Waziri Serikali kama malengo ni kurekebisha tabia za watoto wa Kizanzibari basi hebu akiangalie chuo kwa nini kinarudi nyuma sana, kipatiwe fedha ya kutosha wajenge majengo yatakayoweza kutoa mafunzo, wapewe zana waweze kuwasaidia watoto. Lakini kurekebisha tabia kwa jembe tu, jembe watu wengi hawalipendi, atatoka mle ameshalimishwa akirudi nje haji kulima tena, maana ni ajira lakini kwa kweli ni adhabu. Sasa nilikuwa naomba hilo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo machache mimi sina tatizo sana nikishapata ufafanuzi wa namna gani Halmashauri za Wilaya hasa za Unguja zinaweza kufanikisha makusanyo waliyoyaandika humu, nikiridhika kwamba kweli wana vyanzo vya kutosha basi mimi sina tatizo na bajeti hii. Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe nichukue fursa hii kuwashukuru sana kwa kweli kwa utulivu wenu na michango yenu. Kwa hiyo sasa tunaakhirisha kikao chetu mpaka Jumatatu tarehe 02/06/2014 saa 3:00 asubuhi.

(Saa 1:40 usiku Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 02/05/2014 saa 3:00 asubuhi)